ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tisa – Tarehe 15 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako, naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 98

Tatizo la Usafiri kwa Wanafunzi wa Vyuo Vilivyo Nje ya Mji

Mhe. Fatma Mbarouk Said – Aliuliza:-

(a) Kwa vile takriban ya Vyuo Vikuu vitatu sasa viko nje ya mji (Tunguu) na tatizo kubwa linalowakabili wanafunzi ni usafiri. Je, serikali ina mpango wowote wa kuwasaidia usafiri wanafunzi hawa.

(b) Kwa hesabu za haraka wanafunzi hawa wanatumia shilingi 12,000/= kwa mwezi, wakati kama wangepatiwa usafiri wangeweza kupata nafuu. Je, serikali inalichukulia tatizo hili kwa kiasi gani katika kulitafutia ufumbuzi.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusu yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 98 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba Vyuo vyetu Vikuu vitatu vilioko nje ya mji, ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*), Chuo Kikuu cha Zanzibar ambavyo vyote viwili viko Tunguu na Chuo Kikuu cha Ualimu kilichoko Chukwani, ambavyo vyombo hivi vinapata usafiri wa uhakika kwa kutumia daladala ambazo zinafanya safari kwa wakati unaohusika.

(b) Mhe. Spika, ni kweli kuwa wanafunzi wanatumia wastani wa shilingi 12,000/= kwa mwezi kwa ajili ya usafiri. Kwa kutambua hilo Bodi ya Mikopo ya Zanzibar kwa kuanzia mwaka huu wa fedha mwaka 2012/2013 imetenga shilingi 250,000/= ikiwa ni posho la usafiri, malazi na chakula, fedha hizo zinaweza kutumiwa na wanafunzi kwa kuhudumia usafiri. Posho hilo linatarajiwa kuongezwa kuanzia mwaka wa masomo 2013/2014.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha Taifa Tunguu cha Zanzibar. Chuo kinajiandaa kujenga dakhalia hapo chuoni katika awamu ya pili ya mkopo wa *World Bank* na mazungumzo ya awali yameshafanywa. Mhe. Spika, napenda kutoa wito kwa wazazi kuendelea kuchangia elimu ya watoto wao kwa kuwawezesha watoto hao wa kuwasaidia usafiri wa kwenda na kurudi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Mhe. Waziri, ametueleza kwamba wametenga kwenye bajeti hii posho kwa ajili ya nauli na malazi ya wanafunzi, lakini naomba nimuulize.

Kwa kuwa vyuo vya binafsi vina mabasi na yanaonesha kwamba ni mabasi ya chuo yanachukua wanafunzi. Je, serikali haioni kutonunua mabasi yake ni kujidhalilisha, na kama ndivyo ni lini serikali itaona haja ya kununua mabasi kwa ajili ya wanafunzi wa vyuo hivyo, ili kuwasaidia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, swali ni kwamba mbona vyuo vya binafsi vina mabasi kwa nini vya serikali visiwe na mabasi.

Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali mama serikali haijaweka bado mpango huo wa kuvipatia mabasi vyuo vyake, badala yake serikali itajitahidi kujenga dakhalia katika kila Chuo Kikuu, ili kuhakikisha wanafunzi wanaishi chuoni badala ya kutegemea usafiri wa mabasi ya kwenda na kurudi.

Kwa hivyo, kama nilivyosema kwamba Chuo cha Taifa (*SUZA*) katika mwaka huu wa fedha ujao kutokana na mkopo wa *World Bank* na kiwanja kipo tutajenga Dakhalia ya akinababa na akinamama, ili wanafunzi waishi hapo chuoni.

Vile vile ninayo taarifa kwamba Chuo cha Chukwani kinatafuta eneo na tayari wameshapata wanalo lengo la kujenga Dakhalia pamoja na Chuo Kikuu cha Tunguu cha Binafsi nacho kiko mbioni kujenga Dakhalia.

Mhe. Spika, serikali inaangalia umuhimu wa kujenga dakhalia kuliko kuvipatia vyuo hivi mabasi kwa ajili ya usafiri.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wizara imejipanga kujenga dakhalia na ujenzi huo unaweza kuchukua muda mrefu. Je, wizara ina mpango gani wa muda mfupi ambao wa kuondoshea kadhia wanafunzi hao katika kipindi hiki.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Serikali iliyo makini kama Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inapanga mipango yake ya muda mrefu na wala haipangi mipango ya muda mfupi. Kwa hivyo, muda mrefu ni kujenga dakhalia na muda mfupi ni kununua mabasi ambapo nimeshazungumza katika jibu mama kwamba serikali haikusudii kutafuta mabasi ya usafiri kwa vyuo vyetu hivi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mule ambamo wanavyo Vyuo vya Elimu ya Juu, kwa mfano japo *Form VI*, basi kulikuwa na dakhalia pamoja na magari ya usafiri na wanafunzi walikuwa wakila dakhalia na walikuwa wakilishwa na kushiba na serikali.

Hivi sasa Mhe. Waziri anasema kuwa kutajengwa madakhalia na tunajua elimu yetu ya juu kuna wengine serikali haiwasaidii kuwalipia na wanalipa kila *semister* shilingi milioni moja. Sasa Mhe. Waziri ataniambia vipi kuhusu wanafunzi hawa katika madakhalia hayo, watalala bure na

kula au itabidi pia zaidi ya malipo wanayolipia kwa masomo walipe na fedha za kutafuta chakula na kadhalika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi anazungumza wakati skuli hizo zinahudumia *population* au wakaazi katika jamii wanaofika laki tatu na kidogo. Lakini, hivi sasa tunazungumza wakaazi milioni moja na laki tatu mpaka nne hivi, kwa hivyo idadi bila ya shaka imezidi maradufu wasemavyo watu wa sasa.

Kwa hivyo, kujengwa dakhalia hivi sasa ni suala ambalo limeonekana ni muhimu na umuhimu wake unatokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi na ilihali usafiri unapungua hauongezeki na kinachoongezeka ni nauli za usafiri. Mhe. Spika, serikali kwa muda wake imekaa na kufikiria kwamba suala la kujibu matatizo haya ni kujenga dakhalia.

Kuhusu malipo kwamba watalipa au hawatalipa. Mhe. Spika, dakhalia hizi zitakapojengwa au wakati zinajengwa tutaleta waraka hapa Barazani, kwa ajili ya kuzungumzia Kanuni na Sheria za dakhalia hizi jinsi wanafunzi wetu watakavyoishi kwenye dakhalia na kama kutakuwa na malipo, basi ni kiasi gani kwa ajili ya chakula, malazi, dawa na kadhalika.

Nam. 72

Juhudi za Serikali Kuinua Soka Nchini

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla tunaendelea na mchakato wa kutoka kwenye mfumo wa Analojia na kuingia kwenye mfumo wa *Digital*, na kwa kuwa vyombo vingi vya Zanzibar tangu zamani hadi sasa ni vile vile vya Analojia, ambavyo havina uwezo na kunasa mawimbi ya Digitali bila kuunganishwa na ving'amuzi maalum.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kusambaza ving'amuzi hivyo nchi nzima.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kwamba Zanzibar na Tanzania kwa jumla tunaendelea na utaratibu wa kutoka katika mfumo wa utangazaji na Analojia na kuingia kwenye mfumo wa Digitali. Utaratibu huu unahusisha mabadiliko ya utayarishaji kwa kutenganisha vituo vya utayarishaji wa vipindi (*content provides*) na vituo vya kurushia matangazo (*multiplex operators*) ambavyo hupaswa kutoa vifaa vya kupekelea matangazo majumbani.

Kwa upande wa serikali yetu *multiplex* ya serikali inaendeshwa kwa kushirikiana na Kampuni ya *Agape Associates* na tayari imeingiza ving'amuzi vya awali elfu tano (5,000). Ving'amuzi hivyo

vimeanza kutumika na lengo ni kuviuza kwa wananchi wa Zanzibar katika wilaya zote za Unguja na Pemba.

Aidha *multiplex* ya serikali inakusudia kuingiza ving'amuzi vyengine 30,000 mwishoni mwa mwezi wa Aprili, ambavyo vitauzwa katika ngazi hizo za wilaya. Kwa upande wa Kampuni Binafsi ving'amuzi vinasambazwa katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, ambapo kuna mitambo yao ya kupeperusha matangazo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, hivi sasa tunaingia katika mfumo wa Digitali na Mhe. Waziri hivi karibuni alisema kuingia huku itakuwa tunaingia kidogo kidogo mara tunakwenda kwenye *Analogy* na halafu tunarudi kwenye *Digital*. Lakini hadi leo ukitumia king'amuzi *TBC Tevelevision* huwa inarusha wawimbi na haionekani, wakati unapokwenda kwenye *Analogy* unaikutia safi kabisa.

(a) Je, ni sababu zipi zinazoifanya tukitumia hivyo ving'amuzi ambavyo vinasifikana ni vizuri sana ikiwa mpaka leo *TBC Television* hatuioni katika hali inayostahiki.

(b) Kwa nini kule Pemba tukitumia ving'amuzi hivi vilivyoletwa hatuwezi kuipata *Television* yetu hii ya Zanzibar, yaani *ZBC Television* kwa urahisi na ina matatizo sana na watu wote wanarudi katika mfumo ule wa *analogy*.

(c) Kuna matatizo gani katika *analogy* na *digital* mpaka ikaonekana mambo haya hayaendi katika hali ambayo Mhe. Waziri alituelekeza, wengine wataona kwenye *analogy* safi na kwenye *digital* hawaoni, lakini inakuwa ni matatizo tu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, taarifa kwamba *channels* katika King'amuzi kilichouzwa cha serikali hazionekani vizuri sisi hatujazipata. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi ambao wanatumia ving'amuzi vyetu wakiona kwamba kuna tatizo lolote basi wasisite kutupa taarifa, ili turekebishe matatizo yaliopo ving'amuzi hivyo, pengine ni mitambo yao au *aeria* zao hazijakaa vizuri.

Kwa hivyo, inawezekana ni pande zote mbili, kwa sababu ili king'amuzi kiweze kufanya kazi vizuri basi lazima upate *antenna*, sasa inawezekana labda *antenna* yake haijakaa vizuri au ina matatizo mengine, pia inawezekana kuwa ni upande wetu. Lakini kwa jumla hivi sasa taarifa niliyonayo ya kiufundi na mimi mwenyewe ninaangalia ni kwamba *channels* zilizomo katika king'amuzi hichi zinaonekana vizuri kabisa na mwanzoni kulikuwa na matatizo madogo madogo na hasa baada ya umeme kutulia.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze sana Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa kufanya kazi vizuri, kwamba baada ya umeme kutulia sasa nacho king'amuzi chetu kimetulia sana katika kuendesha *channels* zake Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri. Kwanza nampongeza kwa kuweza kutimiza azma yake ya kuingia katika

mfumo huu wa sasa ambao umekamilika. Kampuni ya *Agape* ambayo tumeipa kazi ya kuingiza nchi kutoka *Analogy* na kuingia *Digital* hivi sasa inasemekana wanatumia vifaa au mitambo ambayo ni ya *ZBC Television*.

(a) Je, kitendo cha Kampuni hii ya *Agape* kutumia mitambo ya *ZBC Television* kumeiathiri kiasi gani huduma zile za *ZBC Television* za kila siku.

(b) Kuna makubaliano gani kati ya Kampuni ya *Agape* na *ZBC Television*, kwamba kampuni hii inatumia mitambo ya *ZBC Television*. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, taarifa niliyonayo kuhusiana na shughuli za *Digital* Zanzibar ni kwamba mitambo mikuu ya kupeperusha matangazo imeletwa mipya na Kampuni ya *Agape* na imefungwa pale Rahaleo na kwa wale ambao watakaopenda kuangalia hilo basi tafadhalini karibuni Rahaleo mutaoneshwa mitambo mikubwa, tena ya kisasa kabisa iliyoletwa kwa ajili ya kutayarisha na kupeperusha mawasiliano hayo.

Sasa katika kupeperusha matangazo Mhe. Spika, kuna baadhi ya maeneo tumekubaliana tutumie ama ile mitambo ya *television* au miundombinu mingine ambayo inamilikiwa na taasisi nyengine na zaidi ni minara.

Kwa hivyo, ni kweli kwamba tunatumia minara miwili ya *ZBC* mmoja uliopo Masingini na mwengine uliopo Chakechake. Vile vile tunatumia minara miwili ya *ZANTEL* mmoja uliopo Muyuni na mwengine uliopo Konde Chanjaani. Mhe. Spika, pia tunatumia minara miwili ya *E-Government* mmoja uliopo Nungwi na mwengine uliopo Kichunjuu Mkoani.

Kwa hiyo, hayo ni makubaliano baina yetu na kwa sababu hakukuwa na sababu ya msingi ya kuendelea nchi yetu ya kujenga minara mingi wakati minara ipo na tunaweza kutumia. Kwa maana hiyo, tunaitumia kwa makubaliano maalum na hali hiyo haiathiri hata kidogo shughuli za matumizi ya taasisi hizo ambazo tunatumia minara yao, *ZBC*, *ZANTEL* na wala *E-Government* haziathiriki.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika, ahsante naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Waziri alitaja Kampuni ya *Agape*, kwamba ndio inayoshughulikia na *digital* hapa Zanzibar.

Je, wizara yake iliweka vigezo gani ambavyo iliwezesha Agape kupewa kazi hiyo na kampuni gani iliyoshindana nayo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali kupitia wizara yangu iliipa kazi Kampuni ya *Agape Assocciates* ya Dar-es-Salaam wakishirikiana na washirika wake wa *Eletronic* kutoka Afrika ya Kusini kutujengea miundombinu hapa Zanzibar.

Vigezo tulivyotumia ni kwanza miundombinu itakayowekwa iwe ni mali ya serikali kwa sababu *information power* hatuwezi kuweka miundombinu ambayo baadaye iwe ni mali ya mtu mwengine, kwa hiyo kwanza miundombinu itakayowekwa iwe ni mali ya serikali.

Pili *transmitter* zitakazotumiwa ziwe za aina ya ***RHODE AND SHWARTZ*** za Kijerumani. Tumefanya hivyo kwa sababu mafundi wetu kwa muda mrefu wamekuwa wakizitumia hizi, kwa hiyo tunaona kwamba *technology* yake mafundi wetu wameweza kuwa nayo kwa muda mrefu.

Tatu ni kwamba mtambo mkuu utakaokuja pale uwe ni wa aina ya *technology* ya kisasa ya *DVB2* badala ya *DVB1* ambayo imezoeleka. Mhe. Spika, *technology* hii inaweza kutupeleka hata kama tutaamua kuingia *High Difinition* badala *Standard Definition* inayotumika sasa.

Lakini la mwisho ni kwamba mitambo hii, yaani *transmitter* za *analogy* zilizopo katika Kituo cha Chakechake na Masingini zisihamishwe kutoka eneo moja kwenda eneo jengine. Hayo ndio masharti ambayo tuliyoyaweka serikali na zaidi kwamba kampuni yoyote itakayopewa iwe imekubali kwamba ikamilishe kazi hii ndani ya muda wa miezi mitatu, kwa sababu ilitoa kazi hii mwezi wa Septemba, ili nchi iweze kuingia katika *digital* sambamba na nchi nyengine za Afrika ya Mashariki mwezi wa Disemba mwisho.

Kwa hivyo, makampuni mengine ambayo *Agape* alishindana nayo ni ***HUAWEI*** ya China iliyotaka milioni 28 Dola karibu milioni 40 kwanza na halafu akaja chini mpaka ananyumbuka na tunaona mtihani kidogo. Kwa kweli milioni dola 28 kwa nchi yetu Mhe. Spika ni nyingi kwa hiyo sisi hatukuweza kuishauri serikali tu-*deal* naye.

Vile vile kuna Kampuni ya *Star Times* nayo ikaja lakini kwa masharti kwamba yeye amiliki mitambo hii na sisi tupitishe *channel* moja tu. Kwa hiyo, hili kwetu sisi ikawa haliwezekani kwa sababu ni kinyume na masharti yetu. Mhe. Spika, Kampuni nyengine ni ***DIXIN*** ya China ilikuwa na yenyewe walikubali kwamba watuwekee *transmitter* za kichina, sasa hii tukaona ni kinyume na masharti yetu ya awali.

Mhe. Spika, baada ya kuangalia kampuni hizi zote zilizokuja na tukaona kwamba bei ya Kampuni ya *Agape* ilikuwa ni dola milioni 4. Sasa ukiangalia dola milioni 4 ya *Agape* na dola 28 milioni za *Star Times* mimi kama Waziri sikuweza kuishauri serikali kwamba tukubali milioni 28 na tuache milioni 4 za *Agape*.

Nam. 73

Uendeshaji Kazi za Sanaa

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kazi ya Sanaa ni muhimu sana, sio tu kwa ajili ya kutoa burudani lakini hata kutoa elimu na mafunzo kwa jamii. Kwa kuwa nchi nyingi zimekuwa zikiwatunza wasanii kwa kuwatungia sheria zenye kulinda haki na kazi zao. Kwa kuwa Zanzibar vijana wetu wengi wamewekeza maisha yao katika kazi za sanaa mbali mbali zikiwemo zile za maonesho, uchoraji, uandishi na uimbaji.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kuendeleza kazi za sanaa sambamba na kuzilinda kazi za wasanii wetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru na kwa idhini yako naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali ina mipango mingi ya kuendeleza kazi za sanaa na kulinda kazi za wasanii wetu. Miongoni mwa mipango hiyo ni Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia Baraza la Sanaa Zanzibar na kwa mashirikiano ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuendeleza kazi za sanaa kwa kuanzisha Mashindano ya Sanaa Maskulini. Kwa kweli hali hii itasaidia kuonesha na kuibua vipaji vya wanafunzi katika sanaa husika.

Aidha sambamba na juhudi za kufufua Nyumba ya Sanaa iliopo Mwanakwerekwe katika mipango ya muda mrefu tunakusudia kuanzisha Kituo cha Utamaduni, yaani *Cultural Centre*, ambayo itaonesha sanaa zote ambazo zinafanyika katika kituo hicho kama vile sanaa za uchoraji, ufundi, ufumaji, ususi, uchongaji, ufinyanzi, kudarizi, usokotaji, ushonaji na ngoma zetu za asili. Hii itasaidia wageni kutembelea katika hili eneo na kuweza kuongeza pato la nchi na pia kuibua zaidi vipaji vya vijana wetu.

Mhe. Spika, katika kulinda sanaa za wasanii nchini Baraza la Sanaa linasajili vikundi vya sanaa na kuwashajihisha wasanii kupeleka kazi zao za sanaa ofisi ya Haki Miliki *(COSOZA)* kwa ajili ya kuzilinda kazi hizo na kupata haki zao pale kazi hizo zitakapotumiwa na watu bila ya ruhusa ya wasanii wenyewe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.
Mhe. Spika, kwa kuwa wasanii katika sanaa za uchoraji pamoja na hata waimbaji kazi zao huwa ni kama kioo, yaani jamii huitumia na kuweza kujirekebisha na hawa wasanii wa kuchora wanasaidia sana katika masuala mbali mbali yakiwemo kuenzi nembo au taaswira ya nchi yetu kupitia michoro yao.

Mhe. Spika, kwa sababu hawa wasanii waliobuni hii nembo ya SMZ kama iliyopo hapo nyuma yako na aliyebuni ile nembo ya Baraza la Wawakilishi imeswibi nembo hizi kwa kweli kutoa taaswira ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na nembo ya Baraza la Wawakilishi.

(a) Je, serikali imetambua vipi kazi yao hii.

(b) Ni lini angalau itatoa cheti kwa hawa waliobuni nembo hizi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ni kweli kwamba shughuli hizi za usanii ni muhimu katika nchi na zinapaswa kuendelezwa sana kwa maslahi ya nchi ili kulinda utamaduni wa nchi lakini pia vipaji vya watu wetu. Sasa kuhusu wasanii waliochora nembo hizi, kwanza kwa taarifa niliyonayo walilipwa hakufanya kazi bure, hiyo kulipwa tu basi walienziwa. Sasa kama ushauri wake kwa sababu walifanya jambo kubwa kwa nchi tuwape cheti, basi ushauri wake Mhe. Spika, tunauchukua na tutakwenda kuufanyia kazi.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri pamoja na harakati tunazoendelea nazo kama vilivyo nchi nyengine duniani, utamaduni ni sehemu ya maendeleo ya nchi. Sasa je, Mhe. Waziri kuna vijana wetu ambao wanajishughulisha sana na shughuli za kuigiza michezo, kuimba na harakati nyenginezo. Wizara yako imejipanga vipi katika kuona kwamba watu hawa unawasaidia ili kuweza kujiendeleza kimaisha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nakubaliana nae kwamba utamaduni kama alivyosema awali kwamba ni jambo zuri sana na masuala haya ya vijana wetu wanaojishughulisha na shughuli hizi wanafanya kazi kubwa sana.

Mhe. Spika, jibu lake ni kwamba shughuli hizi zinatakiwa iwe ni ajira, si suala la kufanya kazi hii kwa ajili ya kustarehesha tu, kwa hivyo ni vizuri kwamba kwanza wajue kuwa shughuli wanayoifanya ni shughuli ya kujipatia kipato kwa hivyo wajielekeze kutafuta namna gani ambavyo shughuli yao inaweza kuwa na soko ili watu waipende, ili watu wainunue. Kwa hivyo katika Baraza la Sanaa huwa tunakaa nao, tunawapa taaluma, tunawapa semina kwamba namna gani waweze kufanya kazi zao ili wajipatie soko ili wapate kipato kutokana na sanaa hizo.

Lakini mbali na hizo sisi Wizara ya Habari tumejenga jingo lile la Rahaleo la Studio ya zamani, tumeligeuza kuwa ukumbi wa vijana wa kurikodia sanaa mbali mbali. Kwa hivyo ni aina moja ya msaada ambao serikali inaweza kutoa. Lakini kwa ujumla wanahitaji shughuli zao wazifanye ziweze kuvutia waskilizaji au watazamaji kwa kupitia hali hiyo ndio inaweza ikapata soko.

Lakini hata hivyo tutashauriana na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, Kiushirika, tuangalie namna gani vikundi kama hivi vitaweza kuwezeshwa.

Nam. 49

Miundombinu na Barabara

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Nina imani kuwa lengo la Wizara ni kuona kuwa wananchi wa Mijini na Vijijini wanafaidika kimaisha kwa kuwa na miundombinu ya barabara inayoweza kutumika kutoa huduma kwa muda wote.

(a) Ni lini serikali itaamua kuwaondolea dhiki hii wananchi kwa zile sehemu ambazo huduma hii hijafika ipasavyo kama vile vijiji vinavyotumia Barabara ya:-

(i) Makongeni - Kinazini

(ii) Mwembemazizi - Chanjaani

(iii) Mpakanjia - Kiapaka

(iv) Mpakanjia - Kidundo

(v) Uondwe - Kilikong'ombe

(vi) Mkanjuni - Kivumoni

(vii) Uondwe - Nyali

(viii) Bwagamoyo - Mto-mkuu (darajani)

(ix) Barawa - Mtemani

(x) Ziwani - Malindini

Kwa sababu sehemu nilizozitaja ni sehemu za kilimo na wananchi wanapata shida sana ya usafiri kwa siku za mvua.

(b) Serikali haioni kuwa muda mrefu umeshapita tokea Mapinduzi ya mwaka 1964 watu hawa bado hawajafaidika na huduma hiyo kama wanavyofaidika Wazanzibari wenzao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49, lenye vifungu (a), (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi juu ya lengo la Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na serikali katika kurahisisha huduma ya usafiri wa barabara kwa wananchi wake. Aidha serikali tayari imeshaanza kuchukua hatua ya kuwaondolea wananchi usumbufu wa usafiri kwa baadhi ya maeneo ya mijini na vijijini pamoja na barabara hizo kuzifanyia matengenezo madogo madogo.

Baadhi ya barabara kwa kushirikiana na wananchi wa maeneo hayo pamoja na mfuko wa TASAF. Barabara ambazo zimefanyiwa matengenezo madogo madogo na ambazo sasa hivi zinapitika bila ya usumbufu ni pamoja na barabara ya Mwembe Mazizi hadi chanjaani. Barabara hii imechongwa kwa kushirikiana na ZSTC ili kuhakikisha inapitika kwa wakati wowote. Barabara nyengine ya Uondwe hadi Kilikong'ombe, barabara hii imefanyiwa matengenezo kwa kushirikiana na wananchi wenyewe kwa kuiwekea kifusi baadhi ya sehemu korofi.

Barabara nyengine ni ya Uwondwe hadi Nyali hii tayari imeshafanyiwa matengenezo madogo madogo kwa kushirikiana na wananchi wa eneo hilo na hivi sasa inapitika vizuri. Barabara nyengine ya Bwagamoyo hadi Mto-mkuu (Darajani) ambayo barabara hii tayari imeshafanyiwa matengenezo mara mbili kwa kushirikiana na mfuko wa TASAF. Aidha ujenzi wa daraja umefanyika kupitia mfuko wa barabara kwa zile barabara ambazo hazijafanyiwa matengenezo ambazo ni za miundombinu na mawasiliano, itaangalia uwezekano wa kushirikiana na Halmashauri katika mpango wao wa kazi ili kuweza kuziingiza katika utaratibu wa kuweza kuzifanyia matengenezo.

(a) Jambo la kujikumbusha ni kwamba miradi ya barabara ni miradi yenye gharama kubwa na sitegemei kama serikali tutaweza kuikamilisha yote kwa wakati mmoja.

(b) Kwa kuzingatia madhumuni haya ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, serikali hivi sasa inaendelea na ujenzi wa barabara ya Bahanasa - Daya hadi Mtambwe na Makongeni nadi Uondwe ambazo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa tatizo la usafiri katika maeneo hayo. Hivyo wananchi hawataendelea kufaidika na Mapinduzi yao matukufu kama walivyo wananchi wengine wa Zanzibar.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata jibu zuri na kwa urefu. Lakini kabla sijauliza swali la nyongeza naomba tu kuweka sawa kuwa barabara ya Uondwe – Kilikongombe ni kweli ilianza kutengenezwa lakini kabla ya kumalizika na kule kwenye shida lile gari halikufika likarejeshwa mpaka leo halikupita tena. Kwa hivyo bado ipo katika hali mbayo ile ile.

Pili Mheshimiwa kasahau naweka sawa tu kwamba barabara ya Makongeni - Kinazini vile vile ilitengenezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, lakini sasa hivi ni mbaya, juzi tumetengeneza kwa pesa kwa mara nyengine.

Mhe. Spika, ningependa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Barabara hizi hazina kifusi na zikitengenezwa ikinyesha mvua hali inarudia vile vile, kwa hivyo inakua huduma iliyokusudiwa haipatikani. Je, Mhe. Waziri haoni kuwa ipo haja baada ya zile barabara kutengenezwa moja baada ya nyengine kuwahiwa kwa vifusi ikawa panapotengenezwa imemalizika alau iweze kupitika. Ikiwa hali ni ngumu hata hivyo atakubaliana na mimi kuwa nichukue dhamana ya kuzifanyia *grading* barabara zote hizi lakini serikali isaidie kuweka vifusi ili shida kwa wananchi iondoke.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kuhakikisha kwamba usumbufu huu wa usafiri unaondoka. Matatizo yaliyopo ni kwamba kuna baadhi ya maeneo tunajaribu kuchonga barabara na kuweka kifusi. Lakini kuna baadhi ya maeneo kifusi kinakaa vizuri kulingana kutokana na maumbile ya ardhi husika. Kwa mfano kama Makunduchi, barabara zile zimejengwa kwa kifusi zimekaa vizuri.
Hivyo basi nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba malengo yetu ya kujenga barabara yapo, maeneo hayo tutakuwa tunayazingatia kwa mazingatio maalum ili kunusuru kifusi kisiondoke kama ilivyo hivi sasa. Lakini baadhi ya maeneo Mhe. Mwakilishi amekuwa akililalamika hayakuwekwa kifusi na hali hiyo inatokana na ile bajeti yenyewe husika kutokana na Halmashauri na wananchi wao wenyewe walichokiomba kwa serikali na kwa kuwa serikali haikuwa na bajeti.

Kuna baadhi ya maeneo yeye mwenyewe Mhe. Mwakilishi naamini atakuwa shahid walichokiomba wananchi ni kwamba angalau wachongewe iweze kupitika barabara. Sasa kama barabara itakuwa imechongwa haikuwekwa kifusi tabaan ikija mvua barabara ile itachimbika. Mategemeo yetu kwamba tunategemea kwa Mhe. Mwakilishi atawahimiza wenzetu wa Halmashauri na kwa kuchangia yeye mwenyewe binafsi, sisi kama Wizara ya Miundombinu

tuko tayari kutoa mchango wa vifaa pamoja na mafundi ili kuweka kifusi kitakachodumu kwa muda mrefu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kufika katika shughuli zetu hapa Barazani kwa mintaraf ya kulijenga taifa letu. Lakini pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Spika, kwa kuwa katika Pemba nzima shehia kubwa ni ya Mtambwe ukilinganisha na Geographia. Na kwa kuwa Mtambwe ndiyo inayotoa mazao ya karafuu kwa wingi. Na kwa kuwa Mtambwe ina vichochoro vingi vya kusafirisha magendo ya karafuu.

(a) Je, haoni Mhe. Waziri ni vyema akatathmini zile njia ambazo kwa kweli ndizo zinazowapa fursa wananchi wetu kupenyeza karafuu kwa magendo.

(b) Ataliambia vipi Baraza lako hili tukufu kwamba suala la njia za Mtambwe zimekithiri ukiacha hii barabara ambayo inajengwa hivi sasa, lakini njia zake zote hazipitiki. Je atakubaliana name kwamba kuna haja ya kutathmini na kuona kwamba hizi njia za panya zinafanyiwa matengenezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakubaliana na mkaelezo aliyotoa Mhe. Mwakilishi kwamba kuna baadhi ya barabara ndani katika jimbo la Mtambwe hazipo hali nzuri. Tunalitambua hilo, lakini jambo la kushukuru kwamba tuna ushirikiano mzuri sana na Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Mtambwe pamoja na wananchi. Mhe. Mwakilishi tumemfungulia milango amekuwa ana desturi ya kuja kuzungumza nasi na tumekuwa tukishirikiana naye katika kupunguza changamoto katika jimbo hilo.

Ninachomuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba sisi kama Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na mifuko mengine inayosaidia ikiwa TASAF na mengineyo, tutawasaidia wananchi hawa kwa kuhakikisha kwamba nyenzo zilizokuwepo za mafundi pamoja na vifaa vinatumika ili kuondoa usumbufu kwa wananchi hawa wa jimbo la Mtambwe kama tunavyoondoa usumbufu katika baadhi ya maimbo hapa nchini kwetu.

Nam. 87

Tatizo la Uvutaji Sigara

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Sigara ni moja kati ya vyanzo vya uharibifu wa mazingira, kwani moshi wa sigara unaathari kubwa katika mwili wa binadamu, na kwakuwa mataifa mengi hutenga maeneo mahsusi kwa wavutaji sigara pale panapokuwa na mkusanyiko wa watu wengi.

Ni lini Zanzibar tutafikia hatua hiyo ya kuwatengea wavutaji wa sigara maeneo yao katika vyombo vya usafiri na hafla mbali mbali zikiwemo za serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi wa Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi sana kama ifuatavyo. Kwamba athari za uvutaji wa sigara kwa mazingira ni ndogo sana, ukilinganisha na athari za uvutaji sigara kwa afya za wanadamu. Kwa kuthibitisha hili katika takwimu ambazo tunapewa watu wa mazingira ni kwama Afrika nzima imechangia katika uchafuzi wa mazingira (hewa chafu) kwa chini ya asilimia moja na Afrika ina wavutaji sigara wengi sana ukiachilia mbali maeneo mengine.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa kujibu swali hili kwa ufasaha zaidi na kwa kuwa serikali inawajibika kwa pamoja ndani ya Baraza lako hili tukufu, Afisi yetu iliwasiliana na Wizara ya Afya kwa kupata majibu, hasa ukizingatia kwamba msingi wa suala la Mhe. Mwakilishi ni kulinda afya ya binaadamu.

Baada ya maelezo hayo mafupi Mhe. Spika, sasa naomba kujibu suala la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

Kwa mujibu wa sheria ya afya ya jamii na mazingira *(The Public and Environmental Health Act)* sheria hii ya Nam. 11 ya mwaka 2012 ambayo tuliipitisha mwishoni mwa mwaka uliopita kifungu cha 109 katika kifungu kidogo cha kwanza. Uvutaji na Uwashaji wa Sigara katika maeneo ya ndani, yenye mkusanyiko wa watu umepigwa marufuku. Hata hivyo kifungu kidogo cha pili kinampa uwezo Waziri wa Afya kwa kuweka kanuni za kuzuia uvutaji wa sigara katika maeneo ya wazi ambayo yataainishwa kuwa ni ya mkusanyiko wa watu au uvutaji wa sigara unaweza kusababisha moto au maafa mengine kwa jamii.

Mhe. Spika, katika kanuni hizi ndipo ambapo serikali itaweka maeneo au itawataka wasimamizi wa maeneo yatakayoainishwa kutenga sehemu maalum kwa wavutaji wa sigara. Kwa hivi sasa imeanza kufikiria namna ya kukutana na wadau mbali mbali ili kutayarisha kanuni hizo ambazo hazina muda mrefu zitakuwa tayari.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba niulize suali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa amesema kimsingi suala langu linasibu katika mambo ya afya na wala sio mazingira. Lakini mimi nasema kwamba afya ya mtu huathirika baada ya mazingira kuwa *contaminated* kwa hivyo nako lipo na ndio nikalipeleka huko.

Mhe. Spika, kwa kuwa ndani ya sigara kuna sumu inaitwa *nicotine* na ni hatari sana kwa afya ya binaadamu kwa sababu inaingizika kwenye damu ukivuta tu sigara ile, ikiwa mwenzako anavuta ukivuta hewa iliyokuwa *contaminated* na *nicotine* basi inachanganyika na *reaction* kwenye damu inaingia katika *cells* za kufanya *distruction* ambayo baadaye inaweza kusababisha kensa.

Ni lini serikali yetu itabagua, sitaki niseme kwamba kuwabagua wananchi lakini tumezoea kwamba ukienda nchi za nje *depercher logs* ina ya *smoking* na *no smoking* wenzetu wanafanya hivyo. Ni lini Zanzibar tutafika huko kwamba hata pale sehemu ya kusafiria utakutia huku wanakwenda huku wanavuta sigara na huku wasiovuta sigara. Kwenye ndege tunaposafiri katika

madege ya nje, abiria hawa huku wanavuta sigara, abiria hawahuku wasiovuta sigara. Ni lini tutafika huko Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba suala lake pia linahusiana na mazingira na hata kama atakuwa amesikia vizuri ile sheria yenyewe hasa inayopiga marufuku uvutaji wa sigara katika maeneo ya mkusanyiko yenyewe inaitwa *The Public and Environmental Health* kwa maana kwamba suala la mazingira ni suala mtambuko.

Lakini athari zaidi za sigara nilichozungumza kwa mwanadamu zipo zaidi kiafya kuliko uchafuzi wa mazingira na ndio maana tumelijibu katika afya ya binaadamu. Hata hivyo anavyouliza suala lake la pili, amelihusisha moja kwa moja na athari ya sigara kwa mwanadamu na kumletea madhara katika kupata maradhi.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba nijubu kama ifuatavyo:

Sheria hii Mhe. Spika, tumeipitisha mwishoni tu mwaka jana, imeshawekwa sahihi na jambo lolote linahitaji maandalizi hasa likiwa jipya katika jamii. Wizara ya Afya inachofanya hivi sasa ni kufanya mikutano ya wadau wote mfano kama alivyozungumza yeye ambao wanahusika na vyombo vya usafirishaji, ambao wanaohusika na maeneo ya mikahawa, hoteli za watalii na aina hiyo,ili kwa pamoja kuweza kukubaliana ni jinsi gani utekelezaji wa sheria hii utaweza kufanyika. Naomba atuamini kwamba mchakato huu unaendelea na baada ya suala lake hili nafikiri Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla italihimiza kuona kwamba kanuni hizi zinaletwa katika jamii mara moja ili athari zaidi kwa wananchi zisiendee kupatikana.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nashukuru Mhe. Spika, kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri suala moja la nyongeza.

Mheshimiwa kikawaida sheria ikishapitishwa na kutiwa saini na Rais inatakiwa ianze kufanyiwa kazi mara moja. Na kwa kuwa sasa ni kipindi kwa sababu tangu kuipitisha sheria hiyo bado tunaendelea kushuhudia watu wakiendelea kuvuta sigara kwenye mikusanyiko kana kwamba hakuna sheria.

Naomba nimuulize Mhe. Waziri tangu Rais kuisaini sheria hiyo ambayo hivi sasa ni zaidi ya miezi mitano au sita ni watu wangapi wameshakamatwa na kupelekwa mbele ya vyombo vya sheria kwa kukiuka sheria hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba sheria inapopitishwa kinachofuata ni utekelezaji wake. Lakini naomba naye akubaliane na serikali kwamba sheria yoyote inapokuwa mpya kwanza inahitaji kuelimishwa kwa jamii. Jamii iweze kuelimishwa na ili iweze kuelimishwa sheria kama inahitaji kutungiwa kanuni hasa hii ambayo nimeiyeleza kifungu hichi kitakachoainisha maeneo gani mtu anaruhusiwa kuvuta sigara na maeneo gani havuti kipo kwa mujibu wa kanuni ambayo itatungwa na Waziri wa Afya. Kutunga kanuni hii ili iweze kuwa sawa sawa na iweze kutekelezeka unahitaji kuwashirikisha wadau.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Omar aelewe kwamba mchakato huu unaendelea na kwa hivi sasa kwa sababu kanuni zenyewe hazijawa tayari, sinataarifa mimi binafsi kama tayari amekamatwa mtu kwa sababu hayo maeneo yenyewe wapi mtu asivute sigara bado hayajaainishwa kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza suali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri kakiri kama sheria ikishapitishwa inatakiwa itumike, na kwa kuwe sheria imeshatiwa saini zamani na Rais na kwa kuwa kakiri kama kunataka maandalizi na maandalizi yenyewe ni elimu kwa wananchi. Je, ni sehemu ngapi ambazo wamepita kuwaelimisha wananchi kuhusu suala hili. Kama bado ni lini serikali imejipanga kuwaelimisha wananchi kama uvutaji wa sigara, waache kuvuta panapowatu ili wajue kama sheria tumeshaipitisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, katika suala hili kuna elimu ya aina mbili. Kuna elimu ya kwanza inayohusiana na athari ya sigara kwa mwananchi mwenyewe au kwa mwanaadamu. Elimu hii Wizara ya Afya inajitahidi sana kuitoa kila siku kwenye vyombo vyetu vya habari, mabazeti, redio na televishen, kila baada ya muda huwa tunaona elimu hii inatolewa na madaktari wetu.

Elimu nyengine ambayo tumeikusudia hapa sasa ni elimu ya kuielimisha juu ya sheria yenyewe ya upigaji marufuku wa uvutaji wa sigara katika maeneo ya mkusanyiko, ambayo kanuni itakayotungwa na Mhe. Waziri wa Afya ndiyo itakayoainisha hayo maeneo yenyewe.

Mhe. Spika, kwa sababu kanuni yenyewe bado haijawa tayari, eneo hili la pili bado halijafanyiwa kazi.

Nam. 88

Mchango wa Serikali katika kuendesha Sober House

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Wizara ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama mnavyoelewa kwamba shughuli hii tuliianza juzi siku ya Ijumaa na kwa kweli ilikuwa kuna michango ya Wajumbe wawili tu kwa hivyo nategemea shughuli hii tuimalize kipindi cha asubuhi, lakini angalau tupate michango ya Waheshimiwa wawili watatu ili kuongeza nguvu kwenye ripoti ya utekelezaji lakini pia kwenye ripoti mpya iliyowasilishwa. Kwa hivyo haraka haraka basi nimuombe Mhe. Omar Ali Shehe na baadae Mhe. Hija Hassan Hija wachangie hivi sasa na wajitahidi kutumia muda mfupi.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa siku ya leo kuwa ni mchangiaji wa kwanza lakini pili ningependa niipongeze Kamati kwa kufanya kazi nzuri kwa kipindi hiki cha mwaka katika kuzisimamia wizara zake hizi ambazo zimeainishwa katika ripoti.

Mhe. Spika, Kamati hii inafanyia kazi Wizara mbili ambazo ni muhimu sana. Kuna Wizara hii Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na pia Wizara ya Katiba na Sheria ambayo ndio msingi wa utungwaji na marekebisho ya sheria zote katika nchi.

Nianze na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika suala la Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, Utumishi wa Umma linahusiana na wafanyakazi wote katika sekta ya umma na wafanyakazi hawa kwa kweli ndio watumishi wa serikali katika namna ya uzalishaji kama ni suala la uzalishaji wanahusika watumishi wa umma na katika suala zima la utoaji wa huduma wao ndio wanaohusika wafanyakazi. Kwa hivyo tukiwa na wafanyakazi makini, tukiwa na wafanyakazi wenye uwezo ndipo pale huduma za serikali, ndipo pale uzalishaji mali na uchumi wa nchi unapotengamaa katika nchi.

Sasa katika hili naomba niseme kwamba Zanzibar tuna tatizo katika sekta ya umma kwa suala zima la uduni wa mishahara. Mhe. Spika, mishahara ya wafanyakazi wetu katika sekta ya umma hailingani kabisa kabisa na hali ya maisha kitu kinachopelekea kwa asilimia kubwa kuathiri shughuli za utendaji katika sekta ya umma. Naipongeza serikali, naishukuru serikali hasa ya awamu 7 iliyoingia madarakani kwa namna ilivyojaribu kujikakamua katika kuongea maslahi kwa wafanyakazi lakini naomba pia kwa bajeti hii inayokuja baada ya miezi michache ijitahidi kuona kwamba inaongeza maslahi pamoja na mishahara kwa wafanyakazi wa umma.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba kuna uwezekano mkubwa kwa wafanyakazi wetu kuongezewa mishahara. Lakini tukubali kwa upande mwengine tuna tatizo lililozungumzwa juzi na Kaimu Mwenyekiti aliyekwenda kuwasilisha katika masuala mbali mbali na katika mawasilisho yake, kwamba tunakabiliwa na wafanyakazi waliokuwa hawana uwezo katika serikali. Serikali ina idadi kubwa kuliko mahitaji yanayohitajika katika sekta ya umma na kwa vyovyote vile serikali ni muhimu ilikalie suala hili na ilizingatie. Sisemi kama wafanyakazi wapunguzwe kwa sababu sera ya serikali ni kuona kwamba kadiri siku zinavyokwenda lazima

itoe ajira kwa wananchi, kwa sababu ajira kwa wananchi ni jukumu kubwa la serikali. Lakini sasa tuangalie namna gani serikali inawapatia ajira katika sekta gani, tulivyozoea na tulivyojizowesha kwamba ajira inapatikana katika serikali kitu ambacho si sahihi. Serikali haina uwezo wa kuajiri kila mtu. Ni sekta ya umma pekee ndio ambayo inaweza kuchukua zaidi ya asilimia 80 katika soko la ajira. Sasa katika hali tuliyokuwa nayo katika moja ya mipango ya serikali ambayo inatakiwa iifanye ni kuangalia na kutathmini hali halisi ya idadi wafanyakazi wanaohitajika.

Na mara nyingi na katika serikali nyingi duniani haya yanafanyika hata jana tulisikia kule kwamba kuna kitu kinaji-*attachment* ya wafanyakazi, tunapofika pahala tukaona kwamba serikali inabebwa na ziko la wafanyakazi serikali inafanya vitu kama hivi, *re-attachment*. Kwa hivyo naomba Mhe. Spika, serikali inaweza ikatafuta wafadhili popote pale wako wafanyakazi hivi sasa ukiwaahidi ukiwaambia jamani mnaweza mkapewa chenu lakini mstaafu au mfanye vyovyote wapo wafanyakazi ambao wako tayari kufanya hivyo. Kwa hivyo nashauri kwamba serikali ielekee huko na ifikirie suala hili la kupunguza idadi ya wafanyakazi lakini sambamba na kuwafikiria namna nyengine ya kuwapa kazi nyengine katika sekta ya umma.

Na katika hili bado tunaendelea kushuhudia kwamba bado serikali haijawa *active* katika kuihamasisha na katika kuimarisha sekta ya umma. Ninachoamini kwamba sekta ya umma ndio mkombozi wa tatizo la ajira katika nchi yetu. Lakini tuangalie kwamba kiasi gani serikali inafanyia kazi maboresho katika sekta ya umma.

Mhe. Spika, katika mnasaba wa suala hilo nililozungumza umuhimu wa serikali kuboresha maslahi ya wafanyakazi, lakini vile vile tuzingatie suala la ufanisi na utendaji kazi serikalini. Licha ya kuwa na idadi ya wafanyakazi wengi Mhe. Spika, katika serikali tuna tatizo la wafanyakazi kutotekeleza majukumu yao. Sababu moja ikiwa ni hii kwamba mfanyakazi akishaingia kazini anachokifikiria vipi atapata kijio cha mchana na watoto. Mtu anapofikia suala hilo huwa hana fikra ya kufikiria kutenda kazi. Lakini suala hili Mhe. Spika, linatokana pia na suala la usimamizi wa wafanyakazi kwa wahusika.

Mhe. Spika, suala la usimamizi wa wafanyakazi linakuwa tatizo katika sekta ya umma. Naomba nishauri kama nilivyoendelea kushauri kipindi cha nyuma kwamba Mhe. Waziri anapaswa sasa kuandaa utaratibu ama kwa kila Idara ama kwa kila Wizara kuona kwamba mfanyakazi kwa siku anafanya shughuli gani, lazima Mhe. Waziri ufike pahala uwe na kitu kama hicho. Mfanyakazi anaweza akaenda kazini muda wa wiki nzima ukimuuliza umefanya kazi hawezi kukwambia nilifanya kazi gani kubwa ni kwenda kazini na kutoka tu.

Kwa hivyo naishauri Wizara iwe inaandaa utaratibu maalum wa kuhakikisha wafanyakazi kwa siku, ama kwa wiki, ama kwa mwezi analeta ripoti juu ya kazi alizopangiwa na namna alivyozitekeleza katika majukumu yake.

Naomba niondoke hapo niende katika suala zima, tuna tatizo katika sekta ya juu ya suala zima linalohusiana na mishahara. Tunavyojua mpangilio wa mishahara unatokana na sifa pamoja na uzoefu, lakini leo katika sekta ya umma Mhe. Spika, unaweza ukawakuta watu wakiwa na sifa moja wakiwa pengine na uzoefu mmoja lakini wenye viwango tofauti na hilo tumelieleza hasa katika kada ya uhasibu. Mhe. Waziri naomba atakapokuja na hili aweze kutufafanulia. Mathalan

utamkuta Mhasibu katika ngazi ya Wizara lakini utamkuta Mhasibu katika ngazi ya Wizara kwa upande wa Pemba wana elimu moja, wana uzoefu mmoja na hicho ndicho kitu tulichoambiwa ndio kigezo katika kulipa. Lakini unaweza ukafika pahala utakuta kwamba mishahara ni miwili tofauti tena inapishana kwa sehemu kubwa. Naomba Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi.

Mhe. Spika, kitu chengine ambacho naomba nikielezee ni suala zima la utawala kwa hivyo ni sawa na kusema kwamba Mhe. Waziri au Wizara yake ndio yenye jukumu la kuainisha kipimo cha utekelezaji wa kila Wizara katika serikali. Ufanisi uliofikiwa, sasa kama hivyo ndivyo tunataraji kwamba Baraza hili lipate taarifa ya utawala bora kwa maana ya utekelezaji ulio fanisi katika Wizara zetu zote kwa serikali.

Mhe. Spika, naiomba serikali iandae utaratibu basi wa kuweza kuli-*address* suala la utawala bora na utekelezaji wa dhana hii katika kila kipindi cha mwaka mmoja Mhe. Waziri aje atupe taarifa inayohusiana na utekelezaji wa utawala bora katika serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ninajua kwamba suala hili ni suala MTAMBUKA ambalo linahusu katika Wizara zote na katika mashirika yote na katika taasisi zote za umma tulizonazo katika nchi.

Mhe. Spika, vile vile dhana hii ya utekelezaji wa dhana hii unatokana na suala zima la kuwepo kwa mihimili mitatu ya dola inayoheshimiana ndio dhana inakotupeleka huko. Mhe. Spika, hapa kidogo tuna tatizo. Serikali ipo kwa mujibu wa Katiba na ina mamlaka kwa mujibu wa Katiba na Baraza letu lipo kwa mujibu wa Katiba na lina mamlaka kwa mujibu wa katiba. Kadhalika na mahkama ni vile vile, Baraza limepewa jukumu kwa mujibu wa Katiba la Kuisimamia serikali, tukitaraji kwamba maamuzi yatokanayo na Baraza hili kwa serikali yanahitaji yaheshimiwe.

Mhe. Spika, ni kitu cha kusikitisha sana sana kwamba Baraza letu lenye sehemu ya serikali ndani yake tunapitisha maamuzi kwa asilimia mia moja sote chini ya uwepo wako kama Spika wa Baraza la Wawakilishi, mwisho wa siku kwa kweli hatupati majibu ya aina yoyote. Mhe. Spika, kwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume kabisa kabisa na dhana ya utawala bora katika nchi. Tunaweza tu tukawa na jina na Wizara lakini matendo yanayofanywa yakawa yapo kinyume kabisa na utekelezaji wa dhana ya utawala bora na baya zaidi linalotokea Mhe. Spika, ni kufika pahala ukamkuta Waziri anakebehi yale ambayo yanaamuliwa na Baraza hili.

Mhe. Spika, hali hiyo kwa kweli haitoi afya ya maendeleo ya utekelezaji wa dhana ya utawala bora. Itakapofika wakati tutaweza kuyaeleza haya kwa upana wake lakini naomba tu niseme kwamba masuala haya yanahitajika na serikali chini ya uwepo wako kiogozi wa chombo hiki na chini ya uwepo wa Makamu wa Pili ambaye yeye ndie mtendaji na mtekelezaji Mku wa Shuguli za Serikali katika Baraza tunahitaji sote kwa pamoja tuwe makini katika kusimamia Katiba pamoja na sheria zetu na utaratibu wetu tuliojiwekea.

Mhe.Spika, vile vile napongeza serikali kwa kuwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa sababu kuwepo kwa taasisi hii ni kipimo chengine cha utekelezaji wa dhana ya utawala bora katika suala la kuhakikisha kuna nidhamu katika matumizi ya fedha za umma kwa namna yoyote vile kuwepo kwa Ofisi ya Mdhibiti ni kiashirio kwamba nchi sasa imeamua kupambana na ufisadi, kuwepo kwa ofisi hii ni maamuzi yanayoashiria kwamba kuna matumizi sahihi na nidhamu katika masuala mazima ya matumizi ya fedha za umma.Naiomba Serikali tumeshuhudia mara kwa mara Mdhibiti na Mkaguzi akileta taarifa zake katika Baraza

letu, na tunashuhudia pia Kamati yako ya PAC Mhe. Spika, ikiwasilisha ripoti yenye mapendekezo kwa serikali ili kwa ajili ya kuyafanyia kazi, tunataraji kwamba mapendekezo yatokanayo na Kamati ya PAC yatekelezwe kwa ukamilifu wake ili tuone kwamba dhana hii inakuwa ni sahihi na nchi yetu inajipatia sifa.

Mhe.Spika katika Ofisi hii hii ya Mdhibiti, serikali ina kila jukumu na kila wajibu wa kuhakikisha kwamba inaimarisha kadiri siku zinavyoendelea na inaipatia uwezo ofisi hii ili iweze kusimamia vyema majukumu yake iliyojipangia.

Mhe. Spika, sasa naomba niende katika Wizara ya Katiba na Sheria na huko basi naomba nianze na Mahkama. Mhe. Spika, mahkama ni moja kati ya mihimili mitatu ya dola inayofanya dola la Zanzibar. Mhe. Spika, mahkama inataka isiingiliwe lakini kutoingilia kwa mahkama haina maana kama mahkama ifanye inavyotaka. Taratibu zinaeleza kwamba mahkama inatakiwa iwe huru, lakini naomba niseme kwamba uhuru huo haitakiwi mahkama wafanye wanavyotaka. Inapofikia kwamba sasa tukaona kwamba mahkama sasa inafanya inavyotaka, kinyume na utaratibu, kinyume na sheria ni pahala Baraza hili kwa niaba ya wananchi tuweze kujadili na kuona kwamba mahkama yetu ikoje.

Mhe. Spika, na hili tutakuja kueleza katika ripoti lakini baadhi ya maamuzi yanayofanywa na mahkama kwa kweli yanatia shaka kwamba rushwa imeenea katika mahkama, ninasikitika sana kusema hivi lakini maamuzi yanayofanywa na vyombo vyetu vya mahkama au mahkama zetu zinaashiria kwamba rushwa imetopea katika mahkama zetu tulizonazo. Tutakapofika katika hatua hii, Baraza lako litakuwa lina mamlaka kamili kujadili kwa sababu ile ni taasisi ya umma na taasisi ya umma lazima ifuate sheria tulizojiwekea.

Mhe. Spika, naomba nilieleze hilo nikiamini kwamba Waziri wa Katiba na Sheria na nikiamini kwamba Mhe. Jaji Mkuu watalizingatia hili na kuiangalia kwa jicho la kipekee utendaji wa mahkama zetu kwa maana ya majaji wetu na mahakimu wetu tulionao katika mahkama zetu.

Mhe. Spika, jengine naomba nilizungumzie ni suala zima linalohusiana na Ofisi ya Mrajis tuna tatizo katika Ofisi ya Mrajis na hili linagongana na Ofisi ya Msajili wa Vitambulisho. Ninachotaka nikielezee hapa ni kwamba watu wanapoondoka kwenda kutafuta vitambulisho vya ukaazi, mara nyingi vyeti vyao vya kuzaliwa vinakataliwa na Ofisi ya Usajili wa Vitambulisho. Sasa naliomba hili kwa kumuelekeza Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Waziri anayehusika na vitambulisho Mhe. Dr. Mwinyi ikiwa mwananchi ana cheti ambacho kakipata kwa njia yake anayojiona kwamba ni njia halali, leo atakapokwenda katika Ofisi ya Vitambulisho akaambiwa cheti hiki sicho naomba hapa tuambiwe mwenye ku-*certify* vyeti ni nani? Kati ya Ofisi ya Mrajis ama Ofisi ya Vitambulisho, nani mwenye uwezo wa kusema kwamba cheti hiki ndicho au cheti hiki sicho. Kwa sababu vyenginevyo utamuonea mwananchi ambaye hana hatia yoyote au utamkosesha haki mwananchi hana hatia yoyote. Sasa naomba Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais wakae pamoja watupatie jawabu juu ya suala hili.

Mwisho kabisa nisisitize tu, naomba niishukuru serikali sana kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa msimamo alioutoa kwa niaba ya serikali kwamba serikali itaheshimu maamuzi ya wananchi waliyoyatoa Zanzibar kwa ajili ya Katiba mpya. Ninaishukuru sana serikali na naomba wazingatie hilo. Ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwa ufupi kama ulivyoagiza ili niweze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Kiwani na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, niendelee kuwapongeza Mawaziri wawili chini ya Kamati hii ya Sheria ambao kwa kweli wanaendelea kufanya kazi kwa dhana ile ile ya kujenga na kuendeleza taifa letu. Lakini vile vile nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake kwa ujumla kwa jinsi walivyotuletea ripoti nzuri na iliyo makini sana.

Mhe. Mwenyekiti Kamati hii ni Kamati ya Katiba na Sheria inayoongoza Wizara mbili, Wizara moja ni Wizara ya Utawala Bora na Utumishi wa Umma na Wizara nyengine ni Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, nianze na hii Utawala Bora mna neno ambalo nalipenda sana kulitamka neno hili linaitwa Utawala Bora. Mhe. Spika, utawala bora ni maneno mawili yenye herufi kumi na moja silabi sita. Maeneo hayo mawili maneno rahisi sana kuyataja na ni matamu sana mdomoni lakini ni mabaya sana ukiyatia akilini kwa yule mwenye akili.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu kuna watu wanaamini kwamba Zanzibar ina utawala bora na kuna watu wanaamini kwamba Zanzibar haina utawala bora miongoni mwao ni mimi. Na naamini hivyo kwa sababu kuna misingi ya utawala bora ambayo Mhe. Waziri nakumbuka mwaka jana alituletea kitabu kizuri tu ambacho alitueleza misingi ya utawala bora. Kwa hivyo hoja zangu zote zinakwenda kwenye kitabu kile ambacho ni kitabu halali cha serikali kilichoelezea misingi ya utawala bora ni ipi.

Mhe. Spika, naamini kwamba utawala bora haupo kwa sababu tumeshindwa kusimamia misingi ya utawala bora kwa mujibu wa maagizo yenyewe ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nianze kwenye uwazi.

Mhe. Spika, ili utawala bora uwe utawala bora lazima kuwe na uwazi, uwazi katika serikali, uwazi hata katika shughuli zetu za kijamii. Lakini Baraza hili Mhe. Spika, tangu mwaka juzi liliidhinisha zaidi ya dola milioni kumi na nane kwa mradi wa *E-government.* Na tukaomba kwamba tuletewe ripoti kwa sababu Baraza hili lilisema kwamba hizi fedha ni nyingi lakini serikali ikajenga hoja kwamba sio nyingi na zitafanyika kwa ufanisi, tukaomba tuletewe ripoti humu juu ya matumizi ya fedha hizi za umma.

Taarifa nilizonazo Kamati yenyewe ya Katiba na Sheria imeandika barua hata kwa Waziri wa Fedha kupatiwa ufafanuzi wa matumizi haya ya fedha kilichopo ni kimya, hii maana yake hakuna uwazi na kama hakuna uwazi maana yake hakuna utawala bora. Kwa hivyo hoja yangu ya kwanza nasema kwamba tumeunda Wizara ya maneno matamu yenye herufi kumi na moja silabi sita lakini hatuyatekelezi. Kama hakuna uwazi katika mambo yako maana yake hapana utawala bora.

Mhe. Spika, msingi mwengine muhimu wa kuzingatia na hata ripoti wameeleza ni suala la uwajibikaji. Uwajibikaji ni jambo moja ambalo litafanya nchi iende kwa kasi mno kimaendeleo,

lakini Zanzibar tumeshindwa kuwajibika, hususan viongozi tumeshindwa kuwajibika, tunazungumza tu tukiwakutia wananchi hasa wananchi wa chini vijijini huko tumekuwa tukiwadanganya tu kwamba tuko makini tunawajibika lakini hatuwajibiki. Msingi wa uwajibikaji maana yake ni kufanya vitendo vilivyo wazi chini ya sheria. Lakini Mhe. Spika, Baraza hili limepitisha zaidi ya Kamati nne ziko zaidi ya ripoti tatu nyuma, kama wenzangu walivyozungumza tumejadili, tumepitisha hakuna mtu aliyepinga si Waziri, si mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa kawaida lakini hakuna hatua zilizochukuliwa, kilichopo ni kimya tu. Hii ina maana uwajibikaji hapana na kwa hivyo hapana utawala bora.

Mhe. Spika, hata ugawaji wa raslimali za serikali ni dhaifu sana tunategemea sisi kama Wawakilishi wa kawaida tugawe raslimali za nchi kwa maana ya fedha na imani nyengine kwa kuangalia uwiano leo ukifanya utafiti hizi Wizara zetu hizi kuna Wizara A,B na C kuna wengine wanapata fedha nyingi, na wengine wanapata fedha kidogo huo si utawala bora. Mhe. Spika, kwa mfano juzi Wizara ya Mhe. Waziri Utawala Bora ameajiri walimu mia nne na ishirini. Hapa Zanzibar Barazani hapa tumekuwa shahidi tukiambiwa kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi una ongezeko la walimu walio wengi maana yake hawahitajiki wanalazimika kupunguzwa kwenda Pemba, ama Kaskazini Unguja au Kusini Unguja. Lakini walimu 420 walioajiriwa ni walimu 98 tu ndio waliopelekwa Pemba ni sawa na asilimia 23.

Sasa nikiangalia takwimu za sensa, Mkoa ambao unaoongoza kwa idadi kubwa ya watu ni Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa wa pili ni Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mkoa wa tatu ni Mkoa wa Kusini Pemba, Mkoa wa nne ni Mkoa wa Kaskazini Unguja na wa mwisho kwa idadi ya watu ni Mkoa wa Kusini Unguja. Kwa nini ugawaji wa walimu na raslimali nyengine haziendi kulingana na idadi ya watu? Leo Wilaya ya Mkoani mathalan yenye upungufu wa walimu zaidi ya 200 tumepelekewa walimu 14. Mkoa wa Mjini ambao una idadi kubwa ya walimu hawahitajiki ndio wameletwa walimu wengi, maana yake nini? Maana yake hatuna ugawaji raslimali katika nchi. Kwa hivyo kwa msingi huu Mhe. Spika, ni dhahiri kusema kwamba utawala bora Zanzibar uko mbali sana, tunaangalia utawala kwa msingi wa uchaguzi tu kwamba tupige kura tupate viongozi, huo si msingi wa utawala bora peke yake.

Mhe. Spika, suala la walimu kuna maslahi ya walimu wa kisomo cha watu wazima. Walimu kutoka Unguja Mhe. Spika, tangu mwezi Julai, 2012 walipewa posho maalum la shilingi 30,000/- lakini mwalimu huyo huyo Pemba alikuwa anapewa posho shilingi 10,000/- huo si msingi wa utawala wala si ugawaji mzuri wa raslimali. Lakini Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri kwamba bado serikali yake chini ya Wizara yake ina kazi kubwa ya kufanya utafiti hasa katika ajira na masuala ya mishahara. Juzi alipokuwa anajibu swali langu aliniomba nimpe maelezo kama kuna ushahidi, leo sitaki nimtajie namwambia tu nikiamini yeye ni muungwana na mfuatiliaji namtuma aende Mamlaka ya Maji kuna tatizo la ajira, hatuwezi kuwaruhusu wananchi wetu kupata mishahara miwili ndani ya serikali hii. Leo nakwambia kwa ufupi nakuomba nenda tukijaaliwa ikifika bajeti uje utwambie haya niliyoyasema.

Mhe. Spika, nchi hii leo ina wafanyakazi wana mishahara miwili mmoja uko wizara hii mmoja uko wizara nyengine, hayo yanajulikana na kama hayajulikani ndio tunayasema basi achukuliwe hatua. Hata hili likinyamazwa kimya maana yake huwezi kuamini kwamba pana utawala bora kwa nini mtu mmoja apate mishahara miwili. Kwa nini asipate mishahara miwili Rais, kwa nini

asipate mishahara miwili Spika, kwa nini asipate mishahara miwili Jaji Mkuu. Apate mishahara miwili mtu wa chini na huku Idara na Wizara ikimjua si utawala bora.

Sasa Mhe. Spika, nadhani tuwe makini sana hatuwezi kuwafanyia haki wananchi wetu ikiwa mambo yanafichwa, tuwe wazi, tuwajibike na tuchukue hatua. Kama huwezi kuchukua hatua maana yake huwezi kuwa kiongozi. Kama unashindwa kumkemea mtoto wako aliye chini nyumbani mwako huwezi kumkemea mtoto wa mwenzio. Tuanze kuajibika kwa kuanza nyumbani kwetu kwanza kwa maana kwamba kila mwenye wizara ashughulike na wizara yake hatimaye serikali nzima isafishe uovu. Nchi hii Mhe. Spika, mimi naamini si maskini kiasi hicho, tuna tatizo la kulinda watu kwa makusudi.

Mhe. Spika, juzi hapa tumetoa suala la wizi Idara ya Ardhi waziri akasema kwamba maana yake linafatiliwa *CAG* imegundua, kama *CAG* imegundua kuna wizi Idara ya Ardhi kwa nini hatujaiona kwenye ripoti ya *CAG*. Lakini taarifa ambazo mimi ninazo Mhe. Spika, kwamba mtu mwenyewe aliyefanya uovu huo amekiri kwamba nimefanya uovu lakini serikali imeshindwa kumsimamisha, serikali imeshindwa kuchukua hatua. Taarifa ambazo zipo Mhe. Spika, kwamba tayari anaanza kulipa deni kidogo kidogo huo si utawala bora. Kama amechukua shilingi mia kulipa ndio dawa yake basi turuhusiwe, mimi nifungieni benki mule siku moja nitoke baadae mnambie lipa, nitalipa. Lakini msingi sio huo Mhe. Spika, huwezi kuwajibika kwa kulipa deni, kama kulipa deni ndio msingi ndio adhabu yenyewe basi mimi nifungiwe benki.

Mhe. Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma usiendelee tena kupiga mabao namna hiyo sio nidhamu nzuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika nakushukuru. Kwa hivyo, kuchukua hatua kwa kumwambia mtu jifiche baadae utalipa tu uondoke si utawala bora na kama hivyo ndivyo Mhe. Spika, tusingeweka askari mabenki, tungewaacha wananchi wakaingia benki wakachota fedha halafu tukawaambia lipeni kidogo kidogo. Leo serikali inaambiwa na Wawakilishi kwamba a, b, c ni maovu hakuna hatua, kubwa mtu anakwambia basi tusaidie, iwe nini.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Omar Ali Shehe alinambie neno kubwa sana, alinambia yeye kuanzia bajeti ijayo atawashauri wananchi kila mtu aibe, mimi nilimshangaa sana Mhe. Omar Ali Shehe. Nikamuuliza kwa nini? Akanambia kwa sababu nimesema sana hakuna hatua, kumbe tafsiri yake ukisema unakuwa adui ukiiba mwema.

Mhe. Spika, nimalizie najua muda wako mfupi nimwambie Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria nina ma-*document* hizi zote ni kesi, ni kesi ambazo zimetolewa kutoka Mahkama ya Ardhi mpaka Mahkama Kuu, zimeamuliwa kwamba ni kesi halali wananchi wameshinda hakuna utekelezaji, hatuwezi kusema kuna utawala bora, ikiwa Mahkama yenyewe imeamua kesi hii ni halali kwa mtu A, kesi hii ni halali kwa serikali, lakini ufuatiliaji hakuna tu siwezi kusema kuwa kuna utawala bora katika nchi.

Mhe. Spika, niwaombe sana mawaziri wetu wawili wamekabidhiwa dhima kubwa ndani ya nchi wachukue hatua, isiwe tu kulalamika kwamba hatua, hatua, hatua, hatua ni uajibikaji na misingi ya sheria ipo. Mhe. Spika, Waziri wa Katiba na Sheria ana dhima kubwa ya kulinda haki za watu

ndani ya nchi hii, Mahkama ikiamua jambo hili liwe hivi maamuzi halali serikali lazima itekeleze yakivunjwa kwa nguvu huo si utawala bora.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo machache nasema kwamba Kamati lazima ishauri wizara hizi mbili wawajibike kwa vitendo, dhana ya utawala bora na utawala wa sheria uende kwa vitendo na usiende kwa maneno. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya ripoti hii ambayo iko mbele yetu hapa ya Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati wanaoongozwa na Mwenyekiti wao Mhe. Naibu Spika, wa Baraza letu la Wawakilishi Mhe. Ali Abdalla Ali akisaidiana na Mwanasheria mahiri ndani ya Baraza hili Ndugu Ismail Jussa Ladhu, pamoja na wajumbe wengine ambao wamo katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba nimefurahishwa sana na maagizo haya ambayo kamati yaliyatoa katika wizara hizi husika hususan katika Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Spika, katika wizara hii ambayo kwa leo nimeamua kuichangia katika eneo hili la kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi baina ya wananchi, viongozi na watendaji wa serikali na pia kufuatilia suala la rushwa Mahkamani ambapo linagundulika katika maeneo yetu.

Mhe. Spika, Katiba yetu ya Chama cha Mapinduzi ibara ya 5 inaelekeza kwamba, “Kila Chama cha Siasa kinataka kuongoza serikali na malengo makuu ya kuongoza serikali ni kuwatumikia wananchi wake”. Mhe. Spika, ukiangalia malengo makuu ya Katiba yetu ya Chama cha Mapinduzi ina malengo sahihi na ina dira ambayo inalenga kuwasaidia watu ili waondokane na matatizo ambayo yanawakabili, na katika nchi yetu ya Zanzibar baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 jambo kubwa ambalo Rais wetu wa Kwanza wa Zanzibar, Mhe. Abeid Amani Karume ambalo lilikuwa linampa tabu sana lilikuwa ni suala la ardhi kwa namna ambavyo wananchi wa Zanzibar walikuwa wakinyanyaswa. Ndio maana baada ya Mapinduzi Rais Karume alifikia mahala pamoja na serikali yake wakafikia maamuzi kusema kwamba, “Kwa sababu tumepindua na Waafrika hususan Wazanzibar wote ni masikini sasa tutawagawia eka kila mmoja atakuwa na eka tatu kwa ajili ya kujiendeleza kimaisha”. Hili ni jambo kubwa sana la ardhi katika nchi.

Tukiangalia mfano wa ndugu zetu wa Rhodesia kule iliokuwa zamani ambayo sasa ni Zimbabwe wale watu wana matatizo ya dunia kwa sababu ya suala la ardhi. Lakini kwa upande wetu baada ya maendeleo ya uhuru wetu ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar wananchi wetu wamekuwa wakidhalilika sana katika suala la ardhi suala ambalo ndio *source* na mashumuni makuu ya Mapinduzi yetu ya mwaka 1964 hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, sio siri wala sio jambo la kufurahisha kuona kwamba tunapotoa maagizo katika maeneo yanayohusika kwa mfano katika sekta hii ya ardhi, utekelezaji wake tunakuta kuna taarifa tuta, tuta, tuta, hakuna jambo ambalo linaweza kufikia pahala likawafurahisha wananchi wetu ambapo sisi tuko katika madaraka kwa ajili ya kuwatumikia. Hili ni tatizo.

Tumetengeneza sheria nyingi, tumefanya semina nyingi, tumeelekeza kwa wingi, lakini hakuna jambo ambalo linaudhi kwa wananchi wetu kwa sasa kama suala la ardhi.

Mhe. Spika, ndugu yangu ana kesi pale alikuja kuthibitisha kwamba anazo zinahusiana na masuala ya ardhi, sisi hizo kesi hata hatujaja nazo wengine, lakini ni nyingi, ni kubwa, na zinasikitisha Mhe. Spika. Sasa tunaiomba serikali wananchi wanapotoka wakienda ngazi moja nyengine, mpaka wakafikia juu wakenda kuomba kutatuliwa matatizo yao yanayowahusu kutokana na ardhi na mwisho wakafika ngazi za kuu kabisa, tunaomba viongozi wetu mnapoletewa kesi hizi mzitolee maamuzi. Uwezo wa wananchi kusubiri huku chini sasa ushakuwa una mashaka, ushakuwa mzito, tunaomba sana tujitahidi kutatua matatizo ambayo yanakabili wananchi wetu hususan katika mambo ya ardhi.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakuja katika taasisi hiyo hiyo ya utawala bora hususan katika maoni ambayo yametolewa au ushauri na kamati. Kuna maoni matatu hapa ukurasa wa 38, wanasema kwamba, “kamati inashauri serikali kuzidisha umakini katika suala la rushwa na uhujumu wa uchumi. Tukiachilia mbali suala la rushwa sasa hivi na tuje katika uhujumu wa uchumi.

Uhujumu wa Uchumi Mhe. Spika, si lazima mtu aje amnyang’anye mtu au aje amuibie mtu au katika namna nyengine yoyote ile ambayo itakuwa mimi na wewe tunaielewa na wajumbe wengine. Hata mtu anapopewa majukumu ya kuweza kuleta maendeleo katika nchi akatoa sababu zisizokuwa na msingi pia ni uhujumu wa uchumi.

Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati yako ya Fedha na Uchumi kipindi kifupi tu nyuma ulitutuma tukafanye kazi maeneo tofauti ndani ya Zanzibar yetu na wengine tukavuka tukenda mpaka upande wa pili wa Muungano. Ndani ya Zanzibar Mhe. Spika, katika sekta yetu ya Kamati ya Fedha tulipewa orodha ya miradi isiyopungua mia tatu na ushei. Katika miradi ile kwa kweli kuna mambo ya kuhudhunisha sana, kuna miradi ambayo ina miaka sita, minne, bado haijakamilika na serikali inategemea kwamba wale ambao wamekuja kuomba kuendeleza miradi ile serikali iweze kupata pato pale ambalo linaweza kusababisha nchi yetu ikaweza kwenda vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe nashindwa kuunganisha mchango wako na ripoti iliyoko mezani. Kwa mfano alipokuwa akizungumza Mhe. Hija Hassan alikuwa anazungumzia masuala ya ardhi na mambo mengine lakini kwa mnasaba yamekwenda Mahakamani lakini hatua hazikuchukuliwa. Kwa maana Mahakama imetoa maamuzi jambo ambalo liko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria lakini kwa upande mwengine suala zima la utawala bora. Sasa hizi unazoleta wewe najaribu kusikiliza sana lakini nashindwa sasa kuunganisha na ripoti hizi ziliopo mana mengine yangekwenda kwenye Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi nayo bado, mengine yangekwenda kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi pia bado. Sasa changia katika suala liliopo mezani.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Spika, nilikuwa nakuja katika maoni ya kamati namna ambavyo walikuwa wameelezea suala la uchumi. Nilichotaka kukizungumza hapa ni suala la ukamilishwaji wa baadhi ya mambo.

Tukiendelea mbele Mhe. Spika, ni kwamba katika suala zima la hawa wawekezaji ambao wana matatizo haya naona bora tuliache tutakuja kuliunganisha katika wakati wa bajeti.

Mhe. Spika, suala la pili lilikuwa linahusiana na suala la Kamati kusisitiza kuajiriwa kwa maafisa waadilifu na waaminifu na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa. Hili ni jambo zuri na tunahimiza taasisi zinazohusika zichukue hatua kuhakikisha kwamba tunapata watu ambao wana uwezo na kuweza kusaidia ili tuone kwamba masuala yetu haya yanakwenda kwa mujibu wa taratibu ambazo tumejiwekea.

Na la mwisho kabisa kamati ilichukua jukumu la kumpongeza Rais kwa kuweza kufikiria kuanzisha mamlaka ya kuzuia rushwa. Pamoja na mamlaka hii kuanzishwa, Mhe. Spika, tunaomba kuhimiza vile vile na watu wengine wa ziada ambao wataweza kusaidiana na taasisi hii ili shughuli za kuzuia na kupambana na rushwa ziweze kwenda vizuri zaidi.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu. Ahsante Mhe. Spika.
Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa ombi langu la kuomba dakika tano kuchangia na kunikubalia *In shaa Allah*. Lakini la pili Mhe. Spika, nitajitahidi kujali muda wako na sitegemei kama nitamaliza dakika hizo. Nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, miongoni mwa mawaziri ambao tunawategemea waadilifu, watendaji wazuri na wafuatiliaji wa shughuli zao basi Mhe. Waziri wa Wizara hii anastahiki kupigiwa mfano na pongezi za dhati kabisa katika Baraza lako tukufu. Hii inaonesha jitihada zake na inaonesha pale ambapo tunapeleka maswali na vile ambavyo anaweza kuyasaidia na kuyatatua kwa muda wa haraka.

Mhe. Spika, baada ya hilo kubwa ninalotaka kulizungumza ni jitihada za uanzishwaji wa Chuo chetu cha Utawala wa Umma kule Tunguu. Jitihada zimeonekana chuo kimeanzishwa, pamoja na na mapungufu yanayoonekana hivi sasa kama Mhe. Waziri alivyokiri kwamba wanategemea kumaliza matatizo yale katika njia za haraka katiak masuala mazima ya uzio ili kuweka ulinzi na usalama mzuri wa mali za chuo kile.

Lakini Mhe. Spika, kubwa ambalo nataka kulizungumzia ni kumuomba Mhe. Waziri kwa dhati ya nafshi yangu ndani ya Chuo cha Utawala wa Umma kumejitokeza mambo ambayo si mazuri. Mambo ambayo sielewi lakini nina imani kwamba inawezekana atakuwa keshayapata Mhe. Waziri kama hajayapata basi nataka nimsaidie ili ayachukue na kwenda kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, hivi karibuni katika chuo hicho inasemekana kumetokea ubadhirifu wa pesa za Kitanzania zisizopungua 61.3 milioni. Pesa hizi ni malipo ya wanafunzi na kadhia hii Mhe. Spika, iligundulika baada ya wanafunzi kufanya mitihani na wengine kuzuiliwa *results* zao. Sasabu ikaonekana kwa nini tatizo hili liwe, lakini kilichobainika kwamba kuna fojari za risiti, kuna risiti ambazo zilikuwa zinatambulikana Wizara ya Fedha zilitiwa ndani ya mtandao na kuna risiti ambazo zilikuwa hazitambulikani na inasemekana risiti hizi *cashier* alizitumia baada ya kupokea pesa za wanafunzi.

Mhe. Spika, sasa nimuombe Mhe. Waziri kama nilivyotangulia mwanzo kusema ninamuamini na nina imani kwamba kadhia hii ataifanyia kazi hili ni tatizo kubwa, tatizo ambalo mara nyingi tunakuwa tunalipigia kelele juu ya masuala mazima ya ubadhirifu wa pesa za walipa kodi, hili ni tatizo na naomba lifanyiwe kazi.

Lakini jengine ambalo nataka nizungumze Mhe. Spika, katika chuo hicho ni suala zima la mishahara. Mhe. Spika, taarifa hii ina muda mrefu si chini ya mwaka mmoja taarifa sijui kama wizarani imeshafika juu ya suala la kutokuwiana kimishahara baina ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tunguu na Chuo cha Fedha Chwaka, Chuo cha Kilimo Kizimbani na Chuo cha Habari. Sasa nimuombe Mhe. Waziri nalo hili kwa moyo wa huruma kabisa basi aliangalie na kuweza kulifanyia kazi ili wale walimu wetu ambao wanajitolea kufanya shughuli zao waweze kuzifanya shughuli zile kwa kuwa na imani na moyo wa kizalendo katika kuwasaidia wanafunzi wetu.

Mhe. Spika, nilikuwa nina mengi sana lakini kwa kujali muda yote naamua kuyaweka na mengine nitampelekea Mhe. Waziri kwa maandishi ili ziweze kuwasaidia kuweza kutatua kero katika wizara yetu hii ya Utawala Bora. Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru kwa dhati kabisa kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono ripotoi hii ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ya kutoa machache katika maelezo ya kamati hii pamoja na mawaziri husika. Kwanza niwapongeze mawaziri wote wawili kwa kuweza kusimamia vyema wizara zao, aidha, niipongeze kamati hii kwa utendaji mwema katika shughuli zao.

Mhe. Spika, nchi hii ni nchi inayokwenda kikatiba, kisheria na utawala bora; kwa hali ya nchi ilivyo watu wengi tunaowasomesha baada ya kumaliza masomo yao wanategemea kupata ajira serikalini, kwa kuwa bado hatujawaandaa kutegema kwenye sekta binafsi bado wanategemea kwenye sekta ya umma na sekta ya uma iko chini ya utawala bora. Kwa hivyo, wengi wa vijana wetu wanategemea ajira huko serikalini, ajira ambayo Mhe. Spika, hivi sasa ina mbinde, kupata ajira ni tatizo gumu kidogo.

Mhe. Spika, bado kuna matatizo madogo madogo kutokana na marekebisho ya mishahara iliyofanyika kipindi kilichopita, zaidi kwa walimu bado wana malalamiko kuwa mishahara yao haiku vizuri ama wengine hawakufaidika kabisa na waliofaidika kuna madai tofauti yao bado haijarekebishwa. Kama mishahara ilikuwa inaanza Julai kuna wengine marekebisho yao yalifanyika miezi ya mbele. Sasa hii tofauti Julai na pale alipopata kurekebishiwa hapa kati *area* zao bado hawajapatiwa. Wako walimu walio na matatizo ya aina hiyo.

Sasa ili kuondoa matatizo Mhe. Spika, serikali ni vyema ikaandaa *scheme of Service* ya wafanyakazi wake. Vyenginevyo tunaongeza mishahara lakini mtu aliyeajiriwa mwaka na mtu aliyeajiriwa miaka 30 nyuma huwa tofauti yao ni *increment* 2-3 ni tatizo gumu, sugu kweli kweli na linamvunja moyo mfanyakazi huyu aliyetumikia muda mrefu na tofauti yake mfanyakazi mpya ikawa ni ndogo mno na ilichukuliwa hatua ya kuondosha matatizo hasa hawa wanaofanya kazi miaka 39 wako ukingoni kustaafu.

Mhe. Spika, katika miezi ya hivi karibuni Wizara ya Elimu ilikuwa na mpango wa kuwaajiri walimu kadhaa na walitoa matangazo, vijana wakaomba na hatimaye yako majina yaliyotundikwa katika *floor* za wilaya kuwa huenda hawa wakaajiriwa na wakafanyiwa usaili. Lakini hadi leo hali hii iko kimya haijuliji wapi ilipokwama ni kwenye uajiri, au kuna uchunguzi unaofanywa haujakamilika na kama kuna uchunguzi uliokuwa haujakamilika hivyo vijana wetu tunawachunguza kiasi gani hadi ikubalike kuwa huyu anafaa kuitumikia serikali. Kwa sababu zaidi ya miezi minne lakini bado hiyo ajira haijawafika vijana, sisi ndio wanaotuuliza Mheshimiwa vipi, kumbe na sisi hatuna jibu kwa sababu inayoajiri ni serikali wala si Baraza la Wawakilishi.

Kadhalika kwenye Vikosi vya SMZ, navyo hivi karibuni vilitaka kuajiri vilitoa maombi ya ajia, lakini mpaka leo navyo halikadhalika ajira hiyo bado vijana wetu hawajachukuliwa. Kwa hivyo, ningeomba kujua kuna lipi hasa linalokwaza shughuli hizi ambapo serikali tayari imetangaza, vijana wamejitokeza lakini na serikali bado ikakaa kimya bila ya kuchukua hatua yoyote ya kuwaajiri au kuwajibu chochote kile.

Mhe. Spika, nigusie kidogo katika Wizara ya Katiba na Sheria na nianzie kwenye Mahkama. Mhe. Spika, Mahkama zetu sasa kuna mrundikiano wa mkubwa, tuanzie zile Mahkama ziliopo yaani Mahkama ya Mwanzo, Mahkama ya Wilaya, Mahkama ya Mkoa na Mahkama Kuu. Sasa Mahkama hizi zina Mahkama nyengine ambazo hata hivi karibuni tumeanzisha Mahkama ya Biashara hivi juzi tu, Mahkama ya Ardhi, Mahkama ya Watoto na kadhalika. Kwenye kuchangia Mahkama ya Biashara niliuliza swali ambalo sikupata jibu kwa Mhe. Waziri, hebu mgawanyiko wote huu wa Mahkama ni kweli tunao Majaji na Mahakimu wa kuweza kuhudumia?

Kwenye kujumuisha alisahau kunijibu je, ni kweli tunao Mahakimu wa kuweza kuhudumia au tunaunda tu halafu tunakaa, kama hatuna vijana wengi wapo waliomaliza fani hii ya sheria na wanangoja ajira. Kwa hivyo, kama hakuna ningeomba watangaze na vijana wapo wenye fani hiyo ya sheria ili waweze kuwaajiri.

Mhe. Spika, nije kwenye usajili wa vizazi na vifo, hapa kuna matatizo zaidi ya wale ambao hawakupata kusajiliwa mapema. Kuna urasimu mkubwa wa mtu ambaye hakusajiliwa mapema katika kizazi kuweza kupata cheti cha kuzaliwa, mzunguko ni mkubwa na hivyo akifanikiwa basi malipo yake ni makubwa mno. Ningemuomba Mhe. Waziri kwanza urasimu upungue na kadhalika haya malipo yapungue zaidi, ada iliyopangwa kwa cheti kama hiki ni kubwa ambapo watu wetu walio wengi wanashindwa kuilipa. Kwa hivyo, ningeomba urasimu upunguzwe na yule anayefanikiwa pia ada ipungue.

Mhe. Spika, kutokana na hali hii wizara hii ningeiomba iwe makini, kwa sababu wako vijana waliozaliwa kwa bahati mbaya hawana cheti, lakini wazazi wao baada ya kuzaliwa wanakwenda kujisajili kuwa mtoto fulani bin fulani kazaliwa tarehe kadhaa, lakini kwa kutokujua zaidi wazazi hawa hawakumtafutia cheti cha kuzaliwa. Ningeiomba wizara hii ya Katiba na Sheria magamba haya ya kuzaliwa ya kliniki wayakubali ili yaweze kutumika katika taasisi nyengine za vijana waweze kupata mahitaji yao wanayohitaji ya lazima. Kama pengine kuweza kupata kitambulisho cha Mzanzibari, lile gamba la kliniki likubalike kwa sababu nalo linatoka katika taasisi ya serikali ingawaje hakwenda kupata cheti rasmi lakini kimetolewa kwenye taasisi rasmi ya serikali.

Kwa hivyo litumike kama kielelezo cha cheti kuzaliwa. Hivyo naiomba wizara hii ilifikirie na ikiwezekana ilikubali na izitake taasisi zinazohusika anayeleta gamba hili la kliniki wakubaliwe kama cheti chake cha kuzaliwa.

Mhe. Spika, ingawaje mimi hukunipangia muda lakini ili na wenzangu waweze kuchangia naomba nimalizie hapo. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, *wallahi* laadhimu nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi hii alau na mimi kidogo nikatoa yale machache niliyokuwa nayo.

Mhe. Spika, mimi ninataka nianze moja kwa moja kuwapongeza kwanza mawaziri wote wawili; Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria wanajitahidi katika majukumu yao. Lakini kama kawaida changamoto ni kitu cha kawaida na ninaamini tukishirikiana kwa pamoja basi changamoto tutaweza kuzirekebisha.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze ukurasa wa 35 kwenye utekelezaji wa maagizo ya kamati. Idara ya Utawala Bora Mhe. Spika, wameeleza hapa kamati kuipatia ufumbuzi migogoro ya ardhi baina ya wananchi. Mhe. Spika, suala hili kwa kweli limekuwa ni suala sugu na namuomba sana Mhe. Waziri wa Utawala ashirikiane na Mhe. Waziri wa Ardhi pamoja na Waziri wa Makamu wa Pili wa Rais ili kuweza kuyasaidia sana matatizo haya, kwa sababu kwa kweli yamekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wetu.

Lakini Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 38 katika hii ripoti inazungumzia katika masuala ya maoni na ushauri wa kamati, inasema kamati inaishauri serikali kuzidisha umakini katika suala zima la rushwa na uhujumu wa uchumi.

Mhe. Spika, mimi kwanza naishukuru serikali kwa kuanzisha kile kitengo cha kupambana na rushwa. Lakini Mhe. Spika, nina masikitiko makubwa sana kwamba tumeanzisha sheria na hiki kitengo lakini mpaka hivi sasa bado hatujakipa nafasi nzuri hasa ofisi na vitendea kazi. Tunaomba sana kwamba kitengo hiki ni muhimu kwa sababu hiki ndio kielelezo bora katika masuala mazima ya utawala bora. Kwa kweli kitengo hiki mimi ninakiomba sana kwamba wafuatilie sana mijadala yetu ya Baraza la Wawakilishi, tunazungumzia mambo mengi, maovu mengi yanayofanyika na baadhi ya watendaji wetu wasiokuwa waaminifu ili na wao, kwa sababu Mhe. Spika, na hawa kazi yao kubwa nafikiri hapa ndio kianzio cha kazi yao ndani ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo naomba serikali pamoja na kwamba tumeanzisha lakini tukiboreshe ili kuweza kufanya kazi na kujenga imani kwa wananchi wetu.

Lakini vile vile Mhe. Spika ukurasa wa 40 katika ripoti hii ya Kamati imeelezea suala zima kamati inaiagiza Tume ya Utumishi Serikalini ijenge tabia ya kutembelea na kukagua ofisi za serikali ili kuweza kubaini jinsi gani nidhamu ya maofisi inashuka na watu kufanya kazi kwa mazoea bila ya kujali haki na wajibu wao.

Mhe. Spika, hili nalizungumza lakini pia katika ripoti yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nililizungumzia suala hili. Na kwa kuwa Kamati ya Katiba na Utawala Bora wameliona mimi nadhani hii ndio inaonesha kwamba kweli tuna udhaifu mkubwa katika utendaji

wa serikali. Wengi wanafanya kazi kwa mazoea lakini kama nilivyozungumza juzi kwamba Mhe. Spika, hivi sasa kuna watendaji wanafika kazini serikalini tokea asubuhi mpaka anaondoka saa tisa na nusu hakuna kazi yoyote anayoifanya. Lakini vile vile ukiangalia kuna wengine ambazo wanafanya kazi ambazo zipo nje ya majukumu yao.

Sasa mimi nadhani Mhe. Spika, nakubaliana kabisa na ushauri wa kamati kwamba kweli katika suala hili Tume ya Utumishi Serikalini iweze kufanya *research* iweze kuwapitia aidha kuwapa mafunzo na maelekezo lakini vile vile kuwasimamia katika shughuli zao za kazi. Lakini vile vile nazungumzia suala zima kwenye ukurasa huu huu 41 kwenye Kamisheni ya Utumishi ya Umma, kuna kifungu cha 4 kinachosema "Kupokea na kushughulikia rufaa katika mamlaka za kinidhamu lakini vile vile kupokea kushughulikia dhidi ya watendaji wakuu kwenye taasisi za umma".

Hili Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma ajaribu sana kulifuatilia hasa katika suala zima la watendaji na vile vile hatua za zinazochukuliwa za kinidhamu. Mhe. Spika, kuna kadhia kubwa ipo katika Ofisi ya *CAG* kwenye suala zima la wafanyakazi ilifika pahala waka-*suspended* miezi sita hawana kazi wanayoifanya, wanahangaishwa hawajui hatma.

Nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri suala hili aweze kulishughulikia kwa karibu ili haki itendeke, kama wana matatizo basi hatua za kinidhamu zichukuliwe kama tunavyoshauri. Lakini kama hawana tatizo lolote Mhe. Spika, naomba suala hili liweze kushughulikiwa ili haya malalamiko yaweze kuondoka.
Mhe. Spika, vile vile ukurasa wa 43 wa kitabu hiki katika maoni ya kamati. Kamati inasisitiza kuwepo kwa mawasiliano yaani *network* ndani na nje ya Ofisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili wananchi wapate kuelewa mabadiliko na mwenendo wa serikali. Mhe. Spika, hili vile vile naishukuru Kamati ya Utawala Bora kwa sababu hata na mimi katika ripoti yetu ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa hili tulilizungumza.

Hili Mhe. Spika, litaweza kutekelezeka vizuri iwapo wale maafisa habari waliokuwepo katika wizara mbali mbali, nililizungumza hili katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini nikasema hili nimelizungumzia kwa sababu ni wizara ambayo kamati yangu ilikuwa inaisimamia. Lakini kimsingi Mhe.Spika, maafisa habari katika wizara zote bado hawajakabidhiwa au hawapewa majukumu yao ipasavyo au kuna ukosefu mkubwa wa mafunzo na vitendea kazi. Hili Mhe. Spika, limejitokeza katika maoni na ushauri wa kamati. Kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa Waziri hili, hili ni la mawaziri wote waweze kulichukua na kulifanyia kazi. Maafisa habari hawa wakiweza kupewa taarifa zote zinazohusika, wao ndio wataweza kufanya kazi yao ili kuwa kiungo baina ya serikali na wananchi kwa kujua ni kazi gani ambayo serikali inazozifanya hata Mhe. Rais katika ziara zake mbali mbali na yeye pia alikuwa akilisisitiza vile vile.

Mhe. Spika, ukurasa wa 49 wa ripoti hii ya kamati inasema kwamba katika eneo la Mahakama kwenye changamoto, Mahakama imefanya malipo kwa assessors mbali mbali wanaohudhuria katika kesi mbali mbali kuanzia pale walipokuwa hawajalipwa mpaka mahudhurio ya mwisho.

Mhe. Spika, hii ni changamoto na mimi nathubutu kusema kwamba bado kuna ma-*assessors* wengi, mimi mwenyewe nimeonana nao wakanielezea kadhia yao. Kuna ma-*assessors* ambao

wanadai malimbikizo yao ya zile stahiki zao kwa miezi 33. Sasa hapa katika hii ripoti imeandikwa kamba imefanya malipo kwa ma-*assessors* kuanzia kusimamia kesi mbali mbali kuanzia pale walipokuwa hawajalipwa mpaka mahudhurio ya mwisho.

Sasa Mhe. Spika, namthibitishia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria anayeshughulikia masuala ya Mahakama suala hili bado ni tatizo na ninaomba sana aweze kulifanyia kazi kuwamalizia haki yao. Lakini vilevile hili nitaweza kuliunganisha na malipo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.
Mhe. Spika, tulipokuwa kwenye kikao cha bajeti hapa nilizungumza suala la haki au kupandishwa au kurekebishiwa mishahara yao Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao kwa kweli ipo tofauti sana na wale Mahakimu wenzao wa mikoa. Mhe. Waziri aliniahidi hapa na kwa sababu nilizuia bajeti, aliniahidi kwamba Mahakimu wale wa Mahakama ya Mwanzo mishahara yao itaweza kurekebishwa na mheshimiwa alikiri, akasema kwamba kulikuwa kuna fungu kubwa la fedha ambalo lipo katika wizara yake amelitenga na fungu hili litaweza ku-*commodate* ile nyongeza ya mishahara ya Mahakimu wa Mwanzo.

Lakini vile vile Mhe.Rais katika siku ya ile ya inayoitwa Mahakimu ni siku ya binadamu kama sikosei, alitoa ahadi Mhe.Rais baada ya risala ya wale Mahakimu wa Mwanzo kuomba kwamba wao wamesahauliwa katika kurekebishiwa ile mishahara yao.

Mhe. Spika, hili suala kwamba fungu la bajeti kuwa waziri alisema lipo na mpaka leo bado halijafanyiwa kazi. Mhe. Spika, unajua unaangalia saa yako najitahidi kwenda haraka haraka, lakini vile vile ukurasa wa 50 Mhe. Spika, mimi nataka kupongeza sana kwa Mhe. Waziri kukubali ile hoja yetu ya kutenganisha Mahakama za Watoto na kwamba sasa hivi kuna Mahakama za Watoto, na tunashukuru angalau alau kesi Mahakama ile itakuwa japo wiki au sijui mwezi mara mbili nilisoma kwa haraka haraka, lakini kwa kweli hili tunalipongeza na tunaomba basi zile kesi za ubakaji basi na udhalilishaji kwa watoto ziweze kukuchukuliwa hatua za haraka.

Kwa kumalizia Mhe. Spika, ninataka nipongeze sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Mhe. Spika, ukiangalia kitabu hiki kwenye ripoti katika eneo la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni mfano. Ukiangalia yale malengo yao waliyojipangia takriban kwa asilimia kubwa wameweza kuyatekeleza. Ukiangalia hata changamoto tumegundua ni changamoto ni moja tu ambayo kutokufikia lengo lake kuhamia katika ofisi mpya ambayo lile lipo nje ya uwezo wao, kwa sababu fedha zinatoka moja kwa moja serikalini kupitia Wizara ya Fedha. Lakini pamoja na hayo Mhe. Spika, baada ya hayo napenda kuwapongeza sana lakini nitaomba sana Mhe. Waziri hasa anayeshughulikia masuala ya Katiba na Sheria kwenye maeneo ya Mahakama na wale ma-*assessors* aje anipatie jawabu itakayoniridhisha pamoja na wale wananchi walionituma.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuweza kunistahamilia. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi kuchangia hoja ziliopo za ripoti za kamati ambazo ziliopo mbele yetu.
Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda na mimi niwashukuru mawaziri wote wawili kwa utendaji wao wa kazi na niwaombee Mwenyezi Mungu awajaalie wafanye kazi zao kwa ufanisi mkubwa

na uangalizi mkubwa na kwa ajili ya matakwa ya kuwaridhia wananchi wetu na kudra ya Mwenyezi Mungu na katika utendaji wao wa kazi.

Mhe. Spika, naomba kwanza nianze kwa Ofisi ya Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Spika, ni kweli kabisa kama mara nyingi sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi huwa tunalalamika kama palifanywa marekebisho ya mishahara lakini bado kuna matatizo ya baadhi ya watu wanalalamika. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri afanye utafiti mkubwa na kuangalia wale wa watumishi wa umma ambao bado mishahara yao haijakaa vizuri, afanye bidii ili mishahara yao ikae vizuri kuepuka yale malalamiko.

Jambo jengine jengine ambalo nataka nizungumze ni suala la ajira. Tunawapeleka watoto wetu kwenye masomo ya JKU lakini ajira bado zinapotolewa pamoja na kwamba vigezo vinavyotumika lakini kuna vigezo kama mambo ya vikosi na mambo mengine, hayo hasa ndio yanayohusu wale vijana tunaowapeleka JKU kwenda kusoma lakini cha kusikitisha ni kwamba wale vijana wanaopelekwa JKU sio wanaopata hizo nafasi zikija, wanachukuliwa watu nafasi nje ya watu ambao kuwa wamefanya kazi, hasa ukizingatia unapozikuja nafasi kama za vikosi na nini, nafasi nyengine zinachukuliwa na watu kutoka nje ya Zanzibar.

Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri aendelee kuwa na uadilifu mkubwa aone kuwa hizi nafasi za Wazanzibari basi ziende kwa Wazanzibari, na hasa ukizingatia kwamba hizi nafasi zinapokuja hizo taarifa zenyewe zinakuja kama za siri. Kwa hivyo ni bora hasa utawala bora unakuwa upo wazi, nafasi zikija zitangazwe ili kila mwenye haki yake aombe apate nafasi kulingana na uwezo wake. Lakini nafasi zenyewe zisitolewe zikawa zinatolewa kama kwa siri.

Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana nafasi hizi zinapokuja zitangazwe kila mmoja ajue kwamba sasa hivi kuna ajira, watu waombe kila mwenye nafasi yake apate kutokana na nafasi yake. Zitangazwe na sio zitolewe kwa siri.

Mhe.Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumza kwa Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Spika, Mwanasheria Mkuu ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tunashukuru sana katika utekelezaji wake lakini namuomba pia na yeye aangalie kama tupo tumo katika mchakato wa Katiba ya muungano. Yeye kama Mwanasheria Mkuu aangalie yale yanayohusu Zanzibar basi ayasimamie kwa nguvu zake zote ili kuwaridhisha wananchi wetu kuwepo huru na kufanya kazi yao yale ni matakwa yao waliomba. Namuomba sana Mhe. Katiba wa Sheria kwa kushirikikana na Mwanasheria Mkuu waone kama haki ya Wazanzibari imekwenda kwa Wazanzibari.

Suala jengine Mhe. Spika, ni suala la Wakfu na Mali Amana. Mhe. Spika, tunapiga kelele hapa kila siku tukija tunazungumza kama walimu wa madrassa waangaliwe. Sasa naomba hii wakfu na mali amana ipitie yale basi madrassa tu waziangalie, kuna madrassa yetu vijiji ambayo ni *dhalili bil huda* sana, wazione kama zinapendwa kusaidiwa zile madrassa ambazo ni dhalili sana na watu wake ni wanyonge vijijini. Lakini mimi kila siku huwa ninasema kama misaada inapokuja hawa wasimamizi wanasaidia sana mijini, jamani tuelekeenina vijijini, mijini mushajenga misikiti mingi mikubwa na madrassa nyingi, hebu elekezeni macho na kule vijijini muwasaidie wale wanyonge. Kwa sababu misikiti inajengwa kwa ajili ya kusaliwa, leo mijini imeshajaa misikiti imeshajaa bado munakuja huku huku kila anayekuja anajenga ghorofa

munapeleka mjini tu, huku vijijini kuna wananchi pia wana haki wapelekeeni na wao. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri aangalie haja ya kuelekeza macho vijijini kuwasaidia na wale wananchi wa vijijini.

Suala jengine Mhe. Spika, ninataka ninakalokuzungumza na Waziri ni suala la vizazi na vifo, ingawa wenzangu wameshalizungumza sana. Lakini Mhe. Spika, hivi sasa imefika wakati kuwa vyeti vya kuzaliwa ni wajibu kuwa navyo, kwa sababu bila ya vyeti vya kuzalisa utakosa haki zako za msingi zote na bahati mbaya mno zamani ilikuwa cheti cha kuzaliwa sio lazima. Lakini sasa hivi imefika wakati kuwa cheti cha kuzaliwa ni lazima kwa sababu huna cheti cha kuzaliwa hupati kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, hukopi, hukopeshwi, hutoi pesa, huweki pesa, husafiri. Kwa hivyo tuone kuwa hivi sasa imekuwa ni lazima.

Sasa Mhe. Waziri kila tukija tunapiga kelele tunakwambia wale wazee wetu ambao hawana vyeti vya kuzaliwa, serikali muwasaidie. Kuwasaidia kwake serikali tulimwambia Mhe. Waziri walioko Pemba kuwa kusafiri ni lazima waje zamani hapo Mambomsiige hapa Unguja kwa kufuatilia vyeti ni kazi kubwa, akatwambia Waziri kama tumewarahisishia kama vyeti vyote watachukua Pemba. Lakini Mhe. Spika, sivyo ilivyo bado watu wapo katika usumbufu havipatikani Pemba.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri anatwambia kwamba watendaji wake wanachukua vyeti wanasafiri wao wakaja huku, lakini sivyo hata watendaji walioko kule mawilayani tukiwaambia wanatwambia hapana, bado kuna usumbufu mkubwa. Kwa hivyo tunaomba muwapunguzie watu usumbufu.

Halafu suala jengine mzee cheti cha kukipata kwake basi ni zaidi ya shilingi arobaini elfu. Kwa hivyo maskini ya Mungu hana chakula cha kupika leo, cha asubuhi wala cha usiku. Kwa hivyo hawezi shilingi arobaini elfu akazipata kwa urahisi. Kwa hivyo shilingi arobaini elfu ni nyingi. Tunaomba serikali ione kama hiki kiwango ni kikubwa iwapunguzie watu ili wapate vyeti vya kuzaliwa, kwa sababu ni muhimu na ni lazima, kwa sasa hivi kwa cheti cha kuzaliwa ni lazima, huna cheti cha kuzaliwa husafiri, huweki pesa benki.

Kwa hivyo tunakuomba sana Mhe. Waziri ili serikali ione kwamba kuna haja kama ni marekebisho yarekebishwe ili wapate vyeti kwa urahisi sana. Kwa sababu nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwaondoshea wananchi wake usumbufu. Kama kuwaondoshea wananchi wake usumbufu basi ione kama hapa ni magumu iwafanyie nafuu wananchi wake ili wananchi wafaidike.

Mhe. Spika, naona unaniangalia nakushukuru sana naunga mkono hoja.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, ninapenda nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii ya kutoa mchango wangu mdogo katika ripoti hii ya Kamati ya Katiba na Sheria.

Vile vile napenda niishukuru kamati hii kwa kazi yao kubwa waliyoifanya pamoja na mawaziri hawa wawili, hatimaye imetuletea ufanisi mkubwa. Kwani maagizo waliyotoa mawaziri wameyatekeleza vile inavyotakiwa. Kwa hivyo nawashukuru sana na kuwapongeza.

Lakini nikianza na mchango wangu Mhe. Spika, nije katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kuna agizo hili la kuharakishwa kwa taratibu za kuanzishwa kwa mfuko wa bima ya afya Zanzibar. Hapa mimi Mhe. Spika, nataka nipate ufafanuzi zaidi kwa sababu hili ni jambo kubwa la afya na ni jambo la kitaifa. Kwani kama hukuugua wewe basi utauguliwa na hili litakapoanzishwa na kuleta mafanikio litapunguza mzigo mkubwa katika Wizara ya Afya kwa kupeleka wagonja nje ya nchi. Kwa hivyo Mhe. Waziri nataka aje anipe ufafanuzi ni watu gani watakaohusika na mfuko huu wa Bima ya afya tukiwemo wakulima, wafanyabiashara. Kwa hivyo naomba Mhe.Waziri anieleze maelezo mengine ya ziada.

Lakini jengine Mhe. Spika, kuna Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo kuwa kwa agizo la kamati ni kuwa Kamisheni iajiri watumishi wenye sifa zaidi na itoe elimu ya sheria ya utumishi wa umma. Mhe. Spika, hili ni kweli kabisa kuna baadhi ya watumishi wa umma hawana sifa au tuseme hawana taaluma zaidi, na kupitia hili Mhe. Spika, katika ziara zetu za kamati ofisi Kuu ya Pemba Wizara ya Fedha miongoni mwa changamoto zao moja ni kuwa wana wahasibu waliokuwa hawana sifa.

Na hiyo walieleza wenyewe, hatukuwauliza ni ndani ya ripoti yao. Sasa Mhe. Spika, kitengo kama hiki cha uhasibu, kama ni wizara au ni utumishi wa umma kuwaweka wahasibu waliokuwa hawana sifa, hii itakuwa haioneshi sifa nzuri. Hasa ukizingatia katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hivyo Mhe. Waziri hii ni changamoto ipo na wizara hii Ofisi Kuu Pemba ni moja ya changamoto yao. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba hili ulione na uliangalie kwa uangalifu.

Lakini jengine Mhe. Spika, kuna watumishi wanaostaafu. Mhe. Waziri ofisi yako inachukua muda mrefu kuwaajiri watumishi wengine. Hii vile vile tumelikuta katika Wizara ya Kilimo hasa wale wenye fani ya utaalamu na wamesema wenyewe kuwa wamepeleka barua zao, lakini mpaka leo hawajapatiwa jawabu. Kwa hivyo Mhe. Waziri ingawa Mhe. Jussa alisema kuwa Zanzibar ina wafanyakazi wengi lakini naomba wizara yako izingatie wale watu kuwaondoa na kuchukua muda mrefu, kwa sababu Wizara ya Kilimo ni wizara ambayo inategemewa na watu wengi ambao wanaotaka wapate taaluma za kilimo na hasa ukizingatia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetangaza mapinduzi ya kilimo.

Sasa kama kuna wataalamu waliokuwa wameshafikia umri wa kustaafu lakini hatimaye inachukua mrefu wataalamu wale hawajarudishwa pengine hiyo itakuwa ni tatizo. Mhe. Waziri ninakuomba na hilo ulione.

Lakini Mhe. Spika, nije katika Wizara ya Katiba, kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria. Mhe. Spika, hili siku zote husikia humu Barazani kuna wajumbe ambao tunadai tunapofanyiwa marekebisho ya miswada basi angalau tusiletewe ule mswada mzima, lakini kile kifungu ambacho kinafanyiwa marekebisho basi tuletewe kwa ukamilifu na hatimaye tupewe madhumuni na sababu ya kuwekwa kifungu chengine ili sisi wengine tupate uelewa zaidi.

Lakini la mwisho Mhe. Spika, kuna Kamisheni ya Wakfu na Mali Amana. Kama agizo lilivyotoka hapa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iendelee kuwafuatilia mali za watu ili kuepusha zima mbele ya Mwenyezi Mungu. Waziri na wao katika utekelezaji akasema kwamba kuwa juhudi zinafanywa kufuatilia madeni ya mali za watu, kuna mafanikio kiasi fulani.

Nakushukuru Mhe. Waziri kwa kufuatilia hilo lakini pia kuna mashamba ambayo yalikuwa na miti ndani yake, si kufuatilia tu na kupata mafanikio pengine ya kifedha lakini mashamba haya mengine kwa faida inayopatikana hapa basi mashamba haya yanahitaji yaendelezwe, kama yalikuwa na miti ile miti isiachiwe ikafa moja kwa moja lakini inahitaji badala ya kukodishwa mashamba yale basi iweze kushughulikiwa tena kwa kupandwa ile miche mengine na iwe na uimara zaidi.

Lakini naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie katika jimbo lile la Tumbe kuna shamba ngapi za watu, kwa sababu mimi ninajua kuna shamba moja lakini pengine kuna zaidi ya hiyo, naomba unipe ufafanuzi.

Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa na mimi nitachangia kwa muda mfupi sana kabisa.

Mhe. Spika, nianze na utawala bora. Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri anayehusika na mambo haya ya utawala bora kwa jitihada zake kubwa kwa wananchi na jinsi anavyotuonesha utumishi ulio makini na mahiri sana katika kututumikia. Hili ninampongeza sana.

Sasa Mhe. Spika, ili utawala bora usibu katika jamii lazima uteremke katika sehemu zote za utawala. Hivi tunavyozungumza ni kwamba Halmashauri zetu za wilaya takriban nyingi zimekosa kabisa suala zima la wanasheria, jambo ambalo huwezi kuwa na utawala bora ikiwa hii taaluma ya sheria haipatikani katika sehemu zote za nchi.

Sasa inaonekana katika serikali kuu tu ndio kuliko na wataalamu na wengi wa sheria. Sasa ni lini Halmashauri zetu za Wilaya hizi zitapata wataalamu katika mambo ya sheria. Hilo moja.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba suala zima la utumishi hivi sasa lipo chini ya wizara hii. Wakati hivi tunazungumza Mhe. Spika, ni kwamba Wizara ya Elimu ina matatizo ya walimu sana halikadhalika na wizara nyengine, ninatoa mfano kwa Wizara ya Elimu. Hivi juzi juzi tu tulipata habari kwamba Wizara ya Elimu imeshapeleka maombi ya kuajiri walimu zaidi ya elfu saba, yaani ni kipindi kirefu wamepeleka. Sasa ni jambo gani ambalo limefanywa mambo haya yakwame mpaka sasa hivi hawajatoa kibali cha kuwaajiri walimu hawa, kwa nini. Serikali haina fedha au kwa nini hawajatoa kibali, sio Wizara ya Elimu tu na wizara nyengine Mhe. Spika.

Jengine Mhe. Spika, nije katika suala hili agizo Nam. 1 kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi. Matatizo ya ardhi ni kwamba yameenea sana na *infact* kuna matatizo wakati mwengine Mhe. Waziri awe makini sana, kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana ya kutatua migogoro hii, asiviachie vyombo vyengine au ataviachia awe na uangalizi wa karibu mno, yeye mwenyewe au watendaji wake katika kuona dhamana ya matatizo ya ardhi.

Hivi sasa Mhe. Waziri kama huna habari kuna matatizo ya ardhi kipande cha ardhi kinawaniwa pale Chake-Chake baina ya Msikiti wa Istiqama pamoja na hawa watu Mtoni pale. Watu

wametiana ngumi. Mhe. Spika, ninataka aone lile ni tatizo mno sana, askari ilibidi wakae na silaha pale, watu wana kesi Mahakama.

Ninasikia baada ya kushiriki wewe kenda kushiriki na Waziri wa Katiba na Sheria na tume gani kwenda kusababisha mzozo zaidi. Hili analijua Mhe. Spika, na kama analijua atatua lini kwa sababu watu wataendelea kuchapana kule, wataendelea kuhasimiana, huo utawala bora utaendelea kuwa haupatikani. Naomba suala la tatizo la ardhi baina ya Istiqama kule na Msikiti wa Mtoni utie mkono wako ili nusura ipatikane Mhe. Spika, pale.

Jengine Mhe. Spika, twende katika suala zima la ajira, naona nimezungumzia basi nakwenda kwenye Katiba sasa huku. Mhe. Spika, kwenye Wizara ya Katiba na Sheria kwenye kitengo hiki cha Wakfu na Mali ya Amana kuna hizi nafasi za Hijja. Nafasi hizi husikia zinaletwa serikalini watu kwenda Hijja na kwa kweli nafasi hizi Mhe. Spika, huko vijijini tunazisikia tu, zipo kweli hizi nafasi na kama kweli zipo wanaotakiwa waende Makka kuhiji si mawaziri, makatibu wakuu, wawakilishi ni wale wakulima na wafanyakazi nao wanatakiwa wazipate hizi nafasi waende.

Sasa ni utaratibu gani Mhe. Spika, unatumika katika hili. La ikiwa anazitoa juu huu si utawala bora na huku chini ni lazima uzitoe kusudi nao waende Makka wakahiji kwa sababu hizi nafasi zimeletwa serikalini, pesa za walipa kodi hawa kama ukitoa kwa wakubwa tu hiyo ni bias na utawala bora utakuwa haupo hapo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kuna suala la dhamana. Kuna kitu kinaitwa *bail* katika mambo ya sheria kwa sababu naona Mhe. Jussa kageuka, mimi si mwana sheria, mimi ninatokea *teaching professionalism* tena katika mambo ya elimu ya viumbe. Lakini nataka nizungumzie *bail*.

Mhe. Spika, nafuatilia kabisa mchango wako kwa sababu na wewe ni *lawyer*. Nataka munifuatilie sana kwa sababu mimi hii sio fani yangu ya sheria. Mhe. Spika, dhamana kwa mujibu wa tunavyosikia ni haki ya mtuhumiwa. Katika nchi hii Mhe. Spika, kuna mambo mengi ambayo husababisha kesi nyingi, tena sio hivi sasa tu, tangu zamani nadhani hata na baadae, ikiwa mambo hayakurekebishwa basi itakuwa hivyo hivyo kwamba *bail* katika nchi hii ni tatizo.

Sasa nataka Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria aje atoe ufafanuzi ni sababu gani mshtakiwa anakaa pale pengine miaka 2 unaambiwa uchunguzi haujakamilika na wala dhamana hapewi. Siku nyengine unajikuta unakaa unafunguliwa kwa kesi hii, keshokutwa unapelekwa unaambiwa kwa kosa jengine. Katika miaka zaidi ya 20 iliyopita, mimi nilikosa dhamana. Nilikuja kukamatwa nyumbani kwangu, nakumbuka kama leo ni zaidi ya miaka 20 iliyopita, nikapekuliwa na kuonekana na zile *Bismillah* za rangi ya kijani, nikaambiwa kwamba nahatarisha amani, lakini nikakosa dhamana.

Mhe. Spika, nilikuwa nimeoa siku ya Alhamis, Ijumaa nikakamatwa, sasa nikakoseshwa dhamana kwa kuhatarisha amani ya nchi. Nilikaa karibu mwezi kule, hata napelekwa mahakamani baada ya wiki 4 naambiwa kosa la uzembe na uzururaji. Huku nahatarisha amani ya nchi, halafu siku nyengine naambiwa uzembe na uzururaji. Niliporudi nyumbani kule hina imeshafutika, almuradi harusi si harusi tena mimi. Yaani ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Ilikuwa nipewe dhamana nikakae na mke wangu, lakini leo nakamatwa nawekwa ndani miezi miwili sipewi dhamana, nabadilishiwa shauri naambiwa ni uzembe na uzururaji. Nilikuja

kukamatwa ndani nikiwa harusi, nimezururа lini na nimefanya uzembe lini. Hivi kuoa ni uzembe, sasa nataka Waziri wa Katiba na Sheria katika hili muwe makini sana, utawala bora hautapatikana katika nchi Mhe. Spika, naomba mujitahidi sana, kwa sababu sisi ni miongoni mwa dunia na nchi zote zinafuata Katiba, sheria na utawala bora.

Zanzibar dhamana mutoe, itungwe sheria hasa. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria naomba ugeuke unitizame. Mhe. Spika, aniangalie kwa sababu itungwe sheria, ikiwa serikali wameshindwa kufanya uchunguzi na uwekwe muda wa kufanya uchunguzi, ukipita muda huo basi hakimu wa mahakama imtoe huyo mtu impe dhamana, kwa sababu wanaweza kumuweka ndani, halafu ikawa uchunguzi haujakamilika, huku yeye anateketea na wanawe wanateketea kwa njaa. Haya jamani ndio utawala bora huo.

Sasa Mhe. Spika, nimalizie tu kwa jambo moja dogo. Hivi sasa kuna mchakato wa Katiba na umo kwenye rasimu. Kamati imeshapita kuchukua maoni, mabaraza ya wilaya yanakuja. Wewe bwana ndio mwenye dhamana ya Katiba na Sheria katika nchi, ofisi yako inashirikishwaje ili kuona kwamba hayo maelezo hayababaishwi, hayo maoni waliyotoa wananchi ndio, unashirikishwa au wanayafanya tu hivi hivi hawawashirikishi nyie. Kama hawawashirikishi hivyo ndivyo.

Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru.

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor tunakushukuru. Nafikiri Mwenyekiti wa Kamati amesikia, Mawaziri wamesikia, maana umetoa sauti kubwa kweli kweli hapa. Nilikwisha kutamka kwamba huyu ni mchangiaji wa mwisho ili tupate muda wa kufanya majumuisho. Nimuombe Mhe. Hassan Hamad Omar ambaye punde tu ameniomba, nakuomba radhi. Hivi sasa twende kwenye majumuisho tumalize kazi hii na jioni tuingie sehemu nyengine. Nimkaribishe basi Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, napenda kwanza nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuleta majumuisho, katika mjadala wetu ambao ulikuwepo tokea juzi.

Mhe. Spika, pia napenda niwashukuru Wajumbe kwa michango yao mizuri ambayo naamini itasaidia sana katika kuzidisha utendaji wa wafanyakazi wetu katika wizara zetu.

Mhe. Spika, wachangiaji ambao walizungumza katika wizara zetu ni 11, lakini kwa Wizara yangu ni 9 nao ni;

1. Mhe Ismail Jussa Ladhu
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Omar Ali Shehe
4. Mhe. Hija Hassan Hija
5. Mhe. Mohamed Haji Khalid
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Subeit Khamis Faki
8. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
9. Mhe. Saleh Nassor Juma

Mhe. Spika, mazungumzo yote yaliyozungumzwa, nafikiri ni mambo matano ambayo yamezungumziwa. Kwanza ni suala la rushwa mahakamani, likazungumziwa suala la mahakama ya ardhi, mrajis wa vizazi na vifo, pamoja na vyeti vya ndoa na talaka na vyeti vya kuzaliwa hasa. Lakini pia liligusiwa suala la vitambulisho vya Mzanzibari.

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumziwa ni kuhusu wafanyakazi wa mahakama hasa mahakama ya mwanzo, pamoja na kuwa-*assessors* wale ambao wanatakiwa wapewe chochote kile wanachofikia.

Suala jengine Mhe. Spika, ambalo liliulizwa ni kuhusu *work force* ya mahakamani. Mhe. Spika, haya ndio majadiliano makubwa ambayo yalizungumzwa katika Wizara yangu.

Mhe. Spika, kwa kuanzia labda niseme tu kwamba ni kweli katika afisi yangu au katika Wizara yangu sikatai rushwa ipo mahakamani. Hili ni tatizo ambalo tunalipata sana. Kuna baadhi ya mahakimu wetu na baadhi ya watendaji wetu bado hawajawa watu waaminifu. Hili Mhe. Spika, tunalikubali na tunaendelea kulipiga vita.

Hata leo asubuhi nyumbani kwangu kaja mtu kwa bahati nzuri simjui, kanijia kwa matatizo haya haya kwamba ana kesi yake siku nyingi na kuna mambo chungu nzima kanielezea. Mimi nikawasiliana asubuhi hiyo hiyo na DPP katika matatizo haya haya. Kwa hivyo, suala hili tunalo na tunalifuatilia kwa hali ya juu kabisa. Wale ambao tunawajua, basi hatua tunachukua.

Isipokuwa Mhe. Spika, naomba sana kwa sababu mtu atakuja atakuambia kwamba nafikiria kuna rushwa kwa fulani, sasa ukimwambia nipe ushahidi au nipe maelezo zaidi yeye hataki. Sasa hapo anatuweka pabaya kidogo. Hebu tusaidieni katika kutupa ule ushahidi ambao sisi utatufikisha katika kuchukua hatua za mwisho. Lakini ukiniambia tu, halafu yale mambo mengine huniambii, kwa kweli hujafanya kitu, utakuwa na wewe pia unasaidia kuendeleza hiyo rushwa. Lakini naomba sana tushirikiane, tupeane taarifa hizi ili tuweze kuchukua hatua zinazohusika.

Mhe. Spika, rushwa ziko kwenye mahakama zote, mahakama ya ardhi, mahakama hizi za kawaida. Lakini hapa kwenye mahakama ya ardhi tuna matatizo matatu. La kwanza kesi ni nyingi na mahakimu ni kidogo. Mwanzo tulikuwa na hakimu mmoja Unguja na mmoja Pemba, kutokana na kesi nyingi tukaongeza hakimu mwengine Unguja na mwengine Pemba, kwa hivyo tuna mahakimu wanne wa mahakama ya ardhi, lakini bado kesi ni nyingi. Kesi ni nyingi kwa sababu hatujachanganua, kwa sababu kitu kikitajwa ardhi tu basi kila kitu kinakwenda mahakama ya ardhi na wakati mwengine ni suala la miradhi ambalo linazungumzia mambo ya shamba na mengineyo. Kwa hivyo, kesi zote zinakwenda kule inakuwa ni matatizo. Tunajaribu kufanya hivyo kuwaelimisha watu kwamba ni lazima tutenganishe.

Kwa mfano warathi wanagombeana mirathi inayohusiana na shamba, basi itakwenda huko kwenye mahakama ya ardhi, wakati sio ile ni mirathi na iende katika mahakama ya kazi. Kwa hivyo tunayo matatizo hayo na pia tunajaribu kuyatatua ni mengi, lakini *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Lakini pale ambapo mahakama imetoa maamuzi, kama alivyosema Mhe. Hija Hassan. Mahakama imetoa maamuzi, matatizo ya watu wengine ni kwamba mahakama ikishasema, kwa

hivyo pale pale ni lazima apewe na ninazo. Kesi moja ni kutoka Kiwani ambako Mhe. Hija Hassan ametoa mfano, amenijia mtu mimi, amesema mahakama ya ardhi imeshatoa maamuzi haya. Kwa hivyo, lazima nipewe haki yangu. Kwa bahati nzuri walikuwa wameshakuja watu kulalamika, kwamba mahakama ya ardhi imesema hivi na sisi tuna matatizo haya. Mimi nikawaambia kateni *appeal* ndio utaratibu. Kwa hivyo, yule ambaye amepata hukumu anataka pale pale itekelezwe, tunatakiwa tujue kwamba mahakamani kuna utaratibu wake.

Mfano, unakwenda kwenye mahakama ya mwanzo, kama hukuridhika au yule mwengine hakuridhika, basi anapewa ruhusa akate *appeal*, hakuridhika anakwenda mahakama nyengine. Kwa hivyo, huu ni mdorongo mpaka kufika mahakama ya mwisho. Sasa watu hawataki, mtu akipewa hukumu anataka pale pale atekeleze hukumu hiyo, haiwezekani ni lazima tufuate utaratibu. Kwa hivyo, hayo nayo ni mambo ambayo ni lazima wananchi wetu wajue kwamba mahakama haiwezi kuwa ikishatoa hukumu leo, halafu wewe ukapewa hukumu wakati mwengine bado hajaridhika, kuna utaratibu wake lazima tuufuate.

Mhe. Spika, suala la mahakama vile vile lilizungumzwa katika suala la *assessors* na mahakimu wa mwanzo. Ni kweli tatizo la *assessors* fedha zao nyingi zilikuwa hazijalipwa, lakini nashukuru kusema kwamba hivi sasa takriban kwa asilimia kubwa tumeshalipa. Hayo ni matatizo yetu tunayajua sote, fedha tunazopata hazitoshi kwa kufanya kila kitu. Kwa sababu ukisema uwalipe *assessors* fedha zile, uwape wale *assessors* waliopita wa nyuma. Kuna *assessors* ambao hivi sasa tunawaita katika mahakama na wao ni lazima uwape. Kwa hivyo, tunachofanya tunapunguza huku na hawa sasa huwa hawadai tena, tunawatoa huku, lakini huku tunapunguza pengo kidogo kidogo. Ni kweli bado hawajamalizika, lakini kila tukipata fedha tunawapunguza na ninaamini kwamba katika kipindi hiki kifupi kinachofuata, fedha zao wale ambao wanadai zitakamilika. Lakini kuanzia hapo tutakuwa hatuna tena deni ambalo *assessors* watakuwa wanatudai, kwa sababu wao wakija hivi sasa tunawalipa fedha zao. Kwa hivyo nakubali kwamba deni hili lipo kidogo na tutajitahidi, lakini naamini kwamba sehemu kubwa tumeshalipa, ingawa wengine bado wapo.

Mhe. Spika, kuhusu mahakimu. Ni kweli Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan hapa alizungumzia sana katika kikao kilichopita cha bajeti, kuhusu mahakimu wa mahakama ya mwanzo. Hii inatokana na mishahara yao, mshahara wa hakimu wa mwanzo na mshahara wa hakimu wa wilaya, tofauti ni kubwa. Tofauti imekuwa ni kubwa kwa sababu kuanzia DM hakimu wa wilaya, pale lazima awe na Digirii, lakini hakimu wa mwanzo yeye ana cheti tu, ambacho katika hiyo *competition* ni kuwa kile cheti ni tofauti sana na vile vya Digirii. Lakini tukaona kilio cha Wawakilishi na hasa cha Mhe. Hamza Hassan, na nikaahidi kuifanyia kazi na tulifanyia kazi. Tulichofanya ni kwamba hata Mhe. Rais na yeye akaelekeza na tukafanyia hiyo kazi. Ni kwamba huwezi hivi sasa hakimu wa wilaya ambaye ana cheti ukampandisha kwa kiwango kile ambacho kimo katika ile *competition* ya Utumishi. Kwa sababu cheti hana yeye hakimu wa wilaya tu, hata mtu mwengine wa utumishi ana cheti na wa sehemu nyengine ana cheti.

Kwa hivyo, tukitizama vile viwango vya vyeti ni tofauti, lakini nikasema kwa sababu wanafanya kazi kubwa, hebu tuwatafutieni njia nyengine. Tukawapandishia maposho yao kwa kiwango kikubwa na hivi sasa mshahara wao ule wanaoupata pamoja na maposho ni mzuri kwa kiwango chao. Lakini binadamu hatosheki. Juu ya hivyo mimi binafsi nikawaita ofisini kwangu mahakimu wote, lakini waliokuja ni Wawakilishi wao wengi tu. Tukakubaliana vizuri na

tukawaambia njia tulizopita mpaka tukafikia maposho yale ambayo hivi sasa wanapewa. Tukawauliza je, mmekubaliana na sisi wakasema tumekubaliana. Lakini tukawaambia hii isiwanyime nyinyi kufanya mpango mkasoma ili kupandisha kiwango chenu, kwa sababu ukizidisha kiwango cha elimu ndio pale mshahara wako unazidi kupanda na wao wakakubali. Lakini zaidi yote haya tume- *take consideration* kwenye suala zima la *scheme of service*.

Mhe. Spika, sasa *scheme of service* ambayo tumeshapeleka utumishi hivi sasa, imeyazingatia yote hayo na tulichofanya ni kwamba hawa mahakimu wa mwanzo sisi hatukutizama kama ni cheti, digrii au nyengine. Tumesema kutakuwa na hakimu wa mwanzo, hakimu wa wilaya hakimu wa mkoa na Jaji. Sasa *scheme of service*, kwanza tunachotaka ni kwamba hakimu wa mwanzo ni lazima awe na digrii ya sheria na tunao wengi tu.

Kwa hivyo, ukishakuwa na digrii ukitoka hakimu wa mwanzo kwenda hakimu wa wilaya, pale pana *interval* ya kiasi miaka mitatu. Kwa hivyo, ukitoka pale itakuwa ni *automatic* kwenda hakimu wa wilaya, lakini *automatic* hiyo tusije tukaona kwamba unakula rushwa hatukupandishi kuwa hakimu wa wilaya, usije ukafanya mambo mengine kinyume na maadili ya hakimu hatukupandishi. Lakini ukiwa ni hakimu mzuri, unafanya maadili yako vizuri na huna matatizo, basi tutakupandisha kwenda hakimu wa wilaya. Kwa hivyo, itakuwa ni miaka mitatu hapo. Kutoka hakimu wa wilaya kwenda hakimu wa mkoa miaka mingine mitatu, kutoka hakimu wa mkoa kwenda Jaji miaka mingine mitatu ni *automatic* lakini kwa masharti kwamba huli rushwa, huna matatizo na *ethics* zako ni nzuri. Kwa hivyo, utaona kutoka hakimu wa mwanzo mpaka kuwa Jaji ni karibu miaka minane au tisa. Hii kwenye Katiba utaona mtu hawezi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu mpaka awe na digrii na awe ameshatumikia angalau miaka saba. Kwa hivyo, utaona inakwenda vizuri, sasa hii ndio *scheme of service* ambayo tumefanya na hiyo mishahara yao itakuwa inapishana kwa ngazi kama hizo.

Kwa hivyo, Mhe. Hamza hivyo ndivyo tulivyofanya kwa makubaliano na mahakimu wote na wao kwa kipindi hiki tumejaribu kuwapa maposho mazuri, angalau kuwasaidia katika hali hii ambayo wapo.

Mhe. Spika, kuhusu vitambulisho na vyeti vya kuzaliwa. Ni kweli Mhe. Spika, nimepata matatizo ya watu wa vitambulisho wa Wilaya ya Chake Chake. Watu wanaotoa vitambulisho wa Wilaya ya Chake Chake, wanatukorofisha kidogo.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nayakusanya maelezo hayo ili nimuandikie rasmi Waziri pamoja na Mkurugenzi wao. Kwa sababu alikwenda, na kwa bahati nzuri aliyekwenda ni Mhe. Mwakilishi katika Baraza lako. Alikuwa na cheti cha mtoto wake wa kumzaa, vyeti viwili viliharibika akavileta ofisini kwetu vikatengenezwa vizuri. Sasa vyeti vile alipokwenda kutaka kutolewa vitambulisho, watu wa vitambulisho wakasema hivi ni vyeti *fake*. Yeye akasema vyeti hivi nimechukua Mambo Msige. Akaambiwa ndio, lakini ni *fake*.

Mhe. Mwakilishi mwenyewe akanipigia simu mimi na akavituma kwa ndege akampa mtu akaniletea. Mimi nilipovipata, nikavitizama na utaalamu wangu huo mdogo nikaona kama sio *fake.* Lakini nikampa Mrajis wa Vizazi na Vifo, nikamwambia hebu vicheki hivi vyeti. Wakacheki kwenye daftari vipo, namba ni sawa sawa na kila kitu ni sawa. Akaniambia vyeti hivi sio *fake*, tukamrejeshea tukamwambia sio *fake* nenda ukawaambie wakupe vitambulisho. Mhe.

Spika, alikwenda na wakasisitiza kwamba vyeti hivi ni *fake* na hatutoi labda tukupige tu kwa sababu wapo Waheshimiwa.

Kwa hivyo, mimi aliniambia na nikamwambia usikubali, kwa sababu tumeshawaambia wao wana *authority* gani ya kusema kwamba vyeti hivi ni *fake* au si *fake* na Ofisi inayohusika na vyeti ni Wizara ipo na imeshasema. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hawa wanayo matatizo yao binafsi na watu hawa hatutakubaliana kabisa na mimi nitaandika barua rasmi kwamba wachukuliwe hatua kwa sababu wanatufanyia mambo ambayo siyo. *(Makofi)*

Kwa kweli tulikuwa tumeshafika pahala pazuri na nilikwenda na Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba na tukakubaliana kila kitu, sasa hawa wanarudisha nyuma kwa nini atufanyie hivyo, mimi niliwaambia kwamba hivi si *fake*, basi hata hawaheshimu na mimi Waziri nimeshasema si *fake* na wao wana-*authority* gani. Kwa hivyo, hayo yanatokea lakini kwa baadhi na wafanyakazi hawa wanaotuharibia ndio wa kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hiyo ni kweli ilitokea na ninamuomba radhi sana Mhe. Mwakilishi kwa hayo yaliyotokea kwa usumbufu huo. Lakini tutachukua hatua na tutahakikisha kuwa kitambulisho cha mtoto wake anapatiwa na nafikiri ameshapatiwa.

Sasa hayo, Mhe. Spika ndio mambo ambayo kwa kweli yana matatizo katika suala hili.

Lakini suala la vyeti vya kuzaliwa naomba nisikubaliane na Mhe. Mwakilishi aliyesema kwamba sasa watu bado wanasumbuliwa. Mhe. Spika, sifikirii isipokuwa upo usumbufu mdogo mdogo, lakini si mkubwa sana. Kwa kweli tulivyofanya hasa kwa watu kutoka Pemba walikuwa zamani wanakuja huku Unguja na sisi tukazuia na tukasema kwamba mfanyakazi wetu ambaye yuko Wete ndiye mwenye kujaza zile fomu za *birth registration*.

Kwa hivyo, akishakuzijaza zile fomu za *birth registration* anaziangalia yeye kama ni sawa au si sawa na halafu yeye au mtu wake anazileta Unguja yule mzee au mtu ambaye aliyeomba yeye yuko Pemba anaambiwa asubiri na zinaletwa Unguja na kuangaliwa katika fomu hamsini kwa mfano zilizoletwa, 40 zinaweza kuwa hazina matatizo na vyeti vikatengenezwa pale pale na halafu vikapelekwa Pemba ndivyo tunavyofanya.

Sasa kama 10 zina matatizo basi Mrajis wetu wa Vizazi na Vifo au Msaidizi wake anakwenda Pemba kuwa-*interview* wale watu na wala hawaji huku kwa sababu hiyo ya kuwapunguzia mzigo wananchi wetu.

Kwa hiyo, huo ndio utaratibu uliopo hivi sasa na ndio ambao unaendelea sasa, isipokuwa kama kuna hitilafu nyengine ndogo ndogo basi tunaomba sana mutuambie, ili tuweze kuzirekebisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu naye alizungumza kuhusu suala la Maoni ya Katiba na akataka mimi niseme chochote kama Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Spika, mimi namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambaye yeye alizungumza kwa kirefu na kusema

kwamba maoni ya wananchi yataheshimiwa na mimi naunga mkono kwamba maoni ya wananchi ndiyo yatakayoheshimiwa.

Lakini tujue tu kwamba hivi sasa bado mchakato uko katika hatua ya pili kwenye Mabaraza ya Katiba yanakuja ambapo watu watapewa nafasi tena ya kuzungumza na kutoa maoni yao.

Finally hayo watakayokubaliana wananchi bila shaka kama ilivyosema serikali ni kwamba maoni hayo ndiyo yatakayoheshimiwa. Mhe. Spika, zaidi kama alivyotaka *statement* ya serikali mimi ni *opposition* siwezi kutoa *statement* ya serikali na mwenye kuweza kutoa *statement* ya serikali ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambaye yeye ndiye Kiongozi wa Serikali katika Baraza.

Sasa ninachoweza kusema ni kwamba sisi kama ni serikali tunaweza tukaheshimu maoni wa wananchi, ambayo hayo ndiyo tunayoyazungumza kila siku.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk namshukuru alizungumza sana katika maposho haya ya majaji, ambayo tayari nimeshayazungumza, pia alizungumzia suala la *assessors*.

Mhe. Omar Ali Shehe alizungumzia suala la rushwa na kama nilivyosema kwamba nakubali kuwa rushwa ipo, lakini tunajitahidi kuipiga vita. Mhe. Spika, nawaomba sana wananchi kwamba wanapopata ushahidi wasiopoge, maana yake watu wanaona kama wakitupa wao wataji-*expose*, sasa kama hamtwambii ule ushahidi hasa sisi hatuwezi kuchukua hatua, tutakubali lakini hatua haifiki mwisho. Kwa hivyo, ni vyema tushirikiane katika masula haya tupeni ushahidi na tutachukua hatua kama ambavyo tumechukua hatua kwa baadhi ya wengine.

Mhe. Hija Hassan Hija naye alizungumza kuhusu Mahakama ya Ardhi na mimi kama nilivyosema kwamba ni kweli Mahakama ya Ardhi inaweza kutoa maamuzi, lakini ile si *final* kama kuna mtu ambaye hakuridhika kuna mdai na mdaiwa, basi kama mdai hakuridhika basi anayo haki ya kukata *appeal*. Kwa hivyo, usione kwamba Mahakama ya Ardhi imetoa maamuzi na ukafikiria kwamba maamuzi yale ndio ya mwisho, lazima tumpe mtu nafasi ya kukata rufaa.

Mhe. Mohammed Haji Khalid yeye aliuliza swali moja na kusema je hizi mahakama zinazofunguliwa kama vile Mahakama za Biashara, Mahakama ya Watoto, Mahakama ya Ardhi, Mahakama ya. Mwanzo, *District Magistrate*, *Resident Magistrate* na Mahakama Kuu je tunao mahakimu wa kutosha mbona tunafungua tu.

Mhe. Spika, mahakimu wapo ingawa hawatoshi sana, lakini nafurahi kusema kwamba Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora imetupa nafasi 35 za kujaza katika mahakama. Kwa hivyo, nafasi hizo hivi sasa zimeshatangazwa na tutaajiri Mahakimu hao pamoja na wafanyakazi wengine wa mahakama, ili mahakama zetu ziweze kufanya kazi zake vizuri.

Kwa hiyo hatuna tatizo sana na watumishi katika mahakama ingawa upungufu upo kidogo kwa hivi sasa, lakini *Inshaallah* tukimaliza hii ajira ya nafasi 35 nafikiri tunaweza tukafika pahala pazuri.

Mhe. Hamza Hassan Juma nafikiri nimeshamjibu kuhusu *assessors* na Mahakimu wa mwanzo.

Mhe. Subeit Khamis Faki kuhusu mchakato wa Katiba nafikiri nimeshamjibu. Vile vile alisema hii misikiti na madrasa kwa nini inajengwa huku mjini tu kwa nini shamba haijengwi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba misikiti na madrasa kweli Kamisheni ya Wafku pamoja na Ofisi ya Mufti inashughulikia, lakini sisi sio tunaojenga ni mtu mwenyewe tu kama Mhe. Ismail Jussa Ladhu anazo fedha nyingi alizorithi basi atasema mimi nataka kujenga msikiti pahala kadha.

Sasa sisi hatuwezi kumlazimisha kumwambia asijenge hapo na ukajenge pahala pengine na hivyo ndivyo inavyokuja na sisi tuna-*facilitate* tu kwa ajili ya kutafuta kama alivyosema hapo tutafutie kiwanja pahala pale na mambo mengine na kwa sababu ni jambo la kheri tunafanya, lakini wakati mwengine hata kiwanja anatafuta mtu mwenyewe.

Kwa hivyo, ndio maana utaona misikiti hatuna *control* nayo ya kujengwa, isipokuwa ile inayokuja kwetu sisi hiyo tutatafuta. Kwa mfano, tukipata mfadhili ambaye atasema nawapeni kwa ajili ya kujenga misikiti, basi tutatafuta mwahala ambamo misikiti ama ni kidogo au si mizuri sana na hiyo tunaweza tukafanya. Lakini watu wengi wanaokuja wafadhili hawa ni binafsi kwa hiyo hatuwezi kuwa-*control* wapi mfanye au hapa msifanye ama wapi wajenge madrasa na wapi pasijengwe.

Mhe. Spika, tunaweza kumshauri kama mnataka kujenga hapa basi si bora pale, lakini kama yeye mwenyewe anayo hamu ya kujenga pale basi hatuna njia, isipokuwa hatuwezi kumwambia basi usijenge hapo kwa sababu nalo ni jambo la kheri acha lifanywe na ndivyo inavyokuwa.

Vile vile kuhusu nafasi za Hijja. Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba ofisi au wizara yangu haijapata nafasi za kwenda Hijja zinazotolewa kwa msaada, yaani si wizara au Kamisheni ya Wakfu na wala Ofisi ya Mufti, isipokuwa pale ambapo tutapata nafasi hizo basi bila ya shaka lazima tukae na tutizame na tujadili na zitagaiwa namna gani. Lakini tokea nimekuwepo mimi Wizarani pale mpaka hii leo nafasi hizi bado hazijaja.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad alizungumzia kuhusu Tume ya Kurekebisha Sheria na katika uandishi. Mhe. Spika, napenda niseme tu kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria inayo shughuli nyengine, hii inatizama zile sheria ambazo pengine ni za zamani au zina matatizo na utaratibu wake ni mwengine kabisa.

Kwa hivyo, sheria zinazorekebishwa za kawaida hizi zinahusiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na wizara inayohusika. Mhe. Spika, mapendekezo yake nimeyasikia na tutayafanyia kazi na tutafanya hivyo pale ambapo inawezekana.

Pia alizungumzia kuhusu habari za Wakfu. Kwa kweli sitoweza kumwambia hivi sasa kwamba Tumbe kuna mashamba mangapi ya Wakfu. Kwa hiyo, ni vyema nitizame na nitawauliza wenzangu na tutakujibu tukijaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma naye alizungumzia matatizo ya maji kwenye Msikiti wa Istiqama na Mtoni. Mhe. Spika, nafikiri suala hili tumeshalimaliza, kwa sababu kulikuwa na matatizo mengi

baina ya Istiqama na watu wa Mtoni na Mhe. Mwakilishi wa Chakechake ni shahidi na watu wa Mtoni hawahusiki kabisa katika sehemu hii ya Istiqama kwa nyaraka hizo za mwaka 1932 kama hivi na nyaraka hizo tumeziona *Archive* na watu wa Mtoni hawakufika kabisa huku, hivyo watu wa Mtoni hawahusiki.

Kwa kweli suala hili nadhani tumeshalimaliza na wala si vizuri tena kulitaja mara kwa mara na kuwaachia watu, isipokuwa kama kuna matatizo ya maji na mambo mengine, basi vyombo vinavyohusika hivyo vya kushauriwa au kupeleka malalamiko hayo, kwa ajili ya kuweza kuyatatua.

Suala la dhamana, kweli dhamana kwa mujibu wa Katiba ni haki ya mtuhumiwa, lakini ina-*exceptions* zake. Kwa mfano, ikiwa mtuhumiwa tunahisi kwamba atakimbia lile kosa alilofanya tukimtoa nje atakimbia au ikiwa yule aliyetuhumiwa ni kwamba tukimuacha nje fujo linaweza kuzidi ama kutatokea matatizo yoyote, kwa hiyo pale kisheria huwezi kutoa dhamana.

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali dereva anaweza kumgonga mtoto gari akamuua. Sasa kama hujamtia ndani yule, wazee wa mtoto wanaweza kuchukua hatua. Kwa hivyo, ni faida yake yeye kumuweka ndani kuliko kumtoa nje. Kutokana na hali hiyo, ndio tunasema kwamba dhamana inategemea, lakini tunaweza kusema kwamba dhamana ni haki ya mtuhumiwa, lakini kuna *exception*s na halafu kuna kesi nyengine ambazo huwezi kupewa dhamana.

Kwa mfano, kesi ya kuua au kutaka kupindua basi kesi kama hizi huwezi kupewa dhamana na hiyo ni sheria ambayo imesema. Vile vile kuna kesi nyengine ambazo Mkurugenzi wa Mashtaka anaweza kusema kwa hali ilivyo na kwa hali ya nchi ilivyo basi dhamana nazuia.

Lakini kwa zile kesi za kawaida dhamana unapewa na uchunguzi unaendelea na upo utaratibu wake ikifika kipindi fulani kama hakuna uchunguzi au hakuna chochote kilichofanyika basi mtuhumiwa yule anaachiliwa chini ya kifungu fulani ambapo kama baadaye utatokea ushahidi na uchunguzi mwengine unaweza kukamatwa tena.

Kwa hivyo, huo ndio utaratibu wa dhamana kwa maana hiyo mtu anaweza kukamatwa wakati wowote ule hata kama ameoa juzi basi leo atakamatwa na kama tunaona kwamba akitolewa ataleta fujo basi tunaweza kumuweka bila ya kujali kuwa hina inaweza ikatoka au haitoki. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuja kutoa ufafanuzi wa michango ya Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia katika masuala yaliyojitokeza katika Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kupitia Mwenyekiti wao Mhe. Ali Abdalla Ali, ambaye kwa juzi aliwakilishwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa yale

majukumu ambayo wameyafanya katika ufuatiaji na utendaji wa wizara yetu katika kipindi hichi cha mwaka 2012/2013. *(Makofi)*

Niwashukuru sana kwa mashirikiano yao na umahiri wao ambao wameonesha katika kufanya kazi zao na hatimaye wakaweza kuwasilisha ripoti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda niwaahidi kwamba kwa mujibu wa utaratibu wetu tuliojiwekea yale yote ambayo wameyaeleza kama ni maoni au ni maagizo, basi tutayachukulia hatua na kuyafuatilia na tutaleta taarifa kama tulivyoleta taarifa ya safari hii katika mwaka ujao kipindi kama hichi, ili kuonesha kwamba Baraza hili nalo linapewa haki yake katika kuishauri, kuikosoa pamoja na kuiagiza serikali.

Kwa hiyo, naahidi kwamba mengi yalikuwa ni maagizo pamoja na maoni na kwa utaratibu wetu wa sasa hayo naomba niyawasilishe katika kipindi hicho kwa ajili ya kuokoa muda.

Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa uwasilishaji wake kwa mara ya kwanza amemuwakilisha Mwenyekiti wa Kamati na ameonekana umahiri wake. *(Makofi)*

Katika ripoti ile kulikuwa na suala linalohusu kushauri Wizara zote za serikali kutumia na kuwa na Vitengo vile vya *ICT*. Mhe. Spika, napenda niliarifu Baraza letu tukufu kwamba wizara yangu tayari imeshatoa muongozo kwa wizara zote au taasisi zote za umma kwamba ni lazima waanzishe hivi vitengo na utaratibu wa kuviendesha hivi vitengo uwe vipi na muongozo tayari umeshatolewa.

Lakini kama Waheshimiwa Wajumbe wengine walivyosema kwamba kazi yangu sasa itakuwa ni kufuatilia ni nani ambaye ameshaanzisha hivyo vitengo na utekelezaji wake unakwenda vipi, ili kukamilisha ile dhana nzima tuliyoisema hapa ya utawala bora.

Kwa hivyo, naishukuru Kamati kwa maoni haya na sisi tutayafanyia kazi, lakini wizara yangu tayari imeshatoa muongozo kwa taasisi zote za umma kwa kuona huu umuhimu wa hivi vitengo, sambamba na suala zima la matumizi ya *E-Government*.

Mhe. Spika, katika eneo hili nataka niseme kwamba Mhe. Mjumbe alitoa maoni kuwa pengine jambo hili linaweza kubakia kwenye makaratasi. Kwa kweli napenda nimhakikishie kwamba suala la matumizi ya *E-Government* halitobakia kwenye makaratasi na yeye mwenyewe anaelewa kuwa hivi karibuni tu serikali imeingia mkataba na Kampuni ya *ZANTEL*, kwa madhumuni ya kufanya kazi ya kuunganisha baadhi ya taasisi, ili huduma hii iweze kuanza kazi zake mara moja.

Baada ya kuteuliwa kwa Mkurugenzi, kazi nyengine ambayo ilikuwa inafanywa na wizara yangu ni kuhakikisha kuwahamisha baadhi ya wataalamu ambao watafanya kazi katika Taasisi hii ya Mawasiliano ya Habari ya Serikali nzima, ambayo yatakuwepo pale kwenye Kituo chetu cha *E-Government*. Mhe. Spika, tayari tumeshaajiri baadhi ya watu wenye sifa za kufanya kazi hizi.

Kwa hivyo, pengine tutakapokuja kwenye Kikao cha Bajeti tunaweza kueleza vyengine juu ya utekelezaji wa shughuli hii inayohusu masuala ya *E-Government* na mawasiliano ya habari katika serikali nzima kwa jumla.

Vile vile Mhe. Mwakilishi alieleza masikitiko yake juu ya suala la mchanganuo wa gharama za Mradi wa *E-Government* na jambo hili amekuwa analiuliza sana. Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba sisi kama wizara ambayo tumekabidhiwa uendeshaji tunajua gharama za jumla kwamba jumla ya dola za kimarekani milioni 19 zimetumika kwa ajili ya uwekaji mtandao huu wa Mkonga wa Taifa kwa madhumuni ya matumizi ya *E-Government*. *(Makofi)*

Sasa mchanganuo wake yule aliyetumia kupitia Wizara ya Fedha nafikiri Kamati inayohusika na Baraza hili linayo haki ya kujua, mimi nadhani hakuna cha kuficha. Kwa maana hiyo, kamati imetaka haijapata, basi sisi tutasisitizana serikalini, ili huo mchanganuo uweze kupatikana. Lakini jumla ya fedha zilizotumika ni hizo dola milioni 19. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia Mhe. Mjumbe alizungumzia suala la kuharakishwa kwa Mamlaka ya Rushwa ifanye kazi rasmi na Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumzia uhusiano kati ya utungaji wa sheria, uanzishwaji wa mamlaka na uanzaji kazi rasmi. Kwa kweli si hii tu Mamlaka ya Rushwa, lakini taasisi nyingi serikali tunaunga sheria pengine tunateua Mkurugenzi na kinachofuata sasa ni namna gani ya ile taasisi kuanza kazi.

Kwa maana hiyo, kweli kumekuwa na *delay* lakini hiyo si kwa sababu ya makusudi kwamba zile sheria zisiweze kutumika. Jambo hili alilizungumza Mhe. Mwakilishi kwa niaba ya Kamati, lakini Waheshimiwa Wajumbe wengi wameonesha wasi wasi huo.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema ni kwamba kuna mambo mengi ya kuyazingatia, ni kweli Mkurugenzi ameshateuliwa na imezungumziwa pia changamoto ya kutokuwa na ofisi ya kufanyia kazi. Kweli hivi sasa wapo katika eneo la muda, lakini serikali imeshaandaa utaratibu wa kuwatafutia eneo la kwenda kufanya kazi, ili waweze kufanya kazi zao.

Kutokana na hali, hivi sasa tumehamisha baadhi ya wafanyakazi wapo pale, lakini hivi karibuni mumesikia matangazo kwamba tumetangaza nafasi za ajira. Mhe. Spika, nataka nichukue nafasi hii kuwatoa wasi wasi wale ambao wana khofu pengine nafasi hizi za ajira zinafanywa kwa upendeleo, hapana nafasi hazifanywi kwa upendeleo na wala wizara yangu haitathubutu kuajiri watu ambao hawana sifa zinazotakiwa, isipokuwa tutaajiri kwa mujibu wa sheria.

Kwa mfano, hivi karibuni tutaajiri vijana 30 katika Taasisi hii ya Rushwa na tunatarajia kuwapeleka Tanzania Bara kwa ajili ya mafunzo maalum, pamoja na taaluma walizonazo, kwa sababu wengine wanazo taaluma za sheria, manunuzi, fedha, utawala, yaani taaluma tofauti, lakini lazima waende wakapata mafunzo ya ukakamavu kidogo, ili wanaporudi kuja kufanya kazi zao basi wawe wanajua zile kazi za kiupelelezi katika kufanya majukumu yao.

Kwa hivyo, vijana hawa karibu tutawapeleka na mchakato wa kuwaajiri utakapomilika, basi tutawapeleka Tanzania Bara kwa wenzetu watu wa TAKUKURU, ambao wanacho chuo kama hiki na wametuambia kwamba watatupa nafasi ya kuwapa mafunzo, ili vijana hawa waweze kufanya kazi vizuri.

Vile vile na wale watu wetu ambao tayari wapo pale tumewahamisha pia ni wataalamu, basi tunatarajia tutawapatia *short course* katika nchi zenye uzoefu wa masuala haya ya rushwa, ili taasisi hii itakapoanza kazi wawe wana uelewa wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, jengine ambalo limeelezwa kwenye ripoti ya Kamati ni kuhusu Ripoti ya *CAG* kutobaini baadhi ya madhambi, ambayo yanafanyika katika taasisi na hatimaye Kamati ya *PAC* inapokuja inabaini. Kwa kweli tutajitahidi kushirikiana na *CAG* na kuihimiza kwamba watu wao au wafanyakazi wa Ofisi hii ya *CAG* wawe wakakamavu katika kutekeleza majukumu yao. Kwa hivyo, ninachoweza kusema ni hivyo ni kweli kuna tofauti wakati mwengine ripoti ile inakuwa hivyo.

Jambo jengine ambalo limejitokeza kwa Waheshimiwa Wajumbe wengine naomba nitoe ufafanuzi pamoja na majibu hapa hapa badala ya kuja kutaja mtu mmoja mmoja ni kuhusu suala lile linaloonesha kwa nini Ripoti ya *CAG* au Kamati ya *PAC* haifanyiwi kazi.

Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kusema katika vikao vilivyopita, kwamba serikali hivi sasa tumekuwa na mtazamo mwengine juu ya suala hili, kwa sababu haiwezekani tuwe tunapokea ripoti na halafu tuwe hatuzifanyii kazi. Vile vile kama nilivyosema Mhe. Spika, katika vikao vilivyopita ni kwamba serikali hivi sasa tumekuwa na utaratibu kwa Ripoti hizi za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa kweli tumeamua kuzikalia serikalini kwa maana ya kuizungumza na kubaini yale ambayo yamependekezwa, yameshauriwa au yameagizwa na hatimaye kila taasisi inatakiwa iwajibike katika kuyafanyia kazi. Na yale ambayo yanahusu katika uchukuaji wa hatua, yaani kuwachukulia hatua wahusika basi wahusika waweze kuchukuliwa hatua kisheria.

Kwa hivyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hilo limeanza na tutalitilia mkazo, ili liendelee kufanyika kwa dhana ile ile ya mchango wa wajumbe wengi waliosema ili dhana ya utawala bora uwepo lazima uwajibikaji uwepo. Kwa hivyo ninawashukuru sana wajumbe wote ambao wamelizungumza hilo.

Ripoti ya Kamati imezungumzia pia suala la ukosefu wa gari kule Ofisi Kuu Pemba. Nataka niwahakikishie kwamba si muda mrefu kamati ya tenda ya Wizara itaichagua kampuni ambayo itakuwa imeshinda katika ununuzi wa gari hii ya Ofisi Kuu Pemba. Gari ya Ofisi Kuu Pemba ilipata ajali na tulilipwa na Shirika la Bima lakini bahati mbaya fedha ambazo tumelipwa haziwezi kununua gari. Kwa hivyo wizara yangu imefanya uhaulisho reallocation lakini kuhakikisha kwamba Ofisi hii inapata gari kwa hivyo tatizo hili karibu tutalitatua.

Suala jengine lililojitokeza ni suala la mgao wa fedha Ofisi Kuu Pemba na Makao Makuu Zanzibar. Kwanza nataka niseme kwa mujibu wa utaratibu wa kibajeti fungu hili kweli ni moja lakini kasma ni tofauti. Kasma ya Pemba inapelekwa Pemba moja kwa moja wala haipitii makao makuu ya wizara. Sasa kama kuna tatizo la ufinyu wa uingiziaji kasma ya fedha katika Ofisi Kuu Pemba nafikiri hilo linaweza kuwa ni tatizo la kitaifa pengine kutokana na ufinyu wa namna ya

fedha zinavyopatikana katika mfuko mkuu wa hazina lakini haliusiani kabisa na suala pengine la kwamba Makao Makuu inajipendelea Ofisi Kuu. Serikali ilipofanya hivi ilifanya kwa kuondosha matatizo hayo.

Hata hivyo suala hilo nitalichukua kwa mara ya mwisho nilikuwepo Pemba nilihoji ni taasisi zipi bado ambazo hazijapata fedha za kufanyia kazi. Nilibaini kulikuwa na kitengo kimoja na nikaagiza kwamba kitengo hiki na halisababishwi na Makao Makuu kutoka Unguja, linasababishwa na utendaji wao wenyewe pale pale ndani, nikaagiza kwamba kwenye quarter hii tatu lazima kitengo hicho nacho kipatiwe fedha kwa ajili ya kufanyia kazi, kwa mujbu wa bajeti tulivyoipitisha. Sasa kama kuna mapungufu ya kibajeti naomba hili linaweza likawa ni tatizo la kitaifa na sio suala pengine la kwamba Pemba wananyimwa kupewa kasma hizo.

Lakini Mhe. Jussa baada ya maoni hayo ya Kamati na mengine kama nilivyosema nitayachukua ili kwenye Baraza la mwezi wa April kwa mujibu wa utaratibu tuliojiwekea basi nitaleta bango kitita kama tulivyowasilisha juu ya utekelezaji wa yale ambayo kamati itakuwa imetuagiza.

Lakini Mhe. Jussa alisema ana maoni yake binafsi kama Mwakilishi wa Mji Mkongwe na mimi nimshukuru hakutaka kuchanganya yale maoni ya Kamati na yale maoni yake. Na ndivyo utaratibu na kanuni zinaturuhusu. Kwa hivyo yeye alizungumzia lile lile suala aliliuliza kwenye suala la nyongeza moja, ameulizia suala lile na mimi sitokuwa na majibu mengine zaidi ya yale majibu niliyoyatoa katika mkutano huu huu wa Baraza la Wawakilishi. Ila ninalotaka kumwambia Mhe. Jussa kwamba *concern* yake tunaielewa na tunaipokea na hata serikali ilipoamua kufanya mageuzi katika utumishi wa umma lilikuwemo na suala hilo ambalo wewe unaliona kwamba ni tatizo na hatujamaliza bado. Ripoti kweli ilitolewa kama ulivyouliza swali la nyongeza siku ile na mimi nataka nikuhakikishie, sisi tumeshapitia majukumu ya Wizara na ya watumishi kujua kila mtumishi ana majukumu yepi je kweli majukumu haya aliyonayo mtumishi huyu au iliyonayo taasisi hii, iliyona wizara hii yanastahiki kuwa na idadi ya wafanyakazi kumi au wafanyakazi 5 au wafanyakazi wangapi.

Sasa ni mapema mno kuweza kutoa jibu kwamba iwe vipi lakini ninachoweza kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba sisi serikalini tunaliona hilo na ndio maana tukaandaa huu utaratibu wa kuwapima wafanyakazi, kufanya mapitio majukumu ya taasisi na wizara ili kuona kwamba idadi ya watumishi tulionao kama ni wengi au ni wachache. Naomba jibu hilo lifatie baada ya taarifa rasmi itakapokuwa imekamilika ili tuweze kuja kulitolea ufafanuzi.

Kuajiri watumishi wasio na uwezo, kama ulivyosema katika serikali yetu kwenye utumishi wa umma tuna wafanyakazi wapatao thalathini nane elfu. Watumishi ambao wana viwango vya chini vya elimu kuanzia ngazi ya form 1V ni 15,000 kati ya hao 38,000. Sasa katika hili lazima tuta-take time katika kuona ni kwa kiasi gani watumishi wenye sifa zinazolingana tunawanini, lakini hawa ambao wameajiriwa wameajiriwa kabla ya taratibu hizi za sasa za kufata sheria iliyopo ya utumishi wa umma sheria namba 2 ya mwaka 2011 haijaanza kufanya kazi.

Nyote ni mashahidi katika wakati wa sasa tunapotangaza nafasi za ajira mnasikia kwamba tunatangaza nafasi za ajira na sifa za wale wanaotakiwa kuajiriwa. Na mtu anapokwenda kupeleka maombi yake akawa hana zile sifa ambazo zimetangazwa kabisa kwa nafasi hii utakuwa hustahiki subiri kama itatokezea nafasi hiyo ambayo inalingana na elimu yako.

Kwa hivyo tutawa-phase out hawa hatua kwa hatua hatimae tutabaki na wale watumishi ambao wote watakuwa na sifa zinazolingana na majukuju ambayo wamepangiwa. Hatusemi kwamba tutafika pahala kwamba watumishi wote wawe ni wasomi, bila shaka zitakuwepo nafasi ambazo hazihitaji kuwa na elimu kubwa. Naomba kwa hili nizungumzie hapo.

Nije kwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye amezungumzia yule mfanyakazi wa Wizara ya Afya Pemba kwamba nilimuahidi lakini siku ile nilitoa ufafanuzi lakini napenda nimfahamishe kwamba ni kweli tatizo hili lilikuwepo, na sasa hivi Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya inalichukulia hatua, wapo wafanyakazi wawili, tatizo nini? Tatizo ni kwamba kabla ya kuwepo kwa hii sheria ya utumishi wa umma kulikuwa na zile kanuni za utumishi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe wale wanaotoka nje kwa dharura kidogo mkubuke kwamba si muda mkubwa shughuli hii tunategemea kuimaliza, kwa hivyo niwaombe kwamba tushirikiane nasi ili tuweze kumaliza shughuli hizi kwa mujibu wa taratibu wa kutimiza akidi inayohitajika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ahsante sana Mhe. Spika, tatizo ni kwamba hapo nyuma kabla ya kupitishwa kwa sheria hii watu walikuwa wanajisahau wale waliokuwa wanasimamia mamlaka zile za nidhamu. Mamlaka ya nidhamu inaanzia kwa Mkuu wa Taasisi kuanzia ngazi ya Mkurugenzi kuendelea. Sasa taratibu hizi zilikuwa zinasahaulika, mtumishi anafanya kosa kweli lakini anachukuliwa hatua bila ya kuangalia au bila kuzingatia utaratibu uliopo kwa mujibu wa kanuni za wakati ule kanuni za utumishi. Lakini kwa sasa kwa mujibu wa sheria kwamba mtumishi anapofanya kosa anatakiwa ende hatua kwa hatua. Na hiyo ililekea nini? Kwamba mtumishi kweli amefanya kosa lakini anapokwenda mahkamani anaishinda serikali kwa sababu zile taratibu zilizostahiki kuchukuliwa hazikuchukuliwa tokea mapema. Sasa matokeo yake serikali siku zote inakuwa inashindwa.

Kwa sasa madhali sheria ipo inaelekeza vizuri kwamba mtumishi anapofanya makosa ni lazima mamlaka ya nidhamu ianze kuchukua hatua yenyewe naiunganisha na hili suala ambalo amelizungumzia Mhe. Hamza la watumishi wa *CAG*, ni kweli hiyo kadhia ilikuwepo lakini utakutia mkuu wa Taasisi anapoamua tu kwamba huyu amefanya makosa kwa hivyo unawapeleka watumishi kwenye Wizara ya Utumishi, sasa Wizara ya Utumishi, sasa Wizara ya Utumishi iwafanye nini? Au mtumishi amefanya makosa Wizara fulani unampeleka Utumishi wamfanye nini? Anza wewe kumchukulia hatua za nidhamu kwa mujibu wa sheria, mpaka ufikie pahala kwamba sasa yule mtumishi baada ya wewe kumchukulia hatua hakuridhika na hatua ulizomchukulia ata- *appeal* kama taasisi inaendeshwa na bodi ata- appeal kwa bodi. Kama kwenye bodi hakuridhika ata-*appeal* kwenye Tume ya Utumishi ama Kamisheni ya Utumishi. Hatua zote hizo zikichukuliwa kwa mujibu wa sheria hata akenda mahkamani, mahkamani hawezi kufanya maamuzi mengine. Sasa utakutia utaratibu huo ulikuwa ukikosewa, sasa naziomba Taasisi na Wakuu wa Taasisi wale wenye mamlaka ya nidhamu kwamba anapofanya makosa mtumishi wako, wewe mwenyewe kwanza ndio unaewajibika kumchukulia hatua za nidhamu ili kuondosha hii mizozo na migogoro ambayo inaweza isiwe na tija kwa nchi yetu.

Sasa nataka niliseme hili kwamba utaratibu wa watumishi wote wawili wa Wizara ya Afya ambao kesi yao iko mezani kwangu tatizo lenyewe ni hilo kwamba wewe Mkuu wa Taasisi umemsimamisha kazi mtumishi baada ya kumgundua kwamba hana matatizo ni wewe mwenyewe unatakiwa umrejeshe kazini. Unapomsimamisha kazi unaleta nakla utumishi wa umma ili sisi tunaweka block ya mshahara alipwe nusu mshahara. Unapomrejesha kazini baada ya kujiridhisha sisi tunaondosha block ili aweze kupata mshahara kamili. Sasa urasimu huu ukifanyika unaleta utumishi wa umma ufanye nini, wewe amefanya makosa chukua hatua za kinidhamu usimuonee. Ukeshachukua hatua za kinidham hakuna mtu atakaekuhoji kwa sababu sisi tunakwenda kwa mujibu wa sheria, sheria hii tumeipitisha juzi. Ndio pale mnaposema waheshimiwa wajumbe kwamba sheria hatuzifanyii kazi.

Kwa hivyo, naziomba Taasisi zote, wakuu wote wa Taasisi wafate sheria ya utumishi ya umma pale mtumishi anapokuwa amefanya makosa ili kuondosha huu utata ambao unaweza kujitokeza. Kwa hivyo Mhe. Mshimba nikuhakikishie kwamba yule mtumishi ambaye ulinambia na siku ile nilikujibu suala lake litashughulikiwa na atapata haki zake kwa mujibu wa sheria. Tuligundua kwamba kulikuwa na makosa ambauo yalifanyika na hayo makosa hayawezi kumfanya yeye asiweze kupata haki yake.

Nilizungumze la jumla la suala la ajira ya upendeleo. Mimi nataka niwahakikishie waheshimiwa kwamba hivi sasa hakuna ajira ya upendeleo, kwa mujibu wa kifungu cha 57 cha sheria yetu ya Utumishi wa Umma kinatoa mamlaka kwa Tume za Utumishi kufanya ajira. Masharti ya uajiri yapo katika kifungu cha 57 kifungu kidogo cha 3 (a) (b) na (c) kinaeleza wazi uajiri ufanyike vipi. Nafasi zitangazwe ziwe wazi kuwe hakuna upendeleo wa aina yoyote.

Na katika kifungu hiki kifungu kidogo cha sita kinatoa nafasi kwa Kamisheni kuchungua uajiri ama kwa mtu mwenyewe kupeleka malalamiko Kamisheni, ama kwa Taasisi kupeleka malalamiko Kamisheni. Na iwapo Kamisheni itabaini kwamba uajiri huo umefanyika kwa upendeleo au kwa hila au kwa udugu au kwa nini, Kamisheni ndani ya miezi 3 baada ya kufanyika uajiri ina uwezo wa kuchunguza na kusimamisha na kufuta uajri huo na ajira itangazwe upya. Sasa waheshimiwa wajumbe pale mnapoona kwamba kuna tatizo la ajira pahala limetokea, ajira imefanyika kwa upendeleo, basi ni vizuri yule ambaye analalamika apelike taarifa hizo Kamisheni ya Utumishiwa Umma. Ama mtu mwenyewe binafsi anaweza akapeleka malalamiko ama Taasisi ama chombo kwa jamani kulifanyika, samahani natoa mfano kwenye chombo chako kulifanyika uajri Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi ilifanya uajiri, lakini tuna wasiwasi kuna upendeleo umetokea ndani ya miezi mitatu kwa mujibu wa sheria hii Kamisheni ya Utumishi inao uwezo wa kuchunguza na ikijiridhisha kwamba hayo yaliyoelezwa ni sahihi basi uajri huo utafutwa na utatangazwa upya, ndivyo sheria yetu inavyosema.

Sasa kama kuna upendeleo huko unatokea watu hawatoi taarifa hilo litakuwa ni tatizo na wala tutakuwa hatujaisaidia nchi, wala hatujaisaidia serikali. Kwa hivyo ninawaomba waheshimiwa wajumbe kama kuna dalili za upendeleo kwenye ajira hizi basi sheria ipo wazi tuarifiwe. Kwa mfano kama suala lililojitokeza kule juzi Pemba la Shirika tumeagiza bodi ilete taarifa na Kamisheni imeagizwa ifatilie tukibaini kwamba ni kweli yale yaliyoelezwa na yaliyolalamikiwa basi Kamisheni itafuta uajiri kwa mujibu wa sheria hii. Lakini kama hakuna malalamiko maana yake labda mambo yamekwenda sawa.

Natoa mfano kwa Shirika la Umeme ambayo kesi imejitokeza hata imezungumzwa kwenye Kamati Teule. Lakini sambamba na hilo nataka niseme kwamba limezungumzwa pia suala la ajira limezungumzwa hasa ya ualimu pengine imetolewa kwa upendeleo. Au Pemba Mhe. Saleh aliuliza kwa nini hatutoi kibali, napenda nimuarifu kwamba Wizara ya Elimu tumeishaipa kibali cha walimu 408 namna gani sasa hizo ni shughuli zao wenyewe kuwajazisha mikataba lakini tumeshatoa hicho kibali na ilizungumzwa suala la kwamba kuna ubaguzi Pemba wamepelekwa walimu wachache.

Tume tulijitahidi sana kama nilivyoahidi kwenye Baraza hili kwamba sasa tutaangalia mahitaji na mapungufu kule kwenye upungufu ndiko tutakapoajiri. Katika walimu Pemba tulitaka walimuwa Diploma ya sayansi 48, Chake 51, Micheweni 21, Mkoani 38 jumla 158. Digirii Wete 31, Chake 17, Micheweni 8, Mkoani 10 jumla 22. Wote tulikuwa tunahitaji walimu 224. Lakini waliojitokeza na ndio walioajiriwa wenye sifa hizo Wete 33, Chake 28, Mkoani 10, Micheweni 21 jumla 96. Ni kwamba tatizo hawa vijana wetu ukiwaambia unawaajiri pahala fulani penye shortage wengi wao hawataki. Sasa sisi waheshimiwa wawakilishi tuwahamasishe. Walimu wengi wanataka waajiriwe katika miji hasa mji wa Unguja hilo ni tatizo. Sasa Pemba kwa kipindi hiki kwa wale walimu 408 wameajiriwa walimu 96 lakini si kwa sababu upendeleo ndio waliotaka kujitokeza kuajiriwa kwa wale walimu wa sayansi wengine wote hawakutaka. Lakini nafasi tulizozitoa zilikuwa 224 lakini tuliowapata ni 96 tufanyeje. Kwa hivyo mimi niwaombe waheshimiwa wawakilishi tulione hili na tuhakikishe kwamba tunashajihisha vijana wetu ili tuweze kupata walimu.

Limezungumzwa suala la utawala bora ni kweli Wizara hii ina jukumu la kupima namna ya utendaji wa serikali, sisi serikalini tumeshaelewana kwamba nitakapokuwa mimi sasa ninasimamia hilo suala la upimaji nisijeonekana kwamba ninachukua mamlaka ya wakubwa wengine ni jukumu langu kisheria na kwa mujibu wa utatibu. Na bahati nzuri Wizara yangu ni wizara mtambuka vile vile. Kwa sababu hiyo ya kupima utendaji inafanywa na kikundi kazi cha utawala bora kitaifa ambacho kikundi kazi hiki kina wajumbe kutoka wizara zote za SMZ. *Draft* ya awali imekamilika hivi karibuni tunatarajia kuifanyia kazi na kama ilivyo sera na sheria taarifa hiyo ninawajibika kuiwasilisha rasmi ndani ya Baraza lako tukufu Mhe. Spika, na wajumbe wat apata nafasi ya kuichangia. Kwa hivyo hakuna suala la kuficha uovu kuna suala la uajibikaji yule ambaye hawajibiki tutamuonesha na sio kwa madhumuni kwamba yeye azidishe kasi tu atimize majukumu yake. Kwa hivyo ripoti hiyo itawasilishwa Mheshimiwa.

Jambo jengine ambalo nataka nilizungumzie limezungumziwa suala la Taasisi za Serikali kulindwa na askari wenye uwezo, wizi mwingi unatokea katika maeneo hayo. Serikali inakusudia kutengeneza utaratibu wa kuhakikisha Taasisi zote za Serikali zinaalindwa na vikosi vya SMZ. Hilo tumeliona kwa sababu wezi wale wadokozi wanapata nafasi ya kufanya uhalifu. Hivi karibuni umefanyika uhalifu katika Chuo changu kule cha Utawala wa Umma umefanyika uhalifu na kwa sababu askari waliopo pale walikuwa hawana silaha za moto. Kwa hivyo tumeliona hili ni tatizo.

Na kama askari wanaweza kulinda kwenye vituo binafsi vya watu vya biashara why wasiweze kulinda kwenye vituo vya serikali au kwenye Taasisi za Serikali. Serikali ndio inayowalipa mshahara na kama hakuna kazi maalum ya operation basi askari hao ni lazima walinde Taasisi za Serikali na mali za serikali badala ya kulinda mali za watu binafsi peke yao.

Migogoro ya ardhi imezungumzwa sana kazi yangu mimi ni kupokea malalamiko. Kuna suala la kutatua na suala la kupokea malalamiko halafu ukaweza kuyashughulikia. Napenda niwaarifu kwamba malalamiko yote yaliyoletwa Wizarani kwangu tumeyashughulikia na Taasisi zinazohusika wameyapatia ufumbuzi. Lakini sasa unapotaka nishughulikie mimi kesi ya ardhi taratibu haziniruhusu. Kuna Taasisi ya Ardhi, kuna Mahkama ya Ardhi hayo yatashughulikiwa huko, lakini kwa maana ya malalamiko na sio ya ardhi tu ni kweli yanasimamiwa na masuala ya utawala bora.

Sasa kwa jinsi gani yanatatuliwa ndio hayo yatakayokuja kwenye ripoti ya utawala bora kwamba kuna uajibikaji au hakuna uajibikaji. Lakini katika suala la kwenda kuyashughulikia ziko Taasisi kwa mujibu wa sheria zimepewa mamlaka hiyo ya kuyashughulikia kwa maana ya kuyatatua. Sasa sisi kama Wizara tunapokea malalamiko, kama malalamiko hayajaja kwetu hilo jambo hatuwezi kulishughulikia. Malalamiko tutayashughulikia iwapo yatakuja kwetu, tutaagizwa na viongozi wetu wa kitaifa na kwa hapa Baraza la Wawakilishi kiongozi wetu ni Makamo wa pili wa Rais. Yapo ambayo aliyaleta in writing kwenye Wizara yangu na hayo tumeyashughulikia. Lakini Baraza hili linaweza likasema mimi vile vile nikayafatilia. Na nikeshayafatilia nayaweka katika line inayohusika. Linalohusu mahkama linakwenda mahkamani, linalohusu mahkama ya ardhi, litakwenda mahkama ya ardhi. Linalomuhusu mtendaji litakwenda kwa mamlaka ya nidhamu inayohusika na mamlaka nidhamu ichukuwe hatua. Kazi yangu mimi ni kuripoti kwenye ripoti ya utawala bora juu ya uajibikaji.

Mhe. Spika, nilisema niliseme hili kwa sababu limezungumzwa sana. Suala la Scheme of Services limezungumzwa na suala la nyongeza ya mishahara na malalamiko ya mishahara, bado Mhe. Mohammed Haji Khalid na wengine wamelizungumzia hili. Utaratibu upo kama kuna mtu anahisi amepunjwa aseme nimepunjwa ili arekebishiwe. Lakini Scheme of Service za Wizara zote ziko tayari na hizo ndizo zinazotuwezesha kujua kila mmoja na daraja yake na kiwango chake cha mshahara ambacho anastahiki kulipwa.

Mhe. Spika, yalikuwepo mengi lakini kwa sababu ya muda naomba niyaseme hayo machache na mengine tukijaaliwa yale ambayo nimeyapokea hapa nitakuja kuyatolea ufafanuzi siku nyengine kwa sababu naona tumebakiwa na robo saa na kuna Mwenyekiti wa Kamati anataka kuja kutoa ufafanuzi. Mheshimiwa nilokuwa sikuyajibu, sikuyajibu kwa sababu ya muda lakini ningeweza kuyatolea ufafanuzi,

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Spika: Ninafikiri Mwenyekiti wa Kamati muda uliobaki haumtoshi basi niombe Mhe. Waziri atoe hoja kuongeza muda kidogo ili shughuli hii imalizike kwa kumpa wasaa wa kutosha Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Kny. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba tuweke kanuni kando ya muda ili kumruhusu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala

aweze kutoa majumuisho na baada ya shughuli hiyo kumalizika basi ndipo tuweze kuliahirisha Baraza. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tusiwe na wasi wasi, Mjumbe aliyekuja kwa niaba ya Mwenyekiti hapa mambo yake huwa anaweka kwa kifupi, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Kny. Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Azza Wajalla kwa kuendelea kuturuzuku neema zake na kutujaalia kuwa hai na wazima tukiendelea na shughuli za chombo hiki muhimu katika maisha ya wananchi wa Zanzibar.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kufanya majumuisho kuhusiana na mjadala wa Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo inazisimamia wizara mbili hizi Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Tatu Mhe. Spika, naomba niwapongeze na kuwashukuru Wajumbe wote ambao walichangia ripoti yetu hii. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Omar Ali Shehe
3. Mhe. Hija Hassan Hija
4. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
5. Mhe. Ali Salum Haji
6. Mhe. Mohammed Haji Khalid
7. Mhe. Hamza Hassan Juma
8. Mhe. Subeit Khamis Faki
9. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
10. Mhe. Saleh Nassor Juma

Vile vile Mhe. Spika, naomba niwatambue Waheshimiwa Mawaziri makini, mahiri, weledi wawili wanaoongoza wizara hizi Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kufanya kazi mbili, ya kwanza ile ya kuja kuwasilisha ripoti ya utekelezaji kwa ripoti ya mwaka uliopita, lakini hivi punde pia wakiwa wamefanya kazi ya kutoa majibu ya hoja mbali mbali ambazo zilitolewa na Waheshimiwa Wajumbe na pia katika ripoti ya kamati yetu.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba kamati yetu inasimamia wizara mbili tu, lakini umuhimu wake umeonekana kutokana na idadi ya Wajumbe waliochangia lakini na wingi wa hoja ambazo zimetolewa. Mhe. Spika, haraka haraka nimekusanya kama hoja 51 ambazo zimetolewa na

Wajumbe mbali mbali na katika hizo hoja 30 zilikuwa zinahusu Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora na hoja 21 zinahusu Wizara ya Katiba na Sheria.

Wasishituke Wajumbe wako Mhe. Spika, sikusudii kwamba kamati yetu itapitia hizi hoja moja moja katika hoja 51. Mhe. Spika, kama nilivyosema sikusudii kwamba kamati yetu itajibu hoja zote hizi moja moja, kwa sababu kwanza nyingi kati ya hizi tayari zimetolewa ufafanuzi na maelezo na mawaziri wa wizara za sekta husika. Mimi nitagusia yale maeneo ambayo nahisi yanahitaji kutiliwa mkazo na mengine katika kuwasisitiza Waheshimiwa Mawaziri ili wajiandae hasa kwa kikao kijacho cha bajeti waje vizuri zaidi katika masuala haya na kutoa ufafanuzi ambao wananchi wa Zanzibar wanautegemea.

Lakini moja ambalo Mhe. Spika, limezungumzwa na Wajumbe wengi na alilisisitiza sana Mhe. Omar Ali Shehe ni suala zima la uwajibikaji serikalini. Mhe. Spika, kusema kweli hili ni suala ambalo tunapaswa tujifunze sana, katika serikali ambayo inakumbukwa na wananchi na hata sisi baadhi yetu vijana ambao hatukuiwahi lakini tumeisoma, tumewasikia wazee wananchi wa Zanzibar wanaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Kwanza iliyoongozwa na Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume. Bila shaka ilikuwa serikali ya binadamu na ilikuwa na mapungufu yake, lakini kwa maana ya maendeleo mpaka leo imeacha *symbols*, imeacha *monuments* ambazo zinaonekana kwamba haya yalikuwa ni mafanikio ya serikali ile na mpaka leo Wananchi wa Zanzibar wanaendelea kunufaika na huduma ambazo zimeanzishwa wakati ule.

Lakini Mhe. Spika, ukitizama serikali ile ilikuwa ni serikali ndogo sana, serikali ambayo ilileta mabadiliko makubwa sana ilikuwa na jumla ukimchanganya Rais na Makamo wa Rais, Mawazidi na Wasaidizi Mawaziri ilikuwa na watu kumi tu basi Mhe. Spika, na kwa faida ya Wajumbe hawa naomba niwataje ili tuikumbuke hasa.

Ilikuwa inaongozwa na Mhe. Rais mwenyewe Mzee Abeid Amani Karume, Makamo wa Rais, Mhe. Abdalla Kassim Hanga. Lakini ilikuwa ina wizara nyengine sita basi Mhe. Spika, Wizara ya Fedha na Maendeleo iliyokuwa ikiongozwa na Mhe. Hasnu Makame Mwita, Wizara ya Mambo ya Nje na Biashara ilikuwa ikiongozwa na Mhe. Abdulrahman Mohammed Babu; Wizara ya Kilimo ilikuwa ikiongozwa na Mhe. Saleh Saadalla Akida; Wizara ya Kazi, Njia na Nguvu za Umeme iliyokuwa ikiongozwa na Mhe. Idrissa Abdul-Wakil Nombe; Wizara ya Elimu na Utamaduni ilikuwa ikiongozwa na Mhe. Othman Sharif Mussa na Wizara ya Siha ambayo sisi tunasema Wizara ya Afya ikiongozwa na Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi. Na mawaziri wasaidizi wawili tu Mhe. Spika, Waziri Msaidizi katika Ofisi ya Rais ambaye alikuwa Mhe. Abdulaziz Twala na Waziri Msaidizi katika Wizara ya Kazi, Njia na Nguvu za Umeme Mhe. Hassan Nassor Moyo, yuhai mpaka leo, Mwenyezi mungu ampe umri mrefu.

Lakini Mhe. Spika, serikali hii na mawaziri wachache hawa ije ilete mabadiliko katika miaka minane ambayo mpaka leo wananchi wa Zanzibar wanayakumbuka haya. Sasa tujikufunzo hilo Mhe. Spika, ni kweli idadi ya watu wetu imeongezeka, tunaongeza idadi ya serikaki, tunaondeza wananfhina wawakilishi wananchi hapa, lakini bado wanalalamikia uwajibikaji tujitizame tumekosea wapi.

Mhe. Spika. hili nalisema hapa katika majumuisho kwa sababu ni la jumla na ni la muhimu kwamba wizara anayoiongozia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utawala Bora ilitazame tena na iishauri serikali limahauri Mhe. Rais atambue kuna nini. Serikali ya Awamu ya Saba Mheshimiwa imeingia kwa vishindo vikubwa, kulikuwa na Ngurdoto za Zanzibar nyingi tu walijifungia Mawaziri, wakajifungia Makatibu Wakuu, wakafungiwa ndani humo Wakurugenzi wakaja mpaka Masheha, lakini bado ukija katika utendaji wananchi wanalalamika sana.

Mhe. Spika, haikuishia hapo tu, serikali hii ikachukua watendaji ikawapeleka China wakajifunze kasi ya maendeleo ya Wachina na fedha za walipa kodi zikatumika lakini bado tukija tukitizama utendaji watu hawaridhiki. Tumekuja na mabango kitita hadithi ndio hiyo hiyo tukija katika utendaji bado watu wanalalamikia utendaji wa serikali. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hili Mhe. Spika, nadhani imefika pahala ile miongozo inayotolewa na Baraza la Wawakilishi, malalamiko yanayotolewa na wananchi serikali yenyewe ifanye tathmini ijitizame inakosea wapi kuwa bado kuna malalamiko kiasi hichi. Mhe. Spika, hilo nilitaka kusema la jumla.

La pili Mhe. Spika, kama nilivyosema sikusudii kwenda katika michango yote ambayo imetolewa na Wajumbe kwa sababu mingi imeshapata ufafanuzi, nitaomba kuyagusia yale machache ambayo wenzangu wameyaacha. Nianze na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Spika, ambalo halikugusiwa hapa la Mhe. Makame Mshimba kwanza alizungumzia kuhusu uajiri, yeye alitofautiana na mimi katika yale maoni yangu binafsi niliposema kwamba, tuna wafanyakazi wengi lakini tija haionekani, yeye akataka tuongeze uajiri halafu akasema wawakilishi na sisi tupewe. Mhe. Spika, mimi sikubaliani naye kabisa katika hilo na naomba mambo kama haya tuchukulie *serious* Mhe. Spika. Kwa sababu suala la uajiri sisi ndio tuliopitisha sheria ya Utumishi wa Umma hapa, lakini ukianza kuisiasisha, ukai-*politicize* suala la uajiri tutapata matatizo.

Ni kweli tunakerwa sana katika majimbo ni kwa sabahu wananchi wetu wengi hawajaelewa nini kazi ya Mwakilishi, kila mtu lake anakuletea wewe. Kwa hivyo hata suala la ajira anakuletea wewe, lakini tukianza kusema kwamba tupewe nafasi wawakilishi tulete watu katika wizara zinazohusika Mhe. Spika, tutapata matatizo sana. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hili siliwafiki na nashukuru kwamba Mhe. Waziri pia hakulisikia nadhani kwamba haliwafiki na linakwenda kinyume na sheria ambayo tumeipitisha hapa.

Jengine Mhe. Mshimba aliuliza kwamba tumetaja Mahkama ya Makunduchi kamati hawakuiona Mahkama ya Mfenesini? Mhe. Spika, tumeiona na katika mazungumzo mengi tuliofanya na wizara tumelizunguzma, lakini tuliitaja ya Makunduchi katika ripoti ya mwaka huu makusudi kwa sababu hali yake ni mbaya na kwamba hairidhishi hata kutumiwa, inaweza kuhatarisha maisha watu ambao wanakwenda pale kufuata huduma ndio maana tuliitaja mahsusi. Lakini kusema kweli hali ya Mahkama zetu nyingi bado zina matatizo ukiwauliza wizara wana jawabu ya msingi kwamba bajeti bado iliyotengwa kwa kutengeneza majengo haitoshelezi, hivi sasa nguvu kubwa zimeelekezwa katika kutengeneza jengo la Mahkama Kuu lilioko pale Vuga.

Mhe. Oma Ali Shehe kazungumza mengi lakini bahati nzuri mengi yamegusiwa na mawaziri husika kwake nilikuwa naomba niyaguse machache tu. Moja Mhe. Spika, kazungumzia suala la maslahi ya wafanyakazi, hili waziri hakupata bahati ya kuligusia pengine kali-*reserve* kwa ajili

ya hotuba yake ya bajeti *In shaa Allah*. Lakini mimi nataka nikubaliane kwa niaba ya kamati na Mhe. Omar Ali Shehe katika ile hoja moja, kwamba mbali ya suala la kuwa tuna watumishi ambao uwezo wao na sifa zao zina walakini, Mhe. Waziri kazungumzia kwamba kati ya wafanyakazi 38,000 tulionao wafanyakazi 15,000 wana kiwango cha kidato cha nne elimu yao, hii ni hatari.

Mimi naamini tungefanya vizuri zaidi tukagundua kwa sababu pengine hata katika hao kuna udanganyifu. Na ninarejea kwa sababu kulikuwa na ripoti ambayo ilitolewa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi wakati ule Mhe. Ramadhan Muombwa ambayo ukifanya majumuisho ilikuwa inasema kwamba, ni asilimia 18 tu ya wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mpaka inaletwa ripoti kama miaka mitano mpaka sita iliyopita ndio waliokuwa na sifa ya kutumikia nafasi zao. Hiyo maana yake Mhe. Spika, asilimia 82 ni watu ambao ama hawana sifa au wana sifa chini ya viwango vinavyotakiwa. Yote ni matatizo. Tutakwenda Ngurdoto, tutakwenda China, tutakwenda Singapore kama hatulitibu hilo bado tutaendelea kupata matatizo makubwa katika utendaji wa serikali na huduma ambazo tunategemea kuwapa wananchi.

Lakini la pili Mhe. Omar Ali pia amezungumzia la kuliunganisha na lile la maslahi kama nilivyosema. Hili Mhe. Spika, ni la msingi siwezi kuiambia serikali kwa niaba ya kamati kwamba iongeze kwa kiasi kadhaa kwa sababu tunajua hali ya uchumi wetu.

Pia kuna suala la *priority* na kuziba mianya ya kuvuja mapato, na leo Mhe. Waziri wa Fedha hayupo. Kwa sababu mimi naamini tukiziba mianya ya kuvuja mapato watakuja kulijadili kwa urefu ikifika kamai yao ya Fedha, Kilimo na Biashara Mhe. Spika, tunaweza kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambazo zinaweza zikasaidia angalau kupandisha kiwango kidogo. Kwa sababu Mhe. Spika, kuna ile hoja inayosema, *"You pretend to pay me, I pretend to work"*, (unajidai kunilipa na mimi nitajidai nafanya kazi) ukiwa unanilipa chini ya mahitaji yangu.

Mimi ili niishi leo kama mfanyakazi Mhe. Spika, nahitaji angalau akali minal-kalili nipate labda shilingi 20,000 kwa siku, lakini serikali ikinipa mshahara ambao nikiufanyia wastani napata shilingi 10,000 hizi nyengine za ziada nitazipata vipi, nitatafuta njia nyengine na nitakuwa sifanyi kazi niliyopewa nitakwenda kutafuta njia pembeni ili niweze kujiongezea mapato. Kwa hivyo, nasema msingi unasema kwamba, *"You pretend to pay me, I pretend to work*", ndio tutaendelea kufanya kazi katika hali zetu.

Kwa hivyo, hili Mhe. Spika, kwa upande wa Mhe. Omar Ali Shehe katika wizara hii nilikuwa nataka niligusia hili. Lakini pia amegusia na mimi naomba kulisisitiza suala la ripoti za Baraza la Wawakilishi kufanyiwa kazi kwa sababu ndio msingi mmoja wa utawala bora.

Mhe. Spika, hiki ni chombo cha kikatiba na ibara ya tano ya katiba imeweka wazi kifungu cha 5(a) kwamba hiki ni chombo cha usimamizi wa shughuli za serikali na shughuli za umma. Kwa hivyo, wanapokuja hapa wawakilishi wa wananchi wakafanya kazi, wakatumia fedha za walipa kodi chini ya muongozo wako Mhe. Spika, unapounda Kamati Teule wanapotoa ripoti zao zinahitaji zifanyiwe kazi ili matunda yaweze kuonekana.

Mhe. Spika, upande wa Wizara ya Katiba na Sheria hoja walizozitoa takriban zote amezijibu Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Hija Hassan amezungumzia kwa urefu zana ya utawala bora na akasema haitoshi kulitamka tu. Mimi nakubaliana naye Mhe. Hija, kwa sababu Waswahili wanasema “jina si mboje”. Mhe. Spika, kulikuwa na zama hapo wakati wa vita vya baridi ukiziona serikali zimetungwa majina ya kidemokrasi ndizo zilizokuwa hazina demokrasi, ile serikali ukisikia Jamhuri ya Kidemokrasi ya Watu wa Korea basi ndio ilikuwa haina demokrasi, ukisikia Jamhuri ya Kidemokrasi ya Ujerumani ilikuwa ndio jina lake hilo ukilinganisha na Ujerumani Magharibi. Kwa hivyo, mara nyengine kweli unaweza kuona jina likawa haliwakilishi sawa sawa kwamba unaheshimu ile misingi ya jina, muhimu ni utendaji wake. Ametoa vitu vingi, mambo ya msingi ambayo mengine amepata majibu hapa.

Mimi nilikuwa nataka kulisisitiza tena lile alilokuwa kalizungumza, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora nashukuru kaligusia ambalo kamati yetu pia imelizungumzia suala zima la mchanganuo wa mradi wa *E-Government*. Amesema mwenyewe Mhe. Waziri kwamba zimetumika US$ 19 milioni hizi ni fedha nyingi sana, sasa kamati imeomba mchanganuo, tulipelekwa pale tukaomba mchanganuo tukaambiwa tutaletewa hatukuletewa, tukaomba tukaambiwa tupeleke maombi Wizara ya Fedha tukapeleka barua kamati mpaka leo mwaka mzima tunaumaliza Mhe. Spika, hatujapata majibu, kunafichwa nini. Mimi binafsi nikichangia hapa niliwahi kusema kwamba ukitizama viwango vilivyokuwa vikihitajika mimi nilileta mchanganuo hapa kwamba fedha iliyokuwa ikihitajika ilikuwa labda ni US$ milioni tano, lakini pakaidhinishwa mkopo wa US$ 19 milioni, lazima tujue fedha za wananchi hizi, huu mkopo ni deni kwa wananchi wa Zanzibar Mhe. Spika, wanalipa kupitia kodi zao kwa hivyo lazima wajue.

Hili Mhe. Spika, naliunganisha hapo hapo na suala ambalo limechangiwa na baadhi ya watu katika suala la Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, imefika pahala ripoti za ofisi hii zibadilike, ripoti zao ni *very shallow* ukilinganisha hata na ripoti za Kamati yako ya Baraza la Wawakilishi Mhe. Spika, hawajifunzi hata hapo upande wa pili wa bahari. Kwenye Jamhuri ya Muungano ukienda juzi kumefanywa tathmini ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande wa Jamhuri ya Muungano imefanywa tathmini ya deni la taifa kwamba limechunguzwa kuonekana kuwa huko kwenye deni la taifa pia kuna ufisadi unafanyika, kwamba kuna pesa zaidi ya shilingi 22 milioni zimeliwa na wajanja chini ya mwamvuli wa deni la taifa.

Sasa mambo kama hayo pengine yalikuwa yanatokea Zanzibar, lakini Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haionekani kwamba inatoa ripoti ambazo ni *comprehensive* Mhe. Spika na hili kusema kweli linaleta walakini mkubwa sana katika utendaji wa serikali. Kwa sababu wao ndio wanaotakiwa wachunge matumizi ya fedha za walipa kodi.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Salum yake yalishaelezwa, alihoji suala la ubadhirifu wa shilingi 61 milioni za Chuo cha Utawala wa Umma. Halikupatiwa nafasi na Mhe. Waziri, lakini nataka nimwambie tu kwamba tutasubiri majibu wakati wa bajeti lakini na sisi kama kamati tunalichukua ili kulifuatilia zaidi, hatukuwahi kulipata tulichokuwa tumekipata ilikuwa ni

madeni ya serikali iliyoikuwa yakidaiwa na chuo kupeleka wanafunzi wake tukawahi kulileta katika Baraza lako Mhe. Spika.

Lakini na hili la pili alilolileta Mhe. Ali Salum kutokuwepo na uwiano katika mishahara baina ya Wahadhiri wa Chuo cha Utawala wa Umma na Wahadhiri na Walimu wa katika vyuo vyengine vya serikali hiyo hiyo. Hili tulileta katika Baraza lako, nilikuwa nadhani hili pia serikali imefika pahala ilitolee ufafanuzi. Kilichokuwepo katika Chuo cha Utawala wa Umma ni kwamba wanalipwa mishahara kama watumishi wengine kulingana na elimu zao, kwamba mshaharta uliowekwa ni huo, lakini kwamba kuna *package* ya Wahadhiri kama ilivyokwua katika vyuo vyengine kama Chuo cha Fedha pale Chwaka. Sasa imefika pahala serikali itazame vizuri.

Mhe. Mohammed Haji Khalid haya yalipata majibu ya kutosha kutoka kwa mawaziri wahusika, yote ya Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa upande wa Mhe. Hamza Hassan Juma la ardhi limejibiwa Mhe. Spika, suala la kuzuwia na kupambana na rushwa na wahujumu uchumi hili na mimi nataka niungane naye, kwamba tumepitisha sheria lakini sio wepesi wa kutunga sheria tu ikawa ndio tumemaliza hapo. Mhe. Waziri katuarifu kwamba wanategemea kuajiri vijana kama 30 ili mamlaka iweze kufanya kazi. Tunadhani ni muhimu ili hili liweze kufanikiwa.

Lakini katika majibu yake Mhe. Waziri amegusia kwamba wanafikiria na wameomba na wamekubaliwa kwenda kupeleka vijana hawa TAKUKURU nao kupata mafunzo. Mhe. Spika, mimi kidogo linanitia mashaka Chuo cha TAKUKURU. Kwa sababu unapeleka watu wako kujifunza pahali ambapo pana *best practice* sijui chuo chake, lakini TAKUKURU ni moja katika taasisi ambazo zimefeli kwa upande wa Jamhuri ya Muungano na kila siku tunasikia malalamiko ya Bunge, malalamiko ya wananchi, malalamiko ya Vyombo vya Habari juu ya kesi nyingi, maelezo mengi yanayokabiliwa lakini imeshindwa kuchukuliwa hatua.

Mimi nadhani na katika taasisi kama hii tulipopitisha sheria ile tulipata sifa nyingi kutoka katika Jumuiya ya Kimataifa, wala sidhani kama tutagharimika kitu pengine wizara ikifanya mazungumzo kwa mfano na Uingereza, ofisi yao ya *Serious Fraud Office (SFO)* ni katika ofisi ambayo inaheshimika dunia nzima katika masuala ya kuchunguza na kupambana na ufisadi na uhukumu uchumi, nilikuwa nadhani hebu wizara ifanye mazungumzo na Ubalozi wa Uingereza pengine wanaweza kupata nafasi ya Serikali ya Uingereza ikakubali hata kama si 30, lakini ikapata nafasi ya kupeleka wale watumishi wa ngazi ya juu ili wakenda kujifunza vipi wenzetu wanaibua ufisadi. Tunakumbuka Mhe. Spika, hapa palikuja suala la rada lilivaliwa njuga Uingereza sio hapa, hapa tungepigwa danadana tu upande wa Bungeni kule, lakini Uingereza lilivaliwa njuga *Serious Fraud Office* ikaibua kashfa nzito ikabidi suala lile mpaka serikali ambazo zimeathirika zikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilipe fidia kutokana na uchunguzi wao. Kwa hivyo, nadhani walitizame kwa karibu sana.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza pia alizungumzia suala la Tume ya Utumishi kufuatilia utendaji wa wafanyakazi. Nakubaliana nao kwa sababu inaonekana hata ile kauli iliyokuwa ikitolewa mwanzo kwamba tubadilike kutokana na *business as usually* sasa wananchi wakaifanyia zihaka

kauli ile. Kwa sababu wanaona kwamba tumesema sana tubadilike lakini walichokiona bado ni *business is usually*. Kwa hivyo, nadhani ule wito wa Mhe. Hamza unafaa kabisa ufanyiwe kazi.

Lakini pia Mhe. Hamza alizungumzia suala la Kamisheni ya Utumishi wa Umma kusikiliza malalamiko kutoka wafanyakazi waliokuwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba kuna watu pale wamesimamishwa imegika pahala suala lao limemalizwa. Sisi hatujalipokea hilo, lakini nakumbuka Mhe. Spika, liko jengine ambalo linahusu hapa hapa tulilitolea kauli, sikupitia kamati ya mwaka huu lakini katika kikao cha bajeti lilijitokeza sana, nadhani pia imefika pahali lije lipate ufafanuzi wakati wa bajeti ukifika nalo nafikiri pia aliliibua Mhe. Hamza huyo huyo kwamba, kuna malalamiko au kuna udugu- *nization* katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika masuala ya ajira. Sasa wizara inaweza kuwa inapitisha watu wanaotaka kuajiriwa lakini namna wanavyoajiriwa na wakapangiwa kazi kuna malalamiko hayo. Hili nadhani pia ikija wakati wa bajeti tuje tupate maelezo ya kutosha.

Yale ya Maofisa wa Habari katika mawizara yote yametolewa maelezo na waziri husika. Ya Mahakimu wa Mahkama za Mwanzo na posho zao na mishahara yamezungumzwa vizuri.

Vile vile amesema Mhe. Hamza amekubaliana na sisi katika kuipongeza Ofisi ya Mwanasheria Mkuu lakini na yeye aka-*note* kwamba tumezungumzia kuwa changamoto pekee iliyokuwepo na kutokamilishiwa fedha kuweza kukamilisha ujenzi wa ofisi yao. Hili Mhe. Spika, naomba nilitilie mkazo tena, kamati yetu inasisitiza sana kuweza kutolewa fedha ili waweze kukamilisha ujenzi wa jingo lao kwa wakati.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu huko tunakokwenda Mhe. Spika, tangu huko nyuma lakini sasa ni zaidi ni ofisi muhimu sana katika utendaji wa shughuli zetu. Tunapotaka kuingia katika uchumi unaojikita katika masuala ya mafuta na gesi asilia, tunapotaka kujikita katika kuwa na kitabu cha mikataba katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu lazima uwe na mazingira mazuri ya kufanyia kazi, wawe na nafasi ya kutosha, wawe na maktaba, wawe na vitu vingi hivyo ni vizuri jengo lile likakamilika ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Lakini Mhe. Hamza vile vile aliniletea mchango mmoja wa maandishi ambao niliukabidhi kwa mawaziri, bahati mbaya muda ulikuwa umemkwaza hakuwahi kulitolea kauli naomba niligusie tu mimi. Mhe. Hamza alizungumzia kwamba Baraza hili Wajumbe wake mara nyingi wamepiga kelele kwamba sheria ya utumishi wa umma na baada ya marekebisho ambayo Mhe. Waziri aliyaleta hapa yaliweka maelekezo na masharti vipi kuchukua wafanyakazi ambao wameshastaafu kupitia njia ya mikataba, kwamba kwa wale tu ambao wamo katika fani maalum ambazo huwapati katika vijana wako, *rare professions* inapatikana, lakini bado kuna malalamiko kwamba bado tunaendelea kuchukua watu ambao wameshachoka hata wengine huo uzoefu unaozungumzwa haupo mana hata zile akili zimeshachoka. Watu wanalalamika kuwa wamewekwa watu utendaji hauonekani wakati wako vijana wengi wengine wapya, wengine wameshatumika kipindi fulani wana sifa, wana viwango vya elimu vizuri, wanapaswa wapewe nafasi na wao watoe mchango wao katika maendeleo ya nchi hii. Kwa hivyo, suala la msingi kabisa tusije tukapigishana kelele wakati wa bajeti hapa tuje tupate maelezo mazuri kutoka serikalini.

Mhe. Subeit Khamis Faki nadhani yake yote yalishapata maelezo kutoka kwa mawaziri wanaohusika. Naungana naye mkono sana alipozungumzia suala la kuheshimiwa maoni ya wananchi wa Zanzibar waliyoyatoa katika suala la mjadala wa katiba, tunausubiri kwa hamu tuone utatufikisha wapi.

Lakini mhe. Spika, pia Mhe. Subeit kazungumzia suala moja ambalo Mhe. Waziri kaligusa Waziri wa katiba na Sheria na mimi naomba kidogo hili nitoe ushauri tu kwa wizara kama inaweza kulifanyia kazi. Kalalamika Mheshimiwa kwamba misikiti mizuri, madrasa nzuri zinajengwa katika maeneo ya miji tu vijijini kunasahaulika. Mhe. Waziri kajibu kwa usahihi kabisa kwamba hii mara nyingi inajengwa na watu binafsi, lakini nilikuwa nadhani labda kupitia uimarishaji wa taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria wamefanya kazi nzuri sana naomba kumpongeza Mhe. Waziri. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Ofisi ya Mufti, basi labda angefanya utaratibu ikawa ikawa mtu akitaka kwenda kujenga huko awe anapitia katika ofisi hizi ili waweze kumshauri hawezi kumpa maelekezo, lakini angalau kumshauri kwamba hapa tayari pana misikiti mizuri hebu paangalie na Micheweni. Nadhani hilo atalitizama vizuri Mhe. Waziri.

Mhe. Bikame yake yameshatolewa ufafanuzi, aliulizia juu ya suala la Mfuko wa Bima ya Afya lakini waziri hakupata nafasi ya kujibu. Lakini nadhani ninavyokumbuka mimi katika *survey* iliyofanyika mwanzo ni kwamba msisitizo uliwekwa kwanza kwa wafanyakazi wa serikali. Kwa sababu ili umpe mtu bima ya afya ni lazima uwe na uhakika wa kulipwa, sasa ukimchukua mkulima huko akija akichukua bima halafu baadae asiende kulipa hakuna utaratibu wa serikali kumhakikishia yule ambaye ametoa huduma. Kwa hivyo, lile suala la kwamba tuanze na watumishi wa umma kama ni *pilot project* tuone itafikia wapi ni la msingi ili kuona kwamba kikitokea chochote basi serikali inaweza kutumia mapato au mshahara wa yule mfanyakazi mhusika ikalipa masuala hayo.

Mhe. Spika, kwa Mhe. Saleh Nassor Juma ambaye alikuwa ni mchangiaji wa mwisho yake takribani yote yametolewa ufafanuzi isipokuwa lile la Hijja tu. Mimi nadhani Mhe. Saleh ana hamu ya kuwa Alhaj na yeye, kwa hivyo zaidi ya zile sifa nyingi ambazo anazo basi kataka pia aungane na wewe Mhe. Spika, awe Alhajj kama wewe. Kwa hivyo, nadhani hili mhe. Waziri kalisikia basi utapata nafasi akishauriwa basi anaweza kukupendekeza kwamba Mhe. Saleh Nassor na yeye vile vile awe Alhajj kwa niaba ya wananchi wa Chake Chake.

Mhe. Spika, nimalizie mwisho kabisa katika suala ambalo aliligusa Mhe. Saleh na waliligusa Waheshimiwa wengine na mimi nililigusa hapo kabla suala la hatma ya Zanzibar katika suala zima la mjadala wa katiba.

Mhe. Spika, nilipokuwa natoa mchango wangu binafsi niliomba kwamba tunahitaji sasa tupate muongozo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala hili, nikasema kwamba wananchi wameshatoa maoni yao wamemaliza kazi yao na nilisema kwamba wakati ule tulipoitaka serikali humu ndani Wawakilishi tuliungana pamoja kutaka serikali utoe muongozo ili kusije kukatokea mgongano huko chini, kwamba Zanzibar kama Zanzibar kwa umoja wake inahitaji ijue inataka nini juu ya suala hil. Tukaambiwa serikali haitaki kufanya hivyo kwa sababu itakuwa inaingilia maoni ya wananchi.

Sasa wameshamaliza tunakwenda katika hatua ya pili na ya tatu ambazo ni muhimu sana Mhe. Spika, hatua ya Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na hatua ya Bunge la Katiba ambalo Wawakilishi wako ndani ya Baraza hili tutapata nafasi ya kuwemo katika Bunge hilo, ni muhimu kuwe na kauli moja. Kwa hivyo, bado nasisitiza kwamba, tunahitaji muongozo wa serikali na katika hili nimuombe sana kama alivyosema Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hili si lake, kauli ya serikali tunataka tumsikie Kiongozi wa Shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Yeye ndiye kiongozi wetu katika Baraza hili na huko nyuma katika vipindi mbali mbali wenzake waliokuwa wameshika nafasi kama yake walikuwa wakitoa kauli nzito kwa niaba ya serikali katika masuala kama haya, na kiongozi mzuri Mhe. Spika, ni yule ambaye ana-*reflect* mawazo ya watu ambao anawaongoza.

Kwa hivyo nadhani hiki kilio cha Wawakilishi zaidi Mhe. Spika, akipokee Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na tuisikie basi kauli ya serikali kupitia mdomo wake juu ya huko tunakoelekea, nini Zanzibar inahitaji. Mhe. Spika, hakuna kitu kitamu kama kuitetea nchi yako hasa ikiwa kisiwa.

Mhe. Spika, *Napoleon Bonapatre*, mmoja katika wanavisiwa mashuhuri aliwahi mpaka kupigana kwa ajili ya Ufaransa dhidi ya Muingereza. Huyu alitokea katika kisiwa na baadae akazikwa katika kisiwa, moja katika kauli yake maarufu anasema "*there is nothing sweeter than the feeling that you are wanted at your birthplace and especially if it is surrounded by water"*. Anasema hakuna hisia nyengine nzuri zaidi kama hisia kuonekana unahitajika kwenu na hasa huko kwenu kama kumezungukwa na maji".

Mhe. Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mhe. Spika: Sasa kwenu Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale wanaokubali na kupokea Ripoti za Utekelezaji za Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya hadi wakati huu kwenye saa saba na dakika ishirini, lakini tumefikia pahala shughuli hii tumeimaliza. Basi nisichukue muda isipokuwa sasa niahirishe kikao hiki hadi saa kumi na moja jioni, ahsateni.

(Saa 7:20 Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11. 00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA YA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwa na afya njema na uzima uliotuwezesha kufika hapa leo na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa.

Aidha naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo ya Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwa dhati kabisa kuipongeza na kuishukuru sana Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake ya Baraza lako tukufu kwa kazi nzuri inayofanya kwa wizara yetu. Nataka nikiri mbele yako kwamba mafanikio tunayoyapata katika Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa sehemu kubwa yanatokana na ushauri pamoja na muongozo unaotokana na kamati hii ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake.

Ushirikiano wetu baina ya kamati na wizara ni mzuri na ni wa kupigiwa mfano na ndio unaotufanya kuweza kutimiza majukumu yetu ya kuwahudumia na kuwatumikia wazee, wanawake, vijana na watoto na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Namshukuru sana mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Amina Iddi Mabrouk kwa uongozi wake na jinsi anavyoisaidia wizara yetu akishirikiana na kamati yake.
Kwa heshima kubwa napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi kwa jinsi wanavyonipa ushirikiano wao wa dhati kwangu mimi binafsi pamoja na watendaji wa wizara, nasema tena kwamba ushauri na maelekezo ya Baraza hili ndio sababu kubwa ya wizara kupata mafanikio katika utekelezaji wa majukumu yetu. Naomba tuendelee kushirikiana ili tuweze kuwatumia uzuri wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo machache ya shukurani, sasa kwa heshima naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati yako ya Kudumu yaliyotolewa na wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2011/2012 kama hivi ifuatavyo.

Maagizo na Maoni ya Kamati niliyoletewa katika Wizara ya Ustawi wa Jamii yalikuwa ni tisa

Nikianza na nambari moja, wizara isimamie katika kuvihimiza vikundi vya ushirika hasa vile ambavyo vimo katika mchakato wa kufikia masharti ya kufaidika na msaada wa hisani kama vile msaada wa mfuko wa UN Habitant Pemba, kuwa na maeneo rasmi ya kufanyia kazi zao ili kuweza kutambulika kirahisi na washirika wa maendeleo.

Utekelezaji.
Wizara imechukua hatua na inaendelea kuchukua hatua za kuelimisha, kuvihimiza na kuvishajihisha vikundi vya ushirika vya wanawake na vijana. Aidha inavisaidia mbinu, utaalamu na utaratibu mzuri wa kuomba na kupata mikopo mbali mbali ikiwemo ya UN *Habitat* hasa Kisiwani Pemba ili vitambulike na wahisani na baadae vipate fursa za misaada kwa mikopo kwa madhumuni ya kuviendeleza na kupata maeneo ya kudumu ya kufanyia kazi zao.

Maelezo:
Kwa mikopo ya *UN Habitat* waliofanikiwa kupata msaada ni vikundi 6; 4 kutoka Pemba na 2 kutoka Unguja. Aidha tumeanzisha Vijana *SACCOS* mbili kubwa. Moja Unguja na moja Pemba kwa madhumuni ya kuwapatia mikopo vikundi vya vijana kutoka mfuko wa vijana ulioanzishwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la kukosa ofisi maalum za kuendeshea shughuli za vikundi vingi vya ushirika Pemba, vikiwemo vikundi vya Youth Centre Mbuzini na Selem Women Wete. Hivyo kamati inaagiza wizara kuvishajihisha vikundi hivyo kuanzisha ofisi rasmi za kazi zao ili kuleta ufanisi zaidi.

Utekelezaji:
Wizara imechukua hatua ya kuvishajihisha na kuvisaidia vikundi vya Youth Centre Mbuzini, Chake-Chake na Selem Women Wete. Kikundi cha Selem tayari wamepata jengo na wameshahamia katika jengo lao.

Maelezo:
Hatua za kuvihamasisha vikundi vyengine Unguja na Pemba inaendelea na hii ni kazi yetu ya kudumu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara ichukue juhudi za ziada kushajihisha wananchi ambao wameathiriwa na matatizo ya udhalilishaji wa watoto kijinsia, kuvitumia vituo vya mkono kwa mkono (*One Stop Center*) ili kuweza kupata huduma za ushauri.

Utekelezaji:
Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto imechukua na inaendelea kuchukua juhudi kubwa ya kuwaelimisha na kuwashajihisha wananchi na jamii kwa jumla katika mapambano dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia na watoto, uanzishwaji wa vituo vya mkono kwa mkono Unguja na Pemba ni moja katika juhudi na mikakati ya wizara ya kuandaa mazingira mazuri ya kuwasaidia waathirika wa vitendo vya udhalilishaji.

Tumeunda kamati ya kitaifa na za wilaya za uhifadhi wa mtoto kwa madhumuni ya kutoa taaluma na mwamko kwa jamii juu ya masuala ya udhalilishaji kwa watoto.

Maelezo:
Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto tayari ina vituo 4; Unguja 3 na 1 Pemba, pia ipo njiani kufungua chengine huko Pemba kwa lengo la wizara hii ni kufungua kituo kimoja katika kila wilaya, yaani kila wilaya tutahakikisha tunaweka kituo kimoja cha *One Stop Centre*.
Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha miradi maalum ambayo itasaidia kutoa huduma kwa jamii hasa watoto na wanawake katika vyuo vya mafunzo (Magereza).

Utekelezaji:
Wizara imelipokea suala la hilo na kwa kushirikiana na Vyuo vya Mafunzo itaangalia uwezekano wa kuanzisha miradi hiyo.

Maelezo;
Suala hili ni la mashirikiano na wizara nyengine linahitaji muda wa mazungumzo na uwezo wa kifedha. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ishauri kuendelea kupitiwa kwa sheria zote za makosa ya jinai na madai ili kuondokana na hali iliopo sasa ya kuwekwa mahabusu watoto na wanawake pamoja na vijana wengi kwa kutuhuma za makosa ambayo suluhu yake ingeweza kupatikana katika jamii.

Utekelezaji:
Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Shirika la Umoja wa Mataifa *UNICEF*, Wizara ya Katiba na Sheria kwa pamoja imeanza mikakati ambayo itaweza kushughulikia suala hili ili kuondosha tatizo la kuwaweka rumande vijana, watoto na wanawake kwa makosa ambayo yanaweza kutanzuliwa kupitia suluhu na ushauri nasaha.

Maelezo:
Tayari tumeanza na sheria ambayo ya Mahakama ya Kazi na mchakato wa kupitia sheria nyengine unaendelea.

Maagizo.
Kuna haja kwa wizara kuimarisha ushirikiano na Chuo cha Mafunzo kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki za watoto na wanawake na jamii kwa jumla zinalindwa kwa kuzingatia misingi ya haki za binadamu.

Utekelezaji:
Wizara tayari imetoa mafunzo ya uhifadhi ya mtoto kwa maafisa wa ngazi ya juu na ngazi ya chini ya Chuo cha Mafunzo ili kuelewa vizuri haki za mtoto na wanawake ili waweze kutekeleza wajibu wao vizuri. Pia kwa kushirikiana na Chuo cha Mafunzo tumeandaa mienendo ya kushughulikia ili kuingiza masuala ya uhifadhi ya mtoto kwa wafungwa. Vile vile wizara inayo kamati maalum inayotembelea Vyuo vya Mafunzo ili kuona mazingira wanayoishi watoto na wanawake katika Vyuo vya Mafunzo.

Kamati imebaini kuwa bado hakuna mwamko wa kutosha wa uanzishaji wa vikundi vya uzalishaji kiuchumi katika maeneo yenye watoto na wenye mazingira magumu. Kamati inatoa rai kwa wizara kwa kushirikiana na wawezeshaji wa wananchi kiuchumi, kuelimisha akinamama ili waweze kuunda vikundi vya uzalishaji ili viweze kuwasaidia katika kukabiliana na hali ngumu ya maisha katika maeneo yao.

Utekelezaji;
Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto inayo mashirikiano mazuri na maelewano na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika katika suala zima la kuwawezesha wanawake wa vikundi vya uzalishaji mali.

Aidha tunayo mipango ya kusaidia na kuhamasisha uanzishaji wa miradi katika maeneo yenye watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Mafunzo kwa wana vikundi vya wanawake yanatolewa mara kwa mara kwa madhumuni ya kuwashajihisha na kuwajengea uwezo wanawake wengi walio vijijini kupitia maafisa wetu wa wilaya.

Maelezo:
Mafanikio mazuri yamepatikana na akinamama wameonesha juhudi kubwa katika harakati za kujinasua na hali ngumu ya kupato kukidhi maisha yao ya kila siku. Kuna umuhimu wa wizara kuwa na mashirikiano na Wizara ya Biashara na Viwanda kuanzisha maonesho ya Kimataifa ya wajasiria mali hasa ya vikundi vya uzalishaji vya bidhaa mbali mbali kwa lengo la kusaidia vikundi hivyo, kuwapatia soko na hata kuweza kujitangaza.

Utekelezaji:
Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto inashirikiana vizuri na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kuhakikisha vikundi vya uzalishaji mali vinashiriki kikamilifu katika fursa za maonesho mbali mbali, ikiwemo maonesho ya saba saba ambayo yanafanyika kila mwaka mjini Dar es Salaam.

Aidha tumeanzisha soko la Jumapili (*Sunday Market*) huko Pemba ili kuwapatia wajasiria mali soko la kuuza bidhaa zao.

Maelezo:
Mafanikio makubwa yamepatikana kwa wajasiria mali wanaoshiriki katika maonesho mbali mbali, wameweza kuzifanya bidhaa zao kuwa bora katika masoko wanayopeleka.

Kamati inashauri serikali kuharakisha ujenzi wa jengo la kudumu la ofisi za Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto Pemba ili kuepuka kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kuendelea kutumia majengo ya kukodi.

Utekelezaji:
Maandalizi ya ujenzi wa ofisi ya pamoja kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji kwa Wananchi Kiuchumi na Ushirika yameanza huko Pemba Gombani. Hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kuteuliwa kwa mhandisi yaani Mhandisi muelekezi (*Consultant Engineer*) na hatua za michoro ya majengo inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kutoa shukurani na kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi tena ya kukutana kuendeleza shughuli zetu. Na pia kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa wa Baraza lako tukufu, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako taarifa fupi ya utekelezaji wa maagizo yanayotokana na ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kwako. Nimepata bahati kwako umekaa wewe mwenyekiti. Na pia naomba nitoe shukurani kwa Baraza lako tukufu na hasa kwa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mashirikiano makubwa wanayoipatia Wizara ya Afya katika kutekeleza majukumu tuliyopewa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya katika ripoti ya 2011/2012 iliagizwa kutekeleza mambo manne na kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba kuyatolewa maagizo ya utekelezaji kwa ufupi.

La kwanza lilikuwa ni kuharakisha kuanza kwa jengo la Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali iliopo Maruhubi.

Utekelezaji:
Hadi kufikia sasa jengo limeshafanyiwa ukarabati wa kuezekwa, kueka milango na madirisha, kutia umeme na dari na jumla ya fedha zilizotumika ni milioni sabini. Kwa Pemba kiwanja kwa ajili ya maabara ya Mkemia Mkuu ya Serikali kimepatikana na hatua za kutayarisha mchoro zinaendelea.

Aidha kuna mpango wa ujenzi wa jengo kubwa na hatua iliyofikiwa ni pamoja na kufanya makisio ya gharama za ujenzi wake. Hatua za kupeleka mradi huo kutafuta wafadhili umeshafanyika na wasaa Mungu tunaweza tukampata mfadhili akatusaidia akashirikiana na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ilikuwa ni kufuatilia na kuzitafutia ufumbuzi wa changamoto za msingi zinazozikabili hospitali nyingi za wilaya na vijiji Unguja na Pemba ili kusaidia upatikanaji wa huduma za msingi za afya katika maeneo hayo kama vile uhaba wa maji safi na salama, wafanyakazi na vifaa.

Utekelezaji:
Katika kutatua changamoto ziliomo katika vituo na hospitali, wizara kwa upande wa uhaba wa wafanyakazi kwa mwaka 2011/2012, Wizara ya Afya iliomba kuidhinishiwa nafasi mpya za wataalamu mbali mbali wa kada za afya na nyenginezo. Jumla ya nafasi zilizoidhinishwa zilikuwa ni mia nne na kumi na nane na kuanzia mwezi wa saba mpaka mwezi wa nne 2012 tuliajiri vijana arobaini na tisa na nafasi zilizobaki zilikuwa mia tatu sitini na tisa. Miongoni mwa nafasi zilizobaki kufuatia tarehe 1 mwezi 10 mpaka mwezi wa 2012 Tume ya Utumishi Serikalini imetupa kibali cha kuajiri vijana mia na tisini na mbili kutoka vyuo mbali mbali na wengine kutoka Chuo cha Taaluma ya Afya ya Mbweni.

Waajiriwa wote hawa ni wa kada tofauti za afya. Aidha Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika mwaka 2012/2013, iliidhinisha pia nafasi mpya za ajira mia nane na kumi na sita katika kada tofauti za afya na zisizo za afya baada ya kuzingatia mahitaji halisi yaliopo katika Wizara ya Afya.

Kutokana na mahitaji ya wafanyakazi katika Wizara ya Afya, ofisi hiyo husika kwa kuanzia imeturuhusu kuajiri nafasi kumi na nne miongoni mwa mia nane na kumi na sita za ajira kwa awamu ya kwanza. Na hawa vijana wameshafikishwa katika *GSO* yaani katika wanaita kuwahakiki na tunasubiri matokeo yao ili tuwaajiri.

Mhe. Mwenyekiti, la tatu wizara ilitakiwa kuzingatia upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa wa akili ili ziweze kusaidia matibabu kwa wagonjwa hao. Mhe. Mwenyekiti, wizara imeshaandaa mfumo ambao unaitwa *Framework Contract* kwa ajili ya kumpata mletaji dawa

kwa mwaka mzima. Serikali ya SMZ imeahidi kutenga shilingi zisizopungua bilioni mbili kila mwaka kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Wizara imeanzisha mfumo mpya wa mahitaji ya dawa kutokana na vituo vya afya, kutoka mfumo wa *Push Sytem* na kwenda *Pull System*. Mfumo ambao kwa Kiswahili ni kwamba dawa zitakuwa huwa zinapelekwa vituoni kwa mujibu wa mahitaji sio kuwapelekea bila ya kuhitaji.

Aidha wizara imepata bahati kupokea msaada wa dawa kutoka kwa washirika wa maendeleo wenye thamani ya bilioni moja laki sita sabini na nne elfu, mia mbili na thamanini na hamsini na mbili kutoka shirika moja lisilokuwa la kiserikali linaloitwa *Project Hope*, na serikali kwa upande wake imetenga shilingi bilioni moja na milioni nne na sitini kwa kipindi cha kuanzia mwezi wa Julai hadi Juni, 2011/2012. Jumla ya shilingi mia tano thamanini na nne, mia tisa na arobaini na tatu na mia tano zimepatikana kupitia serikalini na shilingi milioni thamanini na mbili, mia mbili na arobaini na tatu zimepatikana kupitia msaada wa *DANIDA*. Hivyo hali ya dawa katika hospitali hivi sasa sio mbaya kama vile ilivyokuwa zamani.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa inashirikiana na Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya katika kukipatia ruzuku chuo hicho kama vinavyopatiwa vyuo vyengine.

Utekelezaji:
Wizara imeshawasiliana na Wizara ya Fedha juu ya upatikanaji wa ruzuku na tayari kuanzia mwezi wa Agosti mwaka 2012, chuo kimeanza kupata ruzuku hiyo. Kwa kipindi cha robo tatu kuanzia 2012 Machi mpaka 2013 jumla ya shilingi milioni mia na arobaini na mbili laki tatu na sitini zimepatikana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Wizara ya Elimu na Mafunzo na Amali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mimi na sote tuliopo hapa uzima na afya njema tukaweza kuhudhuria na kushiriki katika kazi ambazo tumejipangia.

Lakini la pili ninakushuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii adhimu na adimu kutoa maelezo yangu mafupi katika Baraza lako tukufu iliyotoa maagizo matano ya wizara yangu katika mwaka wa fedha 2011/2012.
Lakini la tatu ninapenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake wote kwa kazi nzuri walioifanya katika kipindi chote ambacho wao wapo, maelekezo waliyotoa na changamoto waliosaidia kutatua kutokana na umahiri wao na uhodari wao. Ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza wale wote.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imepata maagiza matano ambayo naomba sasa kuyatolea ufafanuzi.

La kwanza ni kwamba wizara ihakikishe kuwa ujenzi wa Skuli ya Paje Mtule, Tunguu na Dimani inayofanywa na Kampuni ya *Electric Engineering* ya Dar es Salaam unakuwa kwa viwango vilivyokusudiwa na unamalizika kwa wakati.

Pili wizara imeagizwa kutumia busara ili mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao wameajiriwa katika taasisi za serikali iweze kurejeshwa. Deni la shilingi bilioni nane ni kubwa na linaathiri maendeleo ya bodi.

Tatu, wizara imeagizwa bajeti ya mwaka 2012/2013 kuhakikisha kuwa inaingiza ada ya skuli, ada ya shilingi milioni tatu ya wanafunzi wa kidato cha nne wanaofanya mitihani kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa dawa hizo.

Nne, wizara imeagizwa kuzihamisha ofisi ya Bodi ya Upimaji na Tathmini katika ofisi zake kutokana na jengo lake kutolewa taarifa rasmi ya ubovu wake na Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Na la tano, wizara imetakiwa kufuatilia kwa karibu matatizo yaliyoikabili Skuli ya Ufundi ya Kengeja yakiwemo hali ya mfumo wa maji machafu, upungufu wa walimu na mafundi, upungufu wa walimu katika Idara ya Umeme, uhaba wa mabweni pamoja na huduma za afya.
Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imeyafanyia kazi maagizo hayo na sasa ninapenda kukiri kuwa baadhi ya maagizo hayo hayajatafutiwa ufumbuzi kamili lakini yapo maagizo ambayo yameshafumbuliwa.

Utekelezaji halisi ni kama hivi ifuatavyo:
Taarifa ya utekelezaji wa yaliyotokana na ripoti ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2011/2012.

Agizo:
Licha ya kuwepo hali isiyoridhisha na ucheleweshaji wa ujenzi unaoendelea wa mradi wa skuli za sekondari za Paje Mtule, Tunguu na Dimani, wizara ihakikishe kuwa ujenzi wa skuli unaendeshwa na kampuni ya *Electronic International Company Limited* ya Dar Es Salaam unakuwa kwa kiwango kilichowekwa na kuzingatiwa ipasavyo.

Utekelezaji:
Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa kazi hii ulitiwa saini tarehe 29 Julai 2010 na ujenzi ulitarajiwa kukamilika wiki 42 ambazo zimekamilika tarehe 26 Agosti, 2011. Mkandarasi ameshindwa kukamilisha kazi, licha ya kuongezewa muda wa ujenzi. Mara ya mwisho Mkandarasi alitoa ahadi mbele ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, kukamilisha ujenzi itakapofika tarehe 28 Februari, 2013, lakini ameshindwa kukamilisha kazi hiyo.

Kazi ya ujenzi imefikia asilimia 90, ujenzi umesimamiwa na mshauri wa ujenzi Kampuni ya *Hydro Plan* ya Ujerumani, ikishirikiana na Kampuni ya *Matro Consult* ya Tanzania na pia wahandisi wa wizara yangu. Kazi zilizofanyika ni kufunga kwa shata za milango, utiaji *tiles*, sakafu, kupaka rangi, kuunga umeme, maji na kazi za nje.

Maelezo:
Kutokana na mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati, hivi sasa mkandarasi anakatwa malipo ya fidia, yaani *dequidated damages*, ambapo kwa kila siku anapochelewa kufanya kazi, anakatwa fidia ya asilimia 0.1 *percent* ya gharama za mkataba wake hadi kufikia asilimia 10 ya gharama hiyo. Hadi sasa mkandarasi ameshakatwa fidia ya shilingi milioni 45,855,103. Mkataba na mkandarasi utavunjwa ifikapo tarehe 9 Juni, 2013, ikiwa mkandarasi huyo hakuweza kukamilisha kazi iliyobakia.

Agizo la Pili. Kamati inaiagiza wizara kutumia busara ili mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ambao waajiriwa katika sekta ya serikali iweze kurejesha mkopo huo. Deni la shilingi bilioni 8 kwa waliokopa ni kubwa na linaathiri mwenendo wa bodi.

Utekelezaji:
Jumla ya deni wanaodaiwa wanafunzi ambao wameshamaliza masomo yao ya juu ya mwaka 2006 au baina ya mwaka 2006 hadi 2012 ni shilingi bilioni 4. Hadi mwezi Machi, 2013 wanafunzi 1,564 waliopewa udhamini na bodi ya mkopo wamemaliza masomo yao. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Idara ya Vitambulisho vya Zanzibar zimeweza kuwatambua wanafunzi waliopatiwa mkopo kupitia bodi yetu ya mkopo.

Pia kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kuwatambua vijana waliopatiwa mkopo huo ambao bado hawajalipa.

Maelezo:
Hadi sasa watahiniwa 257 wanalipa madeni yao na wahitimu wanne wameshamaliza kulipa kabisa. Hadi sasa jumla ya shilingi milioni 78 zimekwishakusanywa kutokana na madeni hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya bajeti nilisema Wizara imeshakusanya shilingi milioni 4. Lakini kwa juhudi zilizochukuliwa na kwa kushirikiana na wenzangu, tumeweza sasa kukusanya shilingi 78 milioni na kazi ya kuwatambua vijana wetu bado inaendelea. Bado wapo vijana wengi waliomaliza masomo ambao hawajapata ajira na hivyo hawana uwezo wa kulipa mkopo huo. Pia bodi imefuatilia wakopaji wanaoajiriwa na sekta binafsi na hadi sasa inafanya uchambuzi wa majina 300 ya waajiriwa wa sekta binafsi ili kuwatambua waliokopeshwa na bodi hiyo. Juhudi zinachukuliwa kukutana na wadhamini wa wakopaji ili kuhakikisha wadhamini hao wanasaidia kukusanya malipo.

Agizo laTatu. Kamati inaagiza Wizara katika bajeti ya mwaka 2012/2013 kuhakikisha kuwa inaingiza ada ya shilingi milioni 3 kwa watahiniwa wa kidatu cha nne kwa lengo la kuhakikisha ulipaji wa ada unatekelezwa.

Malengo na Utekelezaji:
Ni kweli kabisa kwamba katika mwaka wa fedha 2011/2012 wizara ilishindwa kulipa madeni ya mitihani ya Tanzania. Deni la ada la watahiniwa wa kidatu cha nne lenye jumla ya shilingi milioni 434,490,000. Hii inatokana na uhaba wa fedha za bajeti zilizotengwa katika bajeti iliyopita, nayo ilikuwa ni jumla ya shilingi bilioni 1,382 milioni ambapo ingawa zilipatikana kwa asilimia 100, lakini bado hazikukidhi malipo ya Baraza.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza la Mitihani la Zanzibar limepangiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 1,500 milioni, matumizi ya Baraza kwa mwaka huu yamekisiwa kufikia shilingi bilioni 1, na kubakia milioni 500 ambazo zitatosha kulipia deni la mitihani kwa mwaka 2011/2012 tu. Hata hivyo, bado wizara inakabiliwa na deni la watahiniwa wa kidatu cha nne kwa mwaka 2012/2013 ambalo ni jumla ya shilingi milioni 434,465,000.

Katika kipindi hiki deni lililobakia ni shilingi milioni 79, hivyo kufanya deni lote la mtihani wa kidato cha nne kufika shilingi milioni 789,630,454.

Agizo la Nne**.** Kwa kuwa jengo linaloendelea kutumiwa na Ofisi ya Bodi ya Upimaji na tathmini, sasa bodi hii inaitwa Bodi ya Mikopo. Imetolewa taarifa na Mamlaka ya Mji Mkongwe kuwa haifai kwa ajili ya matumizi ya ofisi kutokana na hali mbaya ya ubovu na uchakavu wa jengo hilo.

Kamati inaagiza ofisi ya bodi zihamishwe na kutafutiwa sehemu nyengine, ili kulinda usalama wa wafanyakazi wake.

Utekelezaji:
Wizara inakiri, jengo lililokuwa Ofisi ya Bodi ya Upimaji na Tathmini, kwa sasa ni Baraza la Mitihani la Zanzibar ni bovu. Juhudi za kutafuta jengo jengine kwa ajili ya kuwahamisha maofisa waliomo humo inachukuliwa, lakini bado hazijafanikiwa. Tunatarajia Ofisi ya Baraza la Mitihani la Zanzibar kuhamia katika jengo la Ofisi ya Shirika la Bima la Zanzibar, hapo Shirika la Bima litakapohama mapema iwezekanavyo.

Maelezo:
Mazungumzo yanaendelea na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya kulitaka Shirika la Bima la Zanzibar, wahame katika jengo hilo baada ya kufunguliwa rasmi kwa jengo hilo jipya.

Tano, Kamati imetaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Samahani Mhe. Mwenyekiti, kufuatilia kwa karibu matatizo yanayokabili skuli ya sekondari ya ufundi ya Kengeja ya kuwemo hali mbaya, hali ya mfumo wa maji machafu, upungufu wa walimu wa ufundi katika idara ya umeme na uhaba wa dakhalia pamoja na huduma za afya.

Utekelezaji:
Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2011/2012 wizara ilifanikiwa kukamilisha ujenzi wa madarasa manne mapya ya skuli ya sekondari ya ufundi Kengeja, pamoja na thamani ya madarasa hayo. Pia jengo lenye ukumbi wa chakula ambalo wanafunzi walikuwa wanatumia kwa ajili ya kulala, nalo limetengenezwa dari, milango, kupakwa rangi na kuwekewa mafeni.

Vile vile mfumo wa maji machafu umefanyiwa matengenezo makubwa na sasa hauna matatizo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, wizara imetengewa jumla ya shilingi milioni 400 katika bajeti ya maendeleo ya mradi wa urekebishaji wa elimu na ufundi. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 100 zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa vya karakana ya umeme na shilingi milioni 200 zimetengwa kwa kuanzia ujenzi wa jengo jipya la dakhalia.

Maelezo:
Zabuni ya ununuzi wa vifaa vya Karakana ya umeme imetangazwa na muombaji wa zabuni amejitokeza na maombi kufunguliwa. Hivi sasa tathmini ya maombi ya wazabuni yanafanyiwa tathmini kabla ya kumchagua mzabuni aliyestahiki kuchaguliwa.

Kazi ya ujenzi wa dakhalia haijafanyika kutokana na ukosefu wa fedha. Hadi sasa ni shilingi milioni 50 tu ndizo zilizopatikana. Hivi karibuni wizara imepata kibali cha ujenzi wa awamu ya pili ya fani ya umeme kwa ajili ya skuli ya Sekondari ya Kengeja. Taratibu za uajiri zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha.

TAARIFA ZA KAMATI

Mhe. Hija Hassan Hija: (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru. Naomba kusoma Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumkushuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, nikiwa mzima wa afya ili kuwasilisha Muhtasari wa Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii, kwani bila ya ruhusa yako nisingekuwa na jeuri hii.

Mhe. Mwenyekiti, Shukrani zangu pia ziwafikie Wajumbe wa Kamati, watendaji wa Wizara ya Afya,Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mashirikiano yao makubwa mbele ya Kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, ni vyema kuwatambua Wajumbe wa Kamati ambao walihusika katika kazi za Kamati kama ifuatavyo.

1.	Mhe.Amina Iddi Mabrouk	Mwenyekiti
2.	Mhe Hija Hassan Hija	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe.Asha Abdu Haji	Mjumbe
4.	Mhe Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5.	Mhe Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
6.	Mhe Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7.	Mhe Nassor Salim Ali	Mjumbe
8.	Mhe Saleh Nassor Juma	Mjumbe
9.	Nd. Talib Enzi Talib	Katibu
10.	Nd. Asha Said Mohamed	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 106(e) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2012. Majukumu ya Kamati yameelezwa katika kanuni ya 112 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi, miongoni mwa majukumu yake ya msingi ni kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika, kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa bajeti na hotuba nyengine za mawaziri husika.

Aidha kufuatilia mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa na miradi ya wananchi iliyo chini ya Wizara husika, pamoja na kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali kwa wizara husika ambazo kwa upande wa Kamati yetu inasimamia Wizara

ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Kamati yetu iliweza kutekeleza majukumu hayo niliyoyataja katika kipindi cha wiki sita. Kwa upande wa Unguja ilifanya kazi wiki mbili, kuanzia tarehe 11/09/2012 hadi tarehe 21/09/2012 Kwa upande wa Pemba ilifanya kazi wiki mbili kuanzia tarehe 10/12/2012 hadi 21/12/2012. Aidha, Kamati ilimalizia kazi zake wiki mbili kwa upande wa Unguja kuanzia tarehe 04/03/2012 hadi 15/03/2013.

Baada ya utangulizi huo naomba nianze na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inaipongeza Wizara kuweza kutekeleza malengo yake iliyojipangia katika vipindi vya kota mbili za mwanzo za Julai /Disemba katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 licha ya kuwa na changamoto ya muda mrefu ya ufinyu wa bajeti yake.

Kamati inaipongeza Wizara kwa utendaji wake na ushirikiano mzuri iliotoa kwa kipindi chote ambacho Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ilitekeleza kazi zake hadi kipindi hiki ambacho Kamati zinatarajia kuvunjwa na kuundwa tena kwa mujibu wa utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi Jamii imeridhika na utekelezaji wa Wizara wa maagizo ya mwaka wa fedha uliopita (2011/2012) kama ilivyoelezwa; kwa kuwa Kamati yetu imefuatilia utekelezaji huo na kuona ufanisi wake mkubwa.

Utekelezaji wa malengo mengine ya Wizara.

Malipo ya fidia za wafanyakazi

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Ustawi wa Jamii imekuwa na deni kubwa la muda mrefu la zaidi ya shilingi milioni 98,745,723 kwa ajili ya fidia ya wafanyakazi waliopata ajali kazini ambapo inashindwa kulilipa. Kamati imeona kwamba kuendelea kuachiwa Wizara mzigo mkubwa wa malipo ya deni hilo ni tatizo hasa ukizingatia ufinyu wa bajeti yake. Kamati imeona kuwa malipo hayo ya fidia za wafanyakazi yarejee Hazina na kwamba Wizara ya Fedha na Mipango ya Maendeleo isimamie malipo ya deni hilo.

Udhalilishaji wa Watoto na Wanawake kijinsia

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imebaini kuwa bado tatizo la udhalilishaji watoto kijinsia linaendelea katika visiwa vyetu. Kamati imekuwa ikiishauri serikali mara kadhaa juu ya namna ya udhibiti wa tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa Wizara inaendelea na mchakato wa kufanya utafiti elekezi ili kujua ukubwa wa tatizo na kutafuta mbinu za kupunguza na hatimae kulitokomeza kabisa tatizo la udhalilishaji wa kijinsia na ubakaji. Kamati inaunga mkono wazo la wizara kuwa tatizo hilo litangazwe kuwa ni janga la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliunda Kamati maalum kufuatilia masuala ya udhalilishaji wa watoto,Kamati yetu inasisitiza kwa mara nyingine ni vyema Kamati hiyo ingeleta ripoti yake mbele ya Baraza lako tukufu ili angalau jamii iweze kuelewa namna ya serikali yao inavyolifuatilia kwa karibu suala hilo. Wananchi wengi wamekuwa wakipoteza imani juu ya ufuatiliaji wa udhalilishaji wa watoto hasa katika suala la kupatikana kwa ushahidi. Watoto wanaendelea kudhalilishwa kwa kubakwa na kufanyiwa vitendo vya kinyama vinavyowasababishia madhara makubwa katika ustawi wao.

Kuanzisha Mabaraza ya Watoto Vijijini

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kusimamia uundwaji wa mabaraza ya watoto yapatayo 110 katika Wilaya tatu za Unguja (Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Kusini Unguja). Tunasisitiza juhudi hizo pia ziendelezwe kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzisha mabaraza ya watoto vijijini na kuwajengea uwezo wa kujitambua na kuelewa haki zao za msingi kutasaidia kudhibiti na kupiga vita udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto hao. Aidha, itasaidia katika kuwaweka pamoja na kuibua matatizo yanayowakabili siku hadi siku katika familia na jamii kwa ujumla.

Tatizo la Ajira ya Watoto

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la ajira ya watoto kwa kiwango kikubwa katika maeneo mbali mbali kwa mfano ya Mwambe na maeneo mengine Pemba. Baadhi ya wafanyabiasha wa shughuli za ujenzi wamekuwa wakiwatumikisha watoto katika kazi za uvunjaji wa kokoto katika sehemu hiyo. Aidha, wazazi wenyewe nao huchangia katika kuwashirikisha watoto kutenda shughuli hizo. Kamati inaishauri Wizara kuimarisha miongozo madhubuti ya kisheria dhidi ya udhalilishaji wa watoto ili kusaidia kuondokana na tatizo hilo.

Kuongezeka kwa Tatizo la Ombaomba

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu imesikitishwa na taarifa ya serikali kupitia wizara yake ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu kuongezeka kwa omba omba nchini.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo matokeo ya utafiti yameonesha kwamba Zanzibar kuna omba omba karibu kila eneo ambao wengi wapo katika maeneo ya mijini yenye shughuli nyingi za kiuchumi. Asilimia 86.25 ya omba omba ni wenye umri kati ya mika 40 na 60 ambapo asilimia 65 ni wanawake na asilimia 35 ni wanaume.

Mhe. Mwenyekiti, sababu kuu za uombaji zimeelezwa kuwa ni pamoja na kwamba wengi wamo katika mazingira magumu na hawana elimu wala ajira. Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeona huko tunakoelekea hili ni tatizo na ni aibu. Rai ya Kamati kwanza, omba omba idhibitiwe na kwa kuwa hali za wananchi kiuchumi zimekuwa si nzuri kuna haja kwa serikali kutafua njia endelevu na mbadala za kuisaidia jamii kiuchumi.

Aidha Kamati yetu inahimiza ukamilishaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar ili kusaidia kupunguza ugumu wa maisha kwa jamii zinazoishi katika mazingira magumu na umasikini, hasa wazee.

Utekelezaji wa Mradi wa Kilimo cha Maua ya Rozela na mboga mboga katika Shamba la Tunguu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono juhudi za Wizara kushajihisha vijana kulima kilimo cha maua na mboga mboga ili kuweza kujiajiri. Kwa kuwa Mradi huu umekuwa ukipatiwa fedha nyingi katika kuuendeleza, Kamati inaiagiza Wizara kufanya tathmini juu ya faida ipatikanayo kutokana na Mradi wa mboga mboga na Maua ya Rozela unaoendeshwa na kikundi cha vijana cha *ZASOSE* katika shamba la Tunguu.

Kuhusu Watoto Wanaoishi Katika Mazingira Magumu zaidi

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mambo yanayochangia kuwepo kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ni kukosekana kwa huduma muhimu za kijamii ikiwemo huduma za afya. Kamati itahakikisha inashirikiana na Wizara ya Afya ili huduma za afya ziweze kufikishwa katika maeneo yaliyoathirika kutokana na kutowepo kwa huduma hiyo.

Kamati imebaini kuwa bado hakuna muamko wa kutosha wa uanzishwaji wa vikundi vya uzalishaji vya kiuchumi katika maeneo yenye watoto wenye mazingira magumu zaidi. Kamati inatoa rai kwa Wizara kushirikiana na wizara ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kuelimisha kinamama ili waweze kuunda vikundi vya uzalishaji ili viweze kuwasaidia katika kukabiliana na hali ngumu ya maisha katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza wizara kwa ubunifu wa kuanzisha Mpango maalum wa mikopo kwa vijana kwa kushirikiana na benki ya *CRDB*. Hatua hii imesaidia katika kuvijengea uwezo wa kiuchumi vikundi mbali mbali vya kiuchumi nchini. Vikundi hivyo vimeweza kuunda *SACCOS* moja ya Zanzibar vijana *SACCOS* itakayotoa mikopo kwa wafanyabiashara na wazalishaji wadogo.

Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii Pemba

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yetu ya Ustawi wa Jamii inakabiliwa na tatizo la ofisi ya kudumu Pemba. Serikali imekuwa ikitumia gharama za shilingi milioni 18 kwa mwaka kwa ajili ya kodi za afisi hiyo. Kuendelea kutumia gharama kubwa kwa ajili ya kodi si busara. Kamati yetu inashauri kwamba ikiwa mpango wa ujenzi wa ofisi hizo kwa upande wa Pemba bado haujakaa sawa, serikali iharakishe zoezi la kuhakiki mali zake ikiwemo majengo ili kusaidia kupatikana kwa majengo yake.

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

Hali ya Mapato:

Mhe. Mwenyekiti, wizara katika mwaka wa fedha 2012/2013 ilikadiriwa kukusanya shilingi 22,500,000 kupitia vyanzo vya ada za leseni za walimu na usajili wa skuli za binafsi na kuziwasilisha hazina.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia mwezi Disemba, makusanyo ya mapato yamepanda na kufikia shilingi 4.7 ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita ambapo yalikuwa katika kiwango cha shilingi 3.4. Hata hivyo, makusanyo hayo ni madogo ukilinganisha na makadirio ya mapato ya jumla ya bajeti ya wizara. Kamati imeiagiza ada za leseni za ualimu na usajili wa skuli binafsi ziongezwe.

Kuhusu Matokeo ya Mitihani ya Kidato cha Nne ya Mwaka 2012:

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imesikitishwa na matokeo mabaya sana ya mitihani ya kidato cha nne ya hivi karibuni. Mhe. Mwenyekiti, sisi kipindi kirefu utakumbuka jamii ilishuhudia kufutwa kwa matokeo ya mitihani ya kidato cha nne kutokana na kubainika kuwepo kwa udanganyifu katika mitihani hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaona kuwa hali hiyo inaweza ikawa ni miongoni mwa viashiria vya kushuka kwa kiwango cha elimu nchini. Kamati yetu kupitia taasisi na wadau tofauti wa sekta ya elimu imeweza kubaini mapungufu mbali mbali katika mfumo wa elimu uliopo, ambayo kwa namna moja au nyengine yamechangia katika kufeli kwa wanafunzi wengi katika mitihani hiyo.

- Udhaifu wa usimamiaji na uongozi katika ngazi ya skuli kama ngazi za juu za Wilaya na Mkoa,
- Ufaulu wa chini wa wanafunzi katika madarasa ya chini na baadhi ya masomo;
- Ufundishaji usiokidhi matakwa kama kutosomeshwa mtoto silabasi inayohitajika kikamilifu kwa muda uliopangwa au kukosa mbinu za kujibu masuali ya mitihani;
- Pia kuwepo kwa maamuzi mengi ya kielimu yasiyo sahihi yanayowekwa kutokana tu na mielekeo na mitazamo ya kisiasa;
- Aidha kutotekelezwa ipasavyo kwa Sera na Sheria ya Elimu ya Zanzibar. Pamoja na kuwa na miaka 8 ya kuwepo kwake sehemu kubwa ya sera hiyo haijatekelezwa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri kurudishwa kwa elimu mikononi mwa umma. Jamii yenyewe haijaamka kudai kusimamia elimu. Wenzetu Bara kwa mfano, wana taasisi zinazojihusisha na elimu kama Hakielimu, Twaweza, na kadhalika. Nini kifanyike? Sheria ya Elimu ifanyiwe mapitio.

Aidha kamati inaona kuwe na skuli zilizo katika mazingira ya kufundishika. Kwa mfano, mwaka jana kamati ililazimika kuifunga Banda la Skuli ya Kengeja baada kuona majengo yanahatarisha maisha ya watoto, la kupongeza wizara ilithamini agizo la Kamati na kuchukua hatua haraka. Vile vile hivi juzi kamati ililazimika kulifunga Banda la Skuli ya Kitogani baada ya kutishia

usalama wa wanafunzi ni mategemeo ya kamati, wizara itachukua hatua kama ilivyochukua hatua za haraka Kengeja, ili kurekebisha hali hiyo.

Skuli nyingi ziko katika hali si nzuri, hazina vifaa na wakati mwengine hata walimu. Kumekuwa na maendeleo makubwa ya ujenzi wa mabanda ya skuli, lakini hili halimuhakikishii mtoto kupata elimu. Kwa mfano ujenzi wa skuli za sekondari za wilaya zilitegemewa kuondosha usumbufu wa upatikanaji wa elimu ya sekondari kila wilaya lakini kinyume chake ni kitendawili kwamba majengo yapo lakini yamekosa wanafunzi, walimu na vifaa sambamba na kutowepo kwa dakhalia.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja kwa serikali kuinua hadhi na heshima ya elimu na ualimu uliopoteza muelekeo, hadhi na heshima yake na hauna tena mvuto kwa vijana. Hilo ni tatizo katika kukuza sekta ya elimu nchini.

Jambo la msingi Mhe. Mwenyekiti, kamati inaendelea kuisisitiza serikali kuongeza bajeti ya elimu. Maendeleo ya nchi ni kuwekeza katika sekta ya elimu, afya na ustawi wa watu.

Hata hivyo, wizara isiridhike na kusubiri matokeo ya utafiti unaofanywa na Tume maalum ya serikali ya SMT, ili kubaini tatizo linaloendelea kukua mwaka hadi mwaka la kushuka viwango vya ufaulu. Mhe. Mwenyekiti, kuna haja na SMZ iendeshe utafiti wake hii ni kutokana na sababu ya msingi kwamba tunatafautiana katika baadhi ya maeneo katika mfumo wetu wa elimu kati ya SMZ na SMT.

Aidha katika mitihani ya kidato cha sita iliyofanyika Februari 2013, kulijitokeza mgongano kati ya Baraza la Mitihani na Wizara ya Elimu Zanzibar juu ya sifa za wanafunzi wa kufanya mtihani wa kidato cha sita. Baraza la Mitihani walitangaza wazi kwamba sifa za kufanya mtihani kwa wanafunzi husika ni lazima wawe na pasi tano (*credit* 5), jambo ambalo kwa Zanzibar hakukua na matayarisho hayo, hatua ambayo ilileta taharuki kubwa kwa wanafunzi.

Hata hivyo, Wizara ya Elimu Zanzibar iliingilia kati na kuliomba Baraza kuwaruhusu wanafunzi kufanya mitihani chini ya kiwango hicho na Baraza kukubali ombi hilo la Wizara. Je kamati inajiuliza kukubali huko kwa Baraza la mitihani kuwaruhusu wanafunzi kufanya mitihani chini ya sifa walizotangaza ni kwa nia safi au ujanja?

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaishauri wizara kukaa na Baraza la Mitihani mapema ili kuwa na msimamo wa pamoja ili kuondosha usumbufu kwa wanafunzi wa mwaka ujao.

Mradi wa Ujenzi wa Skuli za Sekondari za Paje-Mtule, Tunguu na Dimani:

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu haikuridhika na utekelezaji wa mradi wa ujenzi huo. Kipindi kilichopita tuliiagiza wizara ihakikishe kuwa ujenzi wa skuli hizo unaoendeshwa na kampuni ya *Electric International Limited* ya Dar-es –Salaam, unakuwa na viwango vilivyokusudiwa na unazingatia wakati kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba uliopo.

Kamati ilipotembelea tena hivi karibuni imegundua hakuna hatua zilizochukuliwa. Aidha Kamati iliambiwa kuwa viongozi wa kitaifa mara kadhaa wamekuwa wakipewa ahadi za kukamilisha ujenzi huo kwa viwango, jambo la kusikitisha hakuna hatua iliyochukuliwa na kampuni hiyo.

Kamati inaishauri wizara kuangalia haja ya kusitisha mara moja mkataba husika katika Mradi wa Ujenzi wa Skuli za Sekondari za Paje-Mtule, Tunguu na Dimani, ifanye hivyo na taratibu nyengine zifuatwe, ili kuepuka ucheleweshwaji mkubwa wa ujenzi wa skuli hizo pamoja na kuepuka gharama kwa taifa.

Mradi wa Ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua nzuri iliyofikiwa ya Mradi wa Ujenzi wa Kampasi ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa Pemba. Hata hivyo, inaishauri serikali kuanzisha skuli ya mazoezi (maandalizi na msingi) ndani ya chuo hicho, ili kurahisisha upatikanaji wa mafunzo ya vitendo kwa walimu.

Aidha Kampuni ya *Quality Building* inayojenga chuo hicho imeonesha umakini na ufanisi mkubwa na hii imeishawishi kamati kusema kuwa kampuni hii na nyengine za kizalendo ndizo za kupewa kazi mbali mbali badala ya kuzipa kampuni za nje ambazo zina ubabaishaji. *(Makofi)*

Mradi wa Ujenzi wa Maktaba Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ni muhimu kwa kweli ni wa muda mrefu na haujakua na maendeleo. Urasimu katika ukamilishaji wa taratibu za matumizi sambamba na uingizwaji mdogo wa fedha unapelekea kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo. Mradi unahitaji zaidi ya shilingi bilioni moja, lakini fedha zilizotengwa na wizara ni milioni 200 ambapo hadi sasa fedha zilizoingizwa ni chini ya asilimia 40.

Skuli za Maandalizi:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri wizara kuwepo kwa Mtaala mmoja kwa Skuli zote za Maandalizi zikiwemo Binafsi na Serikali, ili kuwepo na uwiano wa elimu hiyo. Idara husika isimamie ipasavyo kuidhibiti mitaala hiyo iweze kutumika katika skuli hizo.

Aidha tunashauri kuwepo Bodi Maalum ya kusimamia Skuli za Maandalizi Binafsi, ili kuleta ufanisi. Ingawa kwa sasa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu inafanya usimamizi huo lakini ufanisi haupo katika kuzifikia skuli zote, kwani hali ilivyo hivi sasa inatishia upotoshaji na kuanguka kiwango cha elimu katika Skuli za Maandalizi.

WIZARA YA AFYA:

Hali ya Mapato:

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2012/2013 ilikadiriwa kuchangia shilingi 805,500,000 kupitia vyanzo mbali mbali. Hadi kufikia Disemba wizara imeweza

kukusanya asilimia 17 za mapato hayo ambayo yameshuka ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita ambapo wizara ilifikia makusanyo ya asilimia 21.

Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Moja:

Mhe. Mwenyekiti, kumejitokeza tatizo la kukosekana kwa vifaa muhimu katika Hospitali yetu ya Mnazi moja. Kamati imegundua mashine 3 za *X-Ray* na *Ultra Sound* hazifanyi kazi.

Aidha, kutokuwepo kwa mashine ya kuchomea taka (*INCINERETA*) na kupelekea taka zote kuchomwa katika eneo la ufukweni mwa bahari. Hali ambayo inapingana na majibu ya Mawaziri Barazani ya kuonesha kuwepo kwa mashine hiyo. Hatua hiyo inapelekea uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya ya jamii. Kamati inaiagiza wizara kuhakikisha kuwa vifaa hivyo muhimu vinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imebaini pia kuwa hakuna mashine ya *DNA* katika Idara ya Mkemia Mkuu. Kilichokuwepo ni sehemu tu ya mashine hiyo ambayo imepatikana kupitia msaada wa ufadhili wa *Donors*, baada ya ziara ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Tunaiomba wizara itueleze mbele ya Baraza lako tukufu, matumizi halisi ya fedha zilizopangwa kwa ajili ya ununuzi wa kifaa hicho. Aidha kamati inaiagiza wizara kuhakikisha kuwa sehemu ya *DNA* mashine iliyopatikana (*DNA EXTRACTION MACHINE*) inahifadhiwa vizuri pamoja na kupatikana sehemu ya vifaa vilivyobaki inakamilishwa katika bajeti ya 2013/2014 ili iweze kutumika.

Mradi wa Ujenzi wa Kitengo cha Macho:

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imepata mashaka juu ya kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha katika utekelezaji wa Mradi huo. Mhe. Mwenyekiti, fedha zilizotengwa kwa ajilli ya mradi huo ni jumla ya shilingi milioni 130, lakini malipo yaliyofanywa kwa mkandarasi yalikuwa ni shilingi milioni 25. Kamati inaiomba wizara kutupa ufafanuzi kwa nini walitenga shilingi milioni 30, lakini malipo yaliyofanywa kwa mkandarasi yalikuwa ni milioni 25.

Aidha, Mhe. Mwenyekiti, jengo hilo la Kitengo cha Macho ni bovu na linatishia usalama wa wagonjwa na wafanyakazi wa kitengo hicho. Kamati inaagiza jengo hilo liangaliwe kwa matengenezo au wagonjwa wahamishwe haraka.

Upatikanaji wa Dawa:

Mhe. Mwenyekiti, serikali mara kadhaa imekuwa ikieleza mbele ya Baraza lako tukufu kuhusu utengaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Hata hivyo, kamati imebaini kuwa hakuna uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na badala yake serikali hukaa muda mrefu na hutoa fedha chache zisizokidhi haja na kuwategemea wahisani hasa (*DANIDA*), ambapo pia wamekuwa na masharti yasiyo na muelekeo mzuri wa ufanisi katika upatikanaji wa dawa muhimu kwa afya ya jamii. Kamati imegundua kuwepo kwa upungufu wa baadhi ya dawa kama dawa za UKIMWI.

Hivyo, kama imeiagiza wizara kuhakikisha kuwa inajenga hoja za msingi kwa serikali kuu, ili kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ununuzi wa dawa hizo.

Safari za Wagonjwa Wanaopelekwa Matibabu Nchini India:

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko katika Ubalozi husika kuwa hawawepi taarifa za kabla juu ya safari za wagonjwa kutoka Zanzibar kwenda India, ila hupata taarifa pale tu matatizo yanapotokea kwa mfano kifo au matatizo mengine.

Kamati inaitahadharisha wizara kuwa wagonjwa hao wanaopelekwa matibabu hawapelekwi katika taratibu zinazokubalika. Kamati inaona ipo haja ya kuliangalia suala hili kwa undani zaidi kwani inaonekana pana mambo yaliyojificha ndani yake.

Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeridhika na hatua ya maendeleo ya Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar chini ya washirika wa maendeleo *USAID* na *DANIDA* pamoja na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, ni budi pawepo na umakini zaidi, ili kulinda jengo hilo hasa kwa kuweka maeneo safi.

Baraza la Tiba Asilia:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri wizara kutafuta jengo linalokidhi haja kwa ajili ya afisi ya Baraza la Tiba Asilia. Jengo lililopo ni finyu halina hata huduma muhimu za vyoo. Baraza hili limekosa ufanisi kutokana na kukosa mahitaji muhimu.

Kuhusu Huduma za Mama Wajawazito na Watoto:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri wizara na serikali kwa ujumla kuhakikisha kuwa vifaa vya huduma za mama wajawazito uingizwaji wake unakuwa wa kuendelea, ili kutekeleza agizo hilo la serikali. Kamati imebaini kuwa vifaa vinavyoingizwa ni vichache hasa katika hospitali za vijijini, ambapo idadi ya mama wajawazito inaongezeka na kupelekea ugumu wa kutekelezeka agizo hilo ipasavyo. Kwa ujumla Mhe. Spika, Agizo la Serikali la kutoa huduma bure kwa mama wajawazito halijatekelezwa hata kidogo.

Kuanzisha Darasa Maalum la *Biomedical Engineering*:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza wizara kwa kuanzisha Darasa Maalum la *Biomedical Engineering* kwa ngazi ya *Diploma* katika Chuo cha Afya Mbweni. Wahitimu wa darasa hili watasaidia kufanya matengenezo ya vifaa (*Ulta Sound, X-Ray, CT Scan* n.k) na mashine katika hospitali na kuepuka gharama kubwa za matengenezo ya vifaa hivyo. Kamati inashauri kuwatunza wafanyakazi hawa kwa nia ya kuwatumia baadaye.

Hospitali ya Wagonjwa wa Akili:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri wizara kutafuta njia za kukabiliana na upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongochekundu. Kamati imegundua wafanyakazi ni tatizo hasa madaktari ambao waliopo ni wawili tu. Aidha suala la chakula katika hospitali hiyo bado ni changamoto kubwa.

Madeni Makubwa ya Umeme katika Vituo vya Afya Pemba Kikiwemo Kengeja, Bagamoyo Mtambwe, Bogowa:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri wizara ya afya kutafuta namna ya kuondokana na mlimbikizo wa deni hilo. Wizara imekuwa ikilipa huduma ya umeme katika vituo vingi vya afya kwa shilingi elfu 80 kwa mwezi kinyume na bajeti iliyokusudiwa ya shilingi elfu 20 kwa mwezi.

Kukosekana kwa Fedha za Maendeleo Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, kamati imegundua kuwa kuna ugumu wa kufikishwa fedha za maendeleo Pemba na kupelekea baadhi ya miradi ya afya kushindwa kutekelezeka vizuri. Tunaiagiza wizara kuona umuhimu wa kuanzisha *Account* ya Maendeleo Afisi ya Pemba, ili kurahisisha upatikanaji wa fedha hizo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Madaktari Wanaoajiriwa Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeona kuwa ipo haja kwa wizara kuwa na mpango wa muda mrefu wa kujenga mazingira bora ya makaazi, ili kuwawezesha madaktari wanaoajiriwa Pemba kubakia. Madaktari 56 waliopangwa kutoa huduma Pemba wadhibitiwe, ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaiagiza wizara kuhakikisha kuwa nyumba zote zilizopangwa kuvunjwa, kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali mpya ya Abdalla Mzee zinavunjwa na wahusika kulipwa fidia kwa mujibu wa maelekezo ya tathmini ya Idara ya Mazingira.

Maamuzi hayo yatasaidia katika mpango wa muda mrefu wa matumizi ya eneo la ardhi la hospitali hiyo pamoja na kuepuka athari za kiafya na mazingira zinazoweza kujitokeza kwa jamii kutokana na shughuli za hospitali.

Hali ya Usafiri katika Hospitali ya Wete na Mkoani:

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini kuwa gari zinazoendelea kutumika hivi sasa ni chakavu na hazifai ambazo zimetolewa tangu miaka ya 1990. Hivyo, inaiagiza wizara kuhakikisha kuwa Hospitali ya Wete na Mkoani wanapatiwa gari ya uhakika ya kubebea wagonjwa.

Hata hivyo, kamati imeitaka wizara ihakikishe inavipatia ofisi Vitengo vya Afya Mazingira, Kitengo cha UKIMWI, Afisi ya Afya Elimu na Kitengo cha Ufuatiliaji wa Mwenendo wa

Magonjwa Pemba. Kamati hairidhiki na hali mbaya ya Jengo la Chanjo Machomane ambalo linatumika kwa ajili ya ofisi hizo. Jengo linavuja na kuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi. Kamati ilitoa agizo la kufanyiwa matengenezo lakini hadi hii leo hapana hatua yeyote.

Hitimisho:

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inaelezea kusikitishwa kwake na kuwepo kwa mchango mdogo wa fedha za serikali katika maeneo mengi ya Sekta ya Afya katika utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na makisio yaliyopangwa. Iwapo serikali itaendelea na utaratibu huu kuna uwezekano wa kutowepo kwa ufanisi katika sekta hii muhimu ya afya na pia katika utekelezaji wa miradi husika.

Serikali bado haikuweza kufanikisha ipasavyo utekelezaji wa vipaumbele katika Sekta ya Elimu, Afya na Ustawi wa Watu kinyume na ambavyo imedhamiria. Sekta hizo tatu zinakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu mkubwa wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, tunaanza kuchangia haya tuliyonayo juu ya meza yetu na hivi sasa ninao wachangiaji wanane Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kutoa angalizo tu, kwamba tunafahamu utaratibu wetu tunaokwenda nao. Kwa hivyo, kwa heshima na taadhima naomba tuendelee na utaratibu ule ambao tumejipangia, nawashukuru na mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe niliposimama mimi wamefurahi sana na kusema kuwa wao wako tayari ku-*delay* kunipa mimi dakika 30, ili tuendelee. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia na kwanza naunga mkono hotuba ya Mhe. Mwenyekiti na kuipa asilimia mia moja. Lakini Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuipa asilimia mia moja kamati yetu na ustadi wake ilijitahidi kutafuta mambo yenye kasoro na kwa upande mwengine na sisi Wajumbe kuna mambo mengine ambayo yanakuwa yamesahaulika na tunaweza kuwasaidia kwa mujibu wa utaratibu wa utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo mengine hasa wakati ule wa bajeti tulijaribu kuyaeleza kwa ajili ya kutafuta ufanisi wa utekelezaji kabla ya ile ripoti ya kamati kuletwa hapa, lakini nimegundua Mhe. Mwenyekiti mengine yamekosekana kuwekwa.

Katika muono wa kamati yetu ilivyoona kuhusu mapungufu ya dawa katika hospitali yetu hususan sehemu ya Wagonjwa wa Akili, lakini sio hapo tu isipokuwa dawa nyingi sana katika hospitali zetu zinakuwa zinakosekana. Mhe. Mwenyekiti, siku moja niliuliza swali na Mhe. Naibu Waziri wa Afya sijui siku ile alinifanyia kejeli au alinijibu kwa ufanisi wa aina gani

ambao anaujua yeye, kwa sababu aliniambia kuwa nimfuate ofisini kwake na nikaziangalie hizo dawa ambazo nilizozitaja pale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Waheshimiwa Mawaziri au Manaibu Waziri wakati wanapotujibu, basi ni vyema wazingatie kwa sababu sisi hatukurupuki tu na lengo ni kutengeneza na sio kwamba tuje hapa kwa ajili ya kuonekana tu.

Kwa hivyo, wanapotujibu tunawaomba sana, kwa sababu tunayo sheria na inakuwa haitumiki Mhe. Mwenyekiti kifungu cha 22, kifungu ambacho kwa mujibu wa sheria ya kifungu cha 4 tayari kinambana Mhe. Waziri yeyote ambaye mwenye kutujibu mambo ambayo hayastahiki, basi sheria hii ipo Mhe. Mwenyekiti, achukuliwe na adhibitiwe kwa mujibu wa sheria, lakini sheria hii haifanyi kazi Mhe. Mwenyekiti ndio maana tunajibiwa ovyo baadhi ya wengine wanavyotujibu.

Sasa mimi leo nauliza je hii kamati imesema uongo na imegundua kuwa dawa hazipo kuanzia Hospitali ya Wagonjwa wa Akili na ninakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti na Hospitali ya Rufaa ya Mnazimmoja baadhi ya dawa hakuna, kwa sababu mimi mwenyewe nimeshanunua dawa za ganzi, mabomba na baadhi ya vitu vyengine.

Kwa nini tusiseme ukweli na tukisema ukweli Mhe. Waziri wa Fedha yupo, tena ni mtu mzuri tu ataweza kusaidia, lakini tunaposhindwa kusema ukweli, basi ndio huu Mhe. Mwenyekiti. Kwa mfano, mtu atakwambia nilikuwa nikijibu kisiasa na hapa hakutakiwi siasa hapa Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa panatakiwa jambo la ukweli na siasa tuweke pembeni tutaua wananchi.

Kwa hivyo, panapotakiwa suala la kisheria basi jibu jambo ulililoliona na wala si vibaya ukasema kwamba kweli tunakiri kwamba dawa hakuna, lakini kutokana na mapungufu moja, mbili, tatu na wizara ya Fedha tutakaa nayo kitako na watatusaidia wafadhili kazi imekwisha, lakini mtu anakwenda kusema dawa zipo na ukitaka njoo uzione nitakuonesha ofisini, tunakwenda wapi Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, nimeona kuwa kasoro moja hiyo tunaiweka kando na Mhe. Waziri aifanyie kazi.

Sehemu nyengine Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hata zile kumbukumbu za *files*, yaani ofisi ile wanayoweka *files* nimekwenda kuona Mhe. Mwenyekiti utalia machozi, kwa kweli tunapoteza kumbukumbu za wagonjwa wetu na wengine sijui kama *files* zitapatikana, yaani zimewekwa ovyo kabisa. Hatufikiri kwamba hili ni jambo la muhimu. Mhe. Mwenyekiti, hapo Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazimmoja, lakini tumekwenda kuangalia na hapa pia lipo tatizo hilo.

Kutokana na hali hiyo, tunaomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna mambo mengine si ya kudharau, nadhani ni vyema tutenge ofisi kwa ajili ya kuweza kuokoa suala lile, kwa sababu kumbukumbu ni kitu muhimu kwa mgonjwa kuweza kujua *statement* yake iko vipi na wala hatukulipa umuhimu *files* zimetupwa ovyo zinavujiwa na mvua.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala hili wakati atakapokuja kutoa ufafanuzi basi aje kunijibu kuwa suala lile tayari limeshafanyika na limeshawekwa sawa na hapo tunakubaliana vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu wengine Kituo kama cha Sukari au Macho. Nilikwenda Kitengo cha Macho, kwa kweli kile anaweza kuua wakati wowote, kwa sababu jengo lile limeshafanya ufa na tayari nimeshalizungumza suala hili, kwani mimi mwenyewe nimeshakwenda. Kwa hivyo, nilipokwenda kule Mhe. Mwenyekiti, nilinyatia kutokana na *heavy weight* niliyonayo, kwa sababu ningeliwaangusha chini. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine tukidharau ndipo tunapokuja kuua.

Kwa mfano, siku moja nilisema Mhe. Mwenyekiti kuhusu masuala ya makontena juzi kontena limeanguka pale Mikunguni bado kidogo liue na siku zote nilikuwa nikisema masuala kama haya, kwa sababu sisi wengine ni masharifu tukikwambieni jambo basi mapema muanze kulisawazisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kuwa kwanza Kitengo kile ni cha Watu wa Macho, basi ni vyema wapatiwe eneo la kuweza kujinafasi na kuweza kufanya *operation* pamoja na kutibu watu kwa usalama kabisa. Sasa leo unakwenda kutibu lakini mtu anakuwa ananza kuutizama ule ufa. Mhe. Mwenyekiti, na wao hatuwatendei haki kama hatukuwatafutia eneo ambalo linaweza kuwasaidia.

Vile vile niliangalia sana kitabu hichi kwa ajili ya kutizama suala la Mashine ya Uchunguzi wa Kansa. Mhe. Mwenyekiti, hapa nasikitika sana na nimesema nitaendelea kulisema mpaka karibu ya kutukanwa na wala hili sitoliacha. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amekwenda kufanya ziara na akaambiwa usijali Mheshimiwa kesho tu mashine itakuwa sawa hapa na akauliza mpaka leo mashine bado hazijaanza kazi.

Pia alikwenda Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, yaani viongozi wetu wote wawili lakini bado wameambiwa Mheshimiwa wiki moja utakuta mambo yako sawa. Kwa kweli mpaka leo mashine zile na fedha zilitumika ni za wavuja jasho na wala hakuna *action* yoyote na niliambiwa mimi kwamba itaundwa tume ambayo itatoka Tanzania Bara wataalamu na mimi nitahusishwa tume mpaka leo bado haijaundwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunajibiwa majibu ambayo hayana msingi kabisa na tunaambiwa mashine zimekwaruzika na kumbe sio kukwaruzika, isipokuwa mashine zimepungua vitu na tuseme ukweli tusifiche kwa nini tunaficha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kwa sababu siku moja nilimpeleka mgonjwa mimi, unajua Mhe. Mwenyekiti wanaambiwa akija Mshimba musimpe taarifa na hivyo sivyo na wala mimi siendi kule kwa ajili ya kuuza urembo, isipokuwa nakwenda kupeleka wagonjwa wangu wa jimboni na yale mambo ndio nayakuta yanatokea na nyinyi hamjui.

Kwa mfano, kuna wagonjwa kama watano au sita wamekufa kwa sababu ya maradhi ya kensa wamechelewa kufanyiwa uchunguzi kwa sababu hatuna vifaa. Mhe. Mwenyekiti, watu 65 ambao ni ushahidi tosha na wengine katika jimbo langu sielewi kwa sababu gani kwani Bara kule, hebu tutizame kule Bara, yaani Tanzania Bara nzima inategemea Muhimbili je wewe mtu wa Unguja utawahi kupata humo yaani mpaka vile vinang'oka na kushonewa hapa. Sasa leo mashine iliyotiwa kwenye tenda na wataalamu kwa ajili ya kuwasaida Wazanzibari mnatuua kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, nasema ni suala ambalo linanitia uchungu Makamu wa Rais wawili wamekwenda kuangalia kituo hicho na wote wanadanganywa mpaka leo na anikatalie leo aniambie kwamba mashine zimeshakuwa tayari, leo ninaye mzee wangu yuko hospitali nashindwa kumpeleka Muhimbili kwa sababu najua atachukua muda mrefu sipati jibu, ukitoa rushwa basi wiki mbili au tatu unapewa.

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa mfano munavyotufanyia watu wa Viongozi wa Serikali Kuu munatufanyia kinyume na matakwa ya watu wa *backbenchers*, kivipi basi mnachagua wakandarasi, yule si mkandarasi na yule si mwekezaji wa mambo kama haya, si *specialist* wa kujua masuala kama haya. Keshokutwa mtatuletea katika uwanja wa ndege na leo mnatuletea masuala kama haya hivyo mnavyotufanyia tunaharibikiwa. Tuna *personal interest* ya nini sasa? Hivi mpaka tupate 10% Mhe. Mwenyekiti hili suala linauma sana.

Leo nenda pale hospitali nenda katizame *biosis* zilizokwishatolewa pale hebu katizameni wenyewe fanyeni ziara mkaangalie Zanzibar imekuwa sasa hivi idadi kubwa ya watu wa kensa mitambo ile tunamgojea Mnorway aje mwengine atufadhili tunamalizika ukweli tuseme jamani tunamalizika. Mhe. Waziri hili suala mimi sitokubaliana nalo kuntu kwa sababu hiki kit u kina maslahi ya wazanzibari ambao wataweza kujua time ya kujua kensa yangu mimi ina stage gani, tumepoteza Mheshimiwa inasikitisha sana Mheshimiwa, hili suala mimi ninafikiria tungejaribu sana kuna mambo mengine jamani msione tabu ukisema kweli ndio kutengeneza, unakuwa mzuri sana mtu ukisema ukweli Waziri akija semeni ukweli mnaogopa nini? Huna fedha mwambie Waziri wa Fedha yeye anangojea tu kakaa mwambieni twambieni tumwambie hana tatizo yule lakini hatusemi tunabakia sisi hapa kutudanganya tu, tumechoka kudanganywa na hatudanganyiki tena mwisho.

Mheshimiwa suala la Mkemia, napo hapa vile vile pana matatizo yake Mkemia akisema jambo halifai basi mimi nasema liwe halifai. Unga mpaka leo sijui kama ushaondoshwa pale na haufai sumu tu si wanataka kutuua. Makamo wa Kwanza kenda pale kasema wee mpaka kachoka. Mheshimiwa mambo mengine yanatilisha huruma Mhe. Mwenyekiti mimi naomba sana hili suala ambalo hebu tufanyiwe kazi ya uadilifu na hasa hao uliotuchagulia.

Mheshimiwa ukija suala la maposho la dokta mimi sipingi hata kidogo la kupewa hapa fedha za *calling* madokta. Lakini Mheshimiwa twende na hawa ma-*orderly*, twende na hawa ma-nurse, hivi nao hawastahiki na wao wanakaa kwa sababu nimepata experience nzuri sana hivi nikenda kusoma sasa hivi basi mimi wala sifeli katika masuala ya mambo ya utibaji haya hata kidogo sifeli. First aid ya mwanzo anakuja *orderly* anamtengeneza mgonjwa akiondoka pale anakuja mwenyewe *nurse*, tayari anakwenda pale na yeye anaanza treatment pale aliyosomea first aid ya pale pale anafanya ile kumu-act dokta mwenyewe specialist. Dokta anatafutwa kwa *umbulance* niambie sasa time ya kutoka pale mpaka kuingia chooni, time ya kutoka pale mpaka kufika hospitali nani mlinzi wa yule mgonjwa kama si nurse kwa nini na yeye asiongezwe posho. Hana risk allowance maana yake ana risk hana chochote pale Mhe. Mwenyekiti kwa kweli inasikitisha, ata akija dokta yule keshamaliza temperature imeshashuka. Kama otherwise mgonjwa wa kufa keshakufa.

Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakisha dakika tano.

Makame Mshimba Mbarouk: Nakwenda mbio mbio. Mheshimiwa nakwenda kwenye *point* za mwisho. Tunaenda katika masuala ya elimu. Nimeona humu kuna uimarishaji katika shule za misingi na mambo mengine. Mheshimiwa kule kwetu tuna eneo moja kubwa sana, eneo hilo sasa hivi wawekezaji wamekuja kutaka kutujengea eneo la Kiwengwa. Lakini hapo nyuma eneo hilo lilipimwa mara tatu, baada ya kupimwa mara tatu sasa imekuwa watu wamepewa hati vyoroge vyoroge maana yake huwezi kuamini hizo hati nitasema. Naomba kidogo Mheshimiwa nistahmilie hizo tano niongeze na tano ziwe kumi samahani sana Mheshimiwa wangu tunataka kutengeneza.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja mimi nilikwambieni hapa iko siku tutawataja waheshimiwa wakubwa wamechukua maeneo iko siku tumesema tunatoka. Leo ninasema nilikwambieni mimi hapa jamani ee itafika pahali mimi nimekupeni siku 7 jitokezeni sikuona vimemo kuletewa leo nasema Mhe. Mwenyekiti haiwezekani tunataka kufanya skuli tunashindwa ya maendeleo tukasomeshe wapi watoto maeneo yanachukuliwa na wakubwa leo nataja.

Mhe. Mwenyekiti, nina ramani hii hapa, hapa kuna Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Mifugo anakwenda kuchukua eneo na yeye, tunakuja mwengine kuna Mohammed Ussi Kheri simjui ndio nani na kuna Bi. Amina Juma Shamhuna eneo moja hilo wamepewa watu watatu. Anasema namba 540, na huyu 540 na huyu 540 square metre kila mtu difference yake, mimi nataka kujenga Skuli. Sasa mimi naomba Mhe. Makamo kenda mara ya kwanza katoa kauli nzuri nikasema well and good mara ya pili akatoa kauli akasema zifutwe zote na tatu anasema aa kauli yangu nabadilisha, mimi sibadilishi kauli yangu nasema pale pale, wakati nimekamata msahafu nakwenda nao sambamba na msahafu, nasema wananchi wafutiwe eneo lao kesho tukajenge skuli. Wameshajenga tangi, wapo wafadhili fedha zimekaa tu zinaelea nasema mara moja hivi viwanja kwanza feki halafu isitoshe sijaendelea.

Nakuja mwengine Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya maji nimekwambia nitasoma tu mimi siogopi potelea mbali Mungu ananilinda na msahafu wangu. Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Ujenzi wa zamani eneo hilo moja basi alimradi watu wachukuwe tu. Halafu anakuja tena Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Kiongozi, halafu inakuja tena 540 Asha Ali Juma. Tunakwenda wapi Mheshimiwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti hivi viwanja vishakuwa havifai, vina utaratibu sio vibadilishwe mara moja watu wajenge skuli kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Mwenyekiti nimalizie Wizara ya Kinamama. Wizara ya kinamama lakini nasema leo nawaficha hawa wengine wajitokeze kwa siri waniletee vibuku vi-memory, leo nawataja hawa wengine natoa tena siku 7 one more wengine siku hiyo nitakuja kuwamaliza. Sasa ninakuja katika Wanawake na Watoto. Mheshimiwa nilisema mimi suala la hati la ile Forodhani pale sijapata jibu mpaka leo. Haiwezekani warudisheni kule kule kwao si tatizo hakuna tatizo kule kama haiwezekani kutoka hati basi warejeshwe kule kwao kwenye jengo lao la zamani halina tatizo lile jengo, jengo zuri nafasi wanayo wakicheza vizuri kwenye bustani yao. Warejeshwe hati tunaitaka pale Mheshimiwa tumeambiwa na waziri hati imo katika mayatarisho, matayarisho mpaka lini Mhe. Mwenyekiti, ile hatma ya wale watoto yatima hebu tuifanyeni tuitoe katika mikono yetu. Mheshimiwa mimi naomba hili suala wapewe.

Lakini la pili nimshukuru sana Mhe. Waziri nimpe hongera sana kwa kuithamini hii skaut. Mheshimiwa hili ninampa hongera tena kubwa sana amesema hivi amewasaidia vijana wa skaut na humu nimeona jinsi gani vijana wengi amewasaidia. Hili nampa asilimia mia kwa mia kwa sababu ndio matakwa yetu sisi watu wa backbencher. Lakini la hati simuungi mkono mpaka hati ipatikane.

Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kitope tunasema hivi ripoti kuu ninaiunga mkono ya Mheshimiwa Mwenyekiti Hija mwenyewe mpiganaji mkuu. Ahsante sana.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti kwanza nichukuwe nafasi hii nikushukuru wewe binafsi na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuchangia ripoti hii za mawaziri pamoja na ripoti ya Kamati. Kwanza kabisa niwapongeze mawaziri wote ambao wamewasilisha ripoti zao kwa namna ya utekelezaji ambao walitakiwa na kamati watekeleze.

Lakini nianze na Wizara nyeti ambayo Wizara iliyonizaa mimi. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Wanawake na Watoto ni Wizara nyeti. Lisingekuwepo Baraza lako hili tukufu kama si Wizara hii. Mwanamke ndie aliyetuzaa mtoto kuna mtoto wa kike na mtoto wa kiume lakini hukua hao, wakisha kukua tena wanafanya mambo yao hujumuika na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti hii Wizara kwa nini nikaiita nyeti kwa sababuWizara hii inajumuisha mambo mengi ya kijamii, mwanamke ukimuelimisha mwanamke mmoja unaelimisha jamii. Ukenda katika Ustawi wa Jamii ni jamii yenyewe, sasa niseme kwamba mimi nitakuwa na machache katika Wizara hii nangoja wakati wa bajeti, maana kuna mambo nachunguza chunguza kidogo.

Mhe. Mwenyekiti mimi ninasikitishwa sana, na udhalilishwaji wa watoto, niseme kwamba udhalilishwaji huu wa watoto kwa kweli tuna dhima kwa Mwenyezi Mungu. Niwaombe wananchi wa nchi hii tuache mambo ambayo si mema kwao wala si mema kwetu, kwa sababu kuna msemo mla kuku wa mwenziwe miguu humuelekea. Wewe unamdhalilisha mtoto wa mwenzio unamfanyia vitendo ambavyo si vizuri ujuwe kwamba na wewe utazaa mwanao atadhalilishwa tu kwa vyengine au kwa vyovyote. Niwaombe sana wananchi wa nchi hii tusifanye mambo ambayo kwa upande wa dunia ni mabaya na kwa upande wa akhera ndio kabisa.

Nitoe wito kwa wananchi, nitoe wito kwenye vyuo, nitoe wito kwenye sehemu ambayo kwa kweli inawadhalilisha watoto wetu kijinsia na sasa hivi limeingia wimbi la kuwadhalilisha watoto wa kiume wadogo. Mhe. Mwenyekiti naomba sana jitizame wewe mwenyewe kama ni mtoto wako huwezi ukakubali hilo moja.

Lakini jengine majengo ya Ofisi au majengo ya Wizara ametuelea humu Mhe. Waziri kwamba wako mbioni wameshatia nini, wameshatia mkataba wameshafanyaje, nasema Mhe. Mwenyekiti hebu tuwe wakweli. Mimi kwanza nichukuwe nafasi hii nimshukuru sana marehemu, kwa sababu marehemu Karume alikuwa kitu akikifanya Unguja basin a Pemba kinaanza chochote kile cha maendeleo. Ndio maana ukaona kwamba kuna majengo Zanzibar hapa Unguja yaliyojengwa hapa na Pemba yamejengwa kusiwe na choyo cha kimaendeleo tusibague. Wizara husika hapa zimeshaanza majengo kwa nini walipoanza hapa kujenga wasijenge na Pemba.

Tunapoteza fedha nyingi sana kwa kukodi nyumba za watu binafsi tukizifanyia hesabu fedha tulizolipa basi ni mamilioni tunaweza kujenga hata nyumba 20 tokea tulipoanza kukodi majumba ya watu binafsi. Ninaiomba serikali kama ilivyoanza ujenzi Unguja wa maofisi ya mawizara basi haraka ichukuwe hatua kuanza Ofisi za Mawizara Pemba.

Mhe. Mwenyekiti utakwenda Ofisi za Pemba wewe saa nyengine unashindwa kupanda ofisi mbovu, Afisa Mdhamini anakaa na watu ambao Mkurugenzi, sijui Mkuu wa Idara, sijui mkuu wa nini vyumba vimekatwa patition hata hujui uingie wapi uwche wapi. Naiomba sana serikali, natoa changamoto kwa serikali, tusibague katika mambo yetu ya maendeleo. Majengo hayo hapo tunayaona sijasikia hata siku moja jengo kujengwa Pemba, ukiuliza tuko mbioni, hizo mbio sijui za marathon zitafika wakati gani.

Ninaiomba sana serikali inapofanya kitu cha maendeleo na kitu cha wananchi basi ifanye kote kte Pemba na Unguja. Mhe. Mwenyekiti mimi sitokuwa na mengi Wizara ya Wanawake nimeshaizungumza sasa niko katika Wizara ya Afya.

Kwanza nichukuwe nafasi hii niwape pole Wizara ya Afya kwa matokeo ambayo yametokea hivi karibuni na kuunguliwa na bweni lao hapo Chuoni, niwape pole sana. Lakini niwaombe snaa Wizara ya Afya tuhakikishe tunpitia sana Mnazi mmoja kuna madhambi mengi sana mimi ninayaweka mpaka bajeti, sasa hivi si wakati wake. Kuna madhambi mengine ni ya makusudi, kuna madhambi mengine kutokuwa na uwezo wa fedha hayo hayawezekani kama serikali haikuiipa Wizara ya Fedha, fedha Wizara ya Afya lakini kwa kweli kuna mambo lazima tuyaangalie kwa jicho la huruma. Nilisema Wizara ya Afya niseme maneno hayo.

Nakuja Wizara ya Elimu, kwa sababu wenzangu wameshachangia sana Wizara hii na ndio Wizara ambayo ni Wizara mama sote humu tumepitia kwenye elimu. Lakini nizungumze kuhusu yale majengo ambayo ya sekondari kwa kila Wilaya. Yale majengo jamani tunajua tunapeleka maendeleo tukipeleka maendeleo basi tuhakikishe pale tunapoyapeleka panastahiki. Lakini unajenga majengo kama yale mtoto unamtoa miles and miles aje pale kwa kweli tutafakari na tufikiri, lazima majengo yale tutafute pahala ambapo pana usalama na uhakika zaidi. Tumepata maendeleo kama yale si madogo, niseme tu kwamba Wizara ya Elimu inapopata miradi kama ile basi i-target pale pahala ambapo hata lolote likiwezekana Mungu apishe mbali watu wanaweza wakapata msaada. Lakini kuna majengo mengine likitokea lolote lile hamna msaada. Hata wakifikwa hao wana vijiji kwenye majengo yale basi ni masafa makubwa.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wa Elimu hebu aje anifafanulie haki ya likizo ya walimu. Kwa sababu mfanyakazi yoyote yule ana haki ya kuchukua likizo. Na akichukua likizo unampa haki yake. Sasa kuna utatanishi ambao kwa kweli nije nifahamishwe, hao walimu wanapochukua likizo wanalipwa lipwaje fedha zo? Nikisha kufahamishwa mimi sina matatizo. Tunaelewa kwamba Wizara hii ina watu wengi sana, lakini pamoja na hayo lazima mtie kwenye bajeti. Ninajua kila mwaka mtu ana haki yake ya kwenda likizo kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizoziweka. Si vyema mtu kama yule ambaye ni ufunguo wa watoto wetu katika maisha ukamfanyisha kazi anapotaka kwenda kupumzika ikawa unamdhalilisha kwa fedha zake za likizo.

Naomba sana Mhe. Waziri nije nipate ufafanuzi katika likizo za walimu, lakini pia ufafanuzi wa majengo yale ya sekondari kwa kila Wilaya.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi kuweza kuchagia hotuba hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Mhe. Mwenyekiti imenibidi nichangie hotuba hii kwa sababu maalum ambazo zimenigusa ndani ya nafsi yangu.

Mhe. Mwenyekiti mimi nikiwa mjumbe wa kamati hii niiunge kwanza mkono kwa asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti nikianza kidogo na Wizara hii ya Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti katika suala zima hili la tatizo la ombaomba kwa kweli tatio hili la wazee wetu watu wazima limekuwa likishamiri siku hadi siku hususan katika maeneo ya mijini hapa Unguja, Pemba na sehemu nyengine mbali mbali katika nchi yetu. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti tatizo hili limekuwa ni kubwa na la kusikitisha na ipo haja kuangalia kwa kina kabisa kulifanyia kazi kuhakikisha kwamba wazee wetu wanaondokana na tatizo hili la kuomba omba.

Lakini Mhe. Mwenyekiti cha kusikitisha zaidi kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Dr. Ali Mohammed Shein ilitoa ruzuku ya kuwapatia wazee angalau shilingi elfu tano tano ingawa fedha hizi haziko katika Wizara hii ya Wanawake na Watoto, lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti kwamba fedha hizi wazee wetu kwamba hawapewi kwa wakati ambao unakusudiwa. Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, wazee hawa wana miezi mitatu na huu wa nne unakwenda bado fedha zile bado hawajapatiwa ambazo ziko katika Ofisi za Mikoa. Kwa hivyo ingawa ni pesa kidogo lakini zinawasaidia wazee wetu katika kuondoa shida zao ndogo ndogo. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri kuhakikisha analifatilia hili kwa kushirikiana na Waziri husika ili kuweza kuwapatia wazee wetu wale kile kidogo ambacho Mhe. Rais anawapatia ili kuweza kujikimu na matatizo madogo madogo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti nije katika masuala ya vijana hususan hawa wanaojiendeleza katika kilimo hiki cha maua ya rozela. Juzi hapa wakati naulia swali la nyongeza Mhe. Waziri hakunijibu vile ambavyo mimi ningeliridhika. Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu ambao wamejikusanya na kwa moyo mmoja katika kujikwamua kiuchumi na kujikwamua kimaisha, wamejikusanya wake kwa kiume katika maeneo ya kule Tunguu na kwa kweli vijana hawa ni wa kuigwa mfano. Iwe mfano kwa vijana wengine katika kuitikia wito wa kujikwamua katika kuleta maendeleo kwa wao wenyewe na familia zao. Lakini Mhe. Mwenyekiti kwa kweli vijana hawa wanastahiki kupewa nguvu za ziada na hasa yale maeneo ambayo wanayolima pale katika maeneo ya Tunguu. Mhe. Waziri naona ipo haja kwa kushirikiana na Wizara Kilimo, na Wizara ya Ardhi kuwapatia vijana hawa maeneo mengine ya ziada ambayo yanaendana na kilimo hiki cha mbogamboga. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti pale Tunguu panahitaji kazi ya ziada. Panahitaji maji, pale maji ni tatizo halafu vile vile mazao wanayoyapanda yanaibiwa. Kwa hivyo ipo haja mbali na kuendeleza pale ya kuwapatia maeneo mengine hili Mhe. Waziri nadhani ipo haja kubwa ya kulifanyia kazi kuhakikisha kwamba wanapata maeneo mengine.

Mhe. Mwenyekiti nikija katika Wizara ya Afya ambayo ndio iliyonisababisha mimi leo kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ambayo mimi mjumbe wa kamati hii. Mhe. Mwenyekiti, nadhani ingekuwa ni kikao chengine tu cha nje ningesema basi ningeomba wajumbe tusimame

kwa dakika moja ili kumuombea dua mwananchi mwenzetu, Mzanzibari mwenzetu, mkaazi wa Mwembeshauri Jimbo la Rahaleo ambaye amepoteza maisha kwa uzembe mkubwa uliofanywa na madaktari hawa wanaojiita madaktari asilia wa Kichina.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tu mama huyu ambaye alikuwa na matatizo ya uzazi hana kizazi, baada ya kusikia kwamba kuna dawa za tiba asilia zinazotolewa na Wachina ambao wako pale Vikokotoni. Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha sana, mama huyu alikwenda kupata tiba hii katika *clinic* ile ya Vikokotoni na akapigwa sindano ambayo inasemekana wenyewe wanasema zinamfanya yeye apate mimba na kuweza kupata mtoto. Lakini Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuchomwa sindano ile mama huyu kwa jina anaitwa Safia Francis alipoteza maisha na baada ya kuchomwa sindano ile hali yake ikawa mbaya na madaktari wale walikataa hata kumpeleka katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Lakini kutokana na sindikizo la wananchi walioko pale madaktari wale walipanda gari mpaka Mnazi Mmoja baada ya kufika yule mgonjwa wao wakapita mlango wa nyuma wakakimbia, wakati huo hali yake iko katika kuelekea huko alikoelekea ambako sote tuko nyuma yake.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeiomba wizara na waziri husika wa wizara hii kulifuatilia kwa kina suala hili na kuwafuatilia hao waliohusika na kitendo hiki cha kupoteza maisha kwa mama huyu. Taarifa tulizonazo kwamba hili si la mwanzo hii ni taarifa ya pili.

Juzi tu hapa Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alitupa taarifa ambayo inahusiana na ziara ya Rais wa China na mambo mbali mbali ambayo China wanatusaidia, lakini Wachina hawa wamekuwa badala ya kutusaidia wanatupotezea maisha wananchi wetu. Kwa sababu wanatumia tiba za asilia kwa njia ya kujipatia fedha huku wananchi wetu wakiteketea na kupoteza maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la kupatiwa madawa. Katika ripoti hii imeeleza tatizo la upatikanaji wa madawa hususan zile dawa muhimu ambazo wananchi wetu wanakuwa hawana uwezo wa kuzinunua hasa katika vijiji au mashamba kule waliko wazazi wetu ambao hali zao ni duni. Kwa kweli ipo haja ya kuangaliwa na kulifanyia kazi kwa kina kuhakikisha kwamba dawa zile muhimu zinapatikana na zinakuwemo katika hospitali zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikirudi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, katika wizara hii kuna matatizo ambayo yamezungumzwa katika suala zima la hali mbaya ya mabanda yetu ya skuli. Katika hali hii Mhe. Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Rahaleo pia nalo ni katika skuli ambazo ziko katika hali mbaya ikiwemo Skuli ya Mwenyeladu ya Sekondari mabanda yanavuja kwa kweli ni hali ya kusikitisha kuona kwamba skuli kongwe kama hizi zinakuwa katika hali ya kusikitisha.

Lakini hayo hayatoshi Mhe. Mwenyekiti, Skuli ya Lumumba ni skuli ambayo ina historia kubwa katika nchi hii lakini hali ya skuli hiyo hususan katika masuala ya mazingira kwa kweli utapokwenda pale Mhe. Mwenyekiti, chozi litakutoka kutokana na hali ya mazingira ilivyo. Watu wanachimba mchanga ovyo, mashimo yamejaa na tayari yanaelekea katika skuli yenyewe ipo hatari hata kuja kuanguka skuli ile na kuondoa haiba, uzuri na mandhari ya skuli ile.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kiufuatilia suala hili na kuhakikisha kwamba kutakuwa na mbinu mbadala kuhakikisha kwamba skuli ile inarudi katika hali yake kama ilivyokuwa zamani.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, narudia kusema kwamba, naunga mkono hoja ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii nami nichangie ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii na Ripoti za Mawaziri watatu ambazo wizara zao ziko chini ya kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Makamo Mwenyekiti wa kamati hii mhe. Hija Hassan Hija kwa ripoti yao nzuri na ya kina kabisa, na unapowasilishiwa na mtu kama Mhe. Hija unajua kwamba umewasilishiwa na kamanda. Kwa hivyo, unajua kabisa kwamba mambo yake huwa si ya kubahatisha bahatisha kama ambavyo imethibitika mara nyingi katika michango yake mbali mbali ndani ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kupoteza muda na mimi naomba niende kwenye ripoti kwa mujibu wa maelezo tofauti ambayo yapo katika wizara hizi tatu. Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na Wizara ya Afya, Mhe. Mwenyekiti, tunapongeza hatua mbali mbali ambazo zilikuwa zikichukuliwa kwa ajili ya kufanya marekebisho na kiujaribu kuifanya hali iwe bora zaidi. Jitihada za serikali kwa mfano za kuanzisha Bohari Kuu ya Dawa, kila mtu ambaye ameiona inampa moyo tunadhani kwamba sasa yale matatizo ya upungufu wa dawa mara kwa mara katika hospitali na vituo vyetu vya afya yatapungua.

Lakini vile vile angalau sasa hivi ukienda katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja lile suala ambalo niliwahi kulipigia kelele humu ndani kidogo limefanyiwa marekebisho, ukienda angalau kuna utaratibu unaoeleweka sasa hivi kwamba unaripoti pahala kadhaa kuna mtu anakushughulikia mpaka ukafika kwa daktari na kama kulazwa ukafika kwenye wodi. Kwa hivyo, tunapongeza jitihada hizo Mhe. Mwenyekiti. Lakini pamoja na kupongeza jitihada hizo kuna mambo katika ripoti hii ambayo yanasikitisha na mengine hayamo katika ripoti hii nitayataja ili Mwenyekiti wa Kamati na Mawizara yanayohusika yatapokuja waweze kutupa ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo limenishitua sana ni lile ambalo liko katika ukurasa wa 69 wa ripoti. Mhe. Mwenyekiti, wakati akiwasilisha bajeti yake ya mwaka huu wa fedha tunaoendeleanao na nakumbuka kesi hiyo hata mwaka juzi Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alitwambia moja ya vipaumbele vya bajeti yake ni afya, nadhani ilikuwa mwaka juzi, niliwahi ku-*challenge* hapa ndani kwamba ukifanya hesabu hasa ya wizara moja moja na kasma walizopewa mbona haioneshi hicho kipaumbele cha Wizara ya Afya na zile nyengine ambazo zilitajwa, lakini kwa vile nazungumzia Wizara ya Afya naomba nijikite hapo. Lakini leo ndio nimekuwa hoi bin taaban Mhe. Mwenyekiti.

Ukurasa wa 69 kitabu hiki cha Ripoti za Kamati naomba niisome, utekelezaji wa matumizi ya fedha, fedha za kawaida, Wizara ya Afya ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 18,284,000,000 kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Shilingi 4,592,000,924 kwa kazi za kawaida na shilingi

13,731,080,000 mishahara na maposho. Mpaka kufikia Disemba 2012/2013 jumla ya shilingi 3,918,867,651 ziliingizwa. Mhe. Mwenyekiti, sina *calculator* hapa lakini kwa hesabu ya haraka haraka hii ni kama asilimia 16. Sasa kwa sababu tunazungumzia kipindi cha nusu mwaka tulitegemea angalau asilimia 50 iwe imekwenda hasa kwa sekta muhimu kama ya afya.

Lakini isitoshe, kwenye Fedha za maendeleo Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu katika ripoti. "Kwa upande wa fedha za maendeleo Wizara ya Afya iliidhinishiwa jumla ya shilingi 21,982,205,000 kati ya hizo mchango wa serikali ni shilingi 2,731,600,000. Hadi kufikia Disemba 2012 jumla ya shilingi 192,251,400 zilipatikana.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni hali inayotisa sana, kiwango cha uingizaji wa fedha hakiridhishi hata kidogo. Sasa mimi najiuliza huku tukisikiliza ripoti za kila mwezi zinazotolewa tunaambiwa makusanyo ya serikali yanaongezeka, serikali inajisifu kwamba ilipoingia mwaka 2010 Novemba ilikuwa inakusanya shilingi 13 bilioni kwa mwezi sasa hivi inakusanya shilingi 22 bilioni kwa mwezi, sasa hizi pesa nadhani kwanza zingekwenda kwenye zile sekta ambazo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi masikini wa nchi hii na sekta mbili kubwa ndizo zinasimamiwa na kamati hii, Sekta ya Elimu na Sekta ya Afya. Sasa unapopata uingizaji wa fedha kama hivi Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana, najiuliza mimi nini kipaumbele cha serikali hii au ndio wingi wa safari za wakubwa kwenda na kurudi nje ya nchi kwenda kujifunza mafunzo yaliyokuwa hatuyaoni tija yake katika nchi. Hilo moja Mhe. Mwenyekiti.

Lakini kwamba hawaingiziwi fedha ipasavyo ni suala moja, hio haihalalishi atakuja kutupa maelezo waziri ikifika zamu yake, lakini tukifika wakati wake Waziri wa Fedha pia atakuja kutwambia hapa, lakini nasema hiyo haihalalishi utendaji usioridhisha katika Wizara ya Afya kwenye maeneo mengi Mhe. Mwenyekiti. Nilipongeza yale maeneo machache sibakhili wa kupongeza kwa yale mambo tunayoyaona kuna jambo zuri linafanyika. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tunapokuja maeneo mengine hali inatisha.

Nianze na yale ambayo yalikuwa yametolewa ripoti na kamati. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 73 wa ripoti kamati inasema, "Kamati imeagiza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ya Maendeleo kulifuatilia suala la wizi wa magrili ya dirisha na mlango katika majengo yaliofanyiwa matengenezo kwa ajili ya Ofisi za Mkemia Mkuu wa Serikali huko Maruhubi ili hatimaye kuwabaini wanaohusika na kuchukuliwa hatua za kisheria".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesikitika na hili, kwa sababu hili limezungumzwa ndani ya Baraza hili na kama sikusahau Mhe. Hija Hassan mwenyewe ndiye aliyezungumza ndani ya Baraza hili. Sasa nilidhani ndio hayo niliyosema siku ile tulipokuwa tukiipitia ripoti ya mwanzo ya Ofisi za Viongozi wa Kitaifa kwamba mambo yakishatolewa taarifa tuone hatua tena sio maagizo yale kwa yale yanajirejea kila siku hiyo maana yake serikali haifanyi kazi imelala, ikiwa maagiuzo yale yale yanajirejea katika kila ripoto kwa kila mwaka ndio yale niliyosema tutafika tuko miaka miwili na nusu tuko nusu ya kipindi cha serikali hii ya Awamu ya Saba wananchi wanauliza lipi kubwa mliloliona? Kwa utendaji wa aina hii tutamaliza miaka mitano mingine patakuwa hapana cha kuripoti hapa ndio hayo ninayosema tukisharipotiwa tuone sasa utekelezaji.

Lakini ilizungumzwa hapa wakati wa bajeti nakumbuka Juni/Julai mwaka jana, leo tuko April linajirejea katika ripoti ya kamati maana yake mwaka mzima halikuchukuliwa hatua litafika tena

bajeti tuje tuzuiane vifungu humu kwa sababu wizara imeshindwa kuchukua hatua, kwa nini tunakwenda hivyo Mhe. Mwenyekiti. Sasa hili si la fedha nani anayefichwa au anayefichiwa wizi huu, ndio maana hatwendi Mhe. Mwenyekiti, niondoke hapo hili tunataka maelezo na kama hatuyapati kipindi hiki mana hapa kamati bahati mbaya hazina vufungu, lakini vifungu vinakuja miezi miwili *in shaa Allah* haviko mbali tukijaaliwa kutoka hapa tulipo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hili pia niulize Wizara ya Fedha au Wizara ya afya itakuja kutwambia kama ndio linaathirika kutokana na mipango mibovu ama vipi. Ukurasa wa 72 maoni ya kamati yanasema kwamba, kamati imeshauri Wizara ya Afya kutafuta namna ya kuondokana na malimbikizo ya deni la umeme katika Vituo vya Afya vya Pemba kikiwemo Kengeja na Bogoa. Wizara imekuwa ikilipa huduma ya umeme katika vituo vimngi vya afya kwa shilingi 80 elfu kwa mwezi kinyume na bajeti iliyokusudiwa shilingi 20 elfu kwa mwezi.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, kama kulipangiwa kwamba bajeti ya shilingi 20,000 kwa mwezi kwa kituo cha afya hii haioneshi kwamba tuko *serious*, mtu nyumbani kwake tu kwa mwezi haitoshi shilingi 20,000 ukipangie kituo cha afya 20.000 kwa mwezi tuko *serious* sisi? Kwa hivyo, wamepanga shilingi 20,000 wanatumia shilingi 80,000 hata kama unaweza ku-*survive* kwa shilingi 80,000 pia mimi naona watu wana miujiza mikubwa wanafaa tuwaombee dua waendelee na maarifa waliokuwa nayoh hayo.

Narudi pale pale Mhe. Mwenyekiti najiuliza, *priority* zetu ziko wapi. Kwa sababu wizara hii inayolalamika hivi safari za kupishana za watendaji hazina idadi, wakubwa wanagomba na hii imekuwa ni tabia katika wizara zetu wakubwa wanagombana kwa safari unalijiuliza hiyo ndio *priority* ya watendaji wetu, nilikuwa naomba niambiwe hili kwamba hivi ndio mipango yetu ilivyo kwamba shilingi 20,000 kwa kitu kila mwezi naomba maelezo katika hilo.

Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, pameripotiwa vile vile Hospitali ya Wagonjwa wa Akili. Hili ni aibu, katika watu ambao jamii ya watu wastaarabu inapaswa ipimwe kwanza ni vipi inatunza watu kama hawa, leo wagonjwa wa akili imekuwa hospitali ile kama vile inatembezewa bakuli tu, kutiwa rangi tunakumbuka sote hapa mpaka walikuja watu kutoka nje wakaja wakasaidia wamejikusanya. Lakini leo baada ya marekebisho yaliyofanyika tunaambiwa hata dawa zinashindwa kupatikana. Wagonjwa wa akili watakuwa laki ngapi katika nchi hii hata iwe dawa zao zinashindikana. Mana labda niambiwe katika nchi hii asilimia 10 wagonjwa wa akili kwamba katika milioni moja laki moja tunatembea na wazimu kichwanim nitasema hapo labda kweli tunahitaji madawa mengi kweli kweli, lakini wako wangapi hawa hata ikawa bajeti yake inashindikana hata kupata dawa katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, haya yameripotiwa katika ripoti ya kamati, lakini yako ambayo hayakuripotiwa naomba niyakumbushe haraka haraka. La kwanza wakati wa bajeti mwaka jana mimi mwenyewe Ismail Jussa Ladhu, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe nilihoji hapa juu ya utendaji wa Hospitali ya *MIOT* na malalamiko ya wagonjwa wetu wanaopelekwa kule, tukaibana Wizara ya Afya na ikatupa *commitment* hapa katika bajeti kwamba itatafakari na kuangalia hospitali nyengine.

Tulisema kwamba tatizo liliopo sio kama hospitali mbaya hapana, lakini kwamba imezidiwa na wagonjwa katika nchi ambazo zinajiweza kifedha kama nchi za Arabuni kwa hivyo wagonjwa

wetu wakipelekwa sisi wanakuwa hawa tena wanangoja mpaka ipatikane nafasi ndio wakaribishwe ndani, wanahamishwa katika vyumba tulisema hapa, nilitegemea nilione katika ripoti ya utekelezaji sikuliona Mhe. Mwenyekiti. Nasema sawa, sasa hivi tutapokea lakini tutakuja kukutana katika mwezi wa Juni/Julai nilikuwa naomba maelezo katika hili.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama vile hayo hayatoshi nilikuwa naomba kutoa maelezo kuhusiana na jengo la Kitengo cha Macho katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hili jengo ni bovu, bovu, bovu, ndio hilo nililosema pengine huku kupunguziwa kasma pengine watendaji wa Wizara ya Fedha nao hawaridhiki na matumizi ya wizara hii. Kwa sababu jengo hili tunaambiwa lilitengenezwa na likaingiziwa shilingi 130 milioni lakini mjenzi alipofuatiliwa kasema yeye kapewa shilingi 25 milioni kwa hivyo, kiasi alijenge vile alivyolijenga. Kwa sababu haiwezekani jengo likisiwe shilingi 130 milioni halafu utoe shilingi 25 milioni ukategemea utakuta jengo kama lilivyokuwa mwanzo haiwezekani hata siku moja, kwa hivyo matokeo yake ndio lile jengo lililokuwepo pale. Sasa hebu tupewe maelezo na waziri akija juu ya suala hili.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, tupewe maelezo kuhusu mambo ya ujenzi vile vile jengo la kitengo cha lishe Machomanne Chake-Chake. Naambiwa nalo linavuja lipo taabani. Vile vile namuomba Mhe. Waziri akija anisaidie hivi tushazungumza mara ngapi humu kwamba kifaa cha jenereta kinashindwa kupatikana kiasi kwamba taka zile ambazo nyengine ni sumu zinatupwa baharini badala ya kuharibiwa kwa utaratibu wa kisayansi ambao unaoeleweka. Naomba maelezo katika hili.

Lakini vile Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kwamba lile agizo lilizungumzwa mwaka jana katika bajeti ya mwaka jana kwamba na Pemba kuwe na utaratibu wa kuwa na Benki ya Damu inayoeleweka, pahala fulani inaekwa damu ili ikitokezea haja watu wasihangaike. Ule mgao unaofanywa kila mwezi kwa hospitali uwe pia kwa Pemba imefikia wapi, nilikuwa naomba limefikia wapi, naomba kupatiwa maelezo.

La mwisho kabisa katika Wizara ya Afya ni suala la bohari kuu ambapo ninarudi pale pale. Nimepongeza serikali kwa kuanzisha bohari kuu. Lakini hapa Mhe. Mwenyekiti, pana kitandawili. Bohari kuu ukenda dawa zipo Alhamdulillah si haba lakini Hospitali ya Mnazi Mmoja dawa hakuna. Ukiuliza Hospitali ya Mnazi Mmoja, nilikuwa namuuliza Mhe. Hija Hassan jirani yangu hapa, ananiambia ukiuliza wanakwambia kwamba hakuna, jee mumepeleka maombi ya dawa bohari kuu, wanasema hatujapeleka. Sasa kinachoelezwa hapa kwamba kuna mpango wa kumuhujumu mkuu wa bohari kuu aonekane kama kafeli katika kazi yake.

Ndio maana ukenda bohari kuu dawa zipo lakini ukija huku hospitali ya Mnazi Mmoja dawa hakuna, kuna nini hapo. Naomba Mhe. Waziri kama analijua atueleze hilo.

Na hivyo hivyo Mhe. Mwenyekiti, atueleze kuhusu dawa za ukimwi kwa sababu inasemekana dawa za ukimwi zina upungufu kwa sababu kumekuwa na wimbi kubwa la watu kutoka Bara kuja kupata matibabu hapa kutibiwa hapa, kwa hivyo bajeti yetu imekuwa hazitoshelezi katika dawa hizi. Naomba pia hili akija anisaidie. Mhe. Mwenyekiti, hayo yanahusu Wizara ya Afya.

Sasa kwa ufupi naomba niingie kwenye Wizara ya Elimu. Mhe. Mwenyekiti, samahani nimesahau suala moja mimi nilikuwa nilitaka kumuomba Mhe. Waziri wa Afya, mimi nimefanya

kazi na Mhe. Juma Duni katika Chama chetu cha Wananchi *CUF* alikuwa ni Naibu Katibu Mkuu wangu najua sana uwezo wake wa kufanya kazi, umahiri wake na kujituma kwake. Hebu leo atwambie kuna tatizo gani kwamba mama yule simuoni katika Wizara ya Afya. Zipo taarifa kwamba watendaji wake wanamkwamisha wanamuhujumu atwambie katika Baraza hili. Hili ndilo Baraza la kuisimamia serikali. Ikiwa Katibu Mkuu na timu yake wana vipa umbele vyao, wana safari zao, wana mambo yao mengine atwambie humu ndani tujue hasa. Maana yake kama si hivyo inaweza kuwa ile hadithi ya kwamba anayekamatwa na ngozi, sasa humu tutamkata waziri ndiye atakayekuja kuwajibika humu ndani. Kwa hivyo nilikuwa naomba akija hili anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninakwenda kwenye Wizara ya Elimu na sitaki kwenda kwa undani kwa sababu pengine nitachukua muda mkubwa sana sihitaji kufanya hivyo. Lakini yapo maeneo ambayo pia naomba maelezo.

Moja ni kuhusiana na hili ambalo limezungumzwa humu kwamba katika ukurasa wa 76 na 77 kuhusiana na suala la kukosekana uwiano katika walimu wanaosahihisha mitihani baina ya Unguja na Pemba. Ile takwimu iliyotolewa na sitaki nipoteze muda inatisha kwamba katika walimu karibu mia tatu unapata walimu hamsini kutoka Pemba, kwa nini iwe hivyo. Nchi yetu inaundwa na visiwa hivi na tumeondokana na zile siasa za zamani na tunataka tujenge msingi mpya wa sote tujione tuna haki sawa katika nchi yetu. Nilikuwa naomba atueleze hilo kwa nini linafanyika hivyo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba Waziri pia akija anisaidie mwaka jana tulipopitisha bajeti kuna fungu, sasa hivi haraka haraka halinijii nililipendekeza likatwe lipelekwe katika teacher center vituo vya kujiendeleza walimu. Ninataka kujua jee agizo lile limetekelezwa na kama limetekelezwa ni kiasi gani cha fedha kwa sababu bajeti inakuja tunataka kujua yale maagizo tuliyokuwa tumeyatoa mwaka jana yamefikia wapi Mhe. Mwenyekiti.
Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikuwa nimepata mshituko la madeni ambayo tunadaiwa katika Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) kwamba kuna malimbikizo ambayo yanaendelea na hata katika ripoti ya waziri hapa...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa umebakiza dakika 5.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Zinanitosha Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nije nipate maelezo juu ya deni hili ambalo linaonekana kulimbikiza kila siku kwa sababu badala ya kupungua, lile la mwaka wa nyuma halijalipwa na jengine linaendelea. Kwa hivyo tunataka kujua deni hili limefika wapi.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, niseme haya yalikuwa ni machache na moja nisije nikalisahau kila jimbo linasikitika na skuli zake na matatizo yake. Lakini mimi leo sitaki kuzizungumza skuli za Mji Mkongwe. Nataka kumwambia Mhe. Waziri hebu atupie jicho Skuli ya Kengeja.
Nimesimama kwa sababu tumetukanwa Baraza zima Mhe. Mwenyekiti, katika mtandao, siku hizi mawasiliano yamekuwa ni rahisi sana. Kumeekwa katika mtandao taarifa inaohoji Baraza zima la Wawakilishi kwamba wameshindwa kuiona Skuli ya Kengeja imekuwa kama mabanda ya kufugia ng'ombe na picha ya Baraza la Wawakilishi imeekwa katika mtandao, tumo katika kikao kwamba haya hatuyaoni na ile picha ya skuli pia ikaekwa.

Sasa mbali ya ile skuli ya sekondari ya ufundi ambayo imetajwa katika ripoti mwaka jana iliulizwa na mwaka imo tena, lakini kuna skuli ya sekondari ya Kengeja hali yake kutokana na ile picha inatosha kabisa ya kusikitisha. Hebu atupe maelezo kwamba Wizara ya Elimu imeshindwa kuiona na kama wameiona wana mpango gani wa kuinusuru skuli ile.

Sasa ya jumla Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumzia hizo dakika zangu zilizobakia pengine itakuwa ni 3. Kama nilivyosema tutakuja kuzungumza kwa urefu wakati wa bajeti. Lakini kipimo cha kufanikiwa mfumo wa elimu wa nchi yoyote na ufanisi wake ni matokeo ya mitihani. Kamati imesema imesikitishwa, wazazi wanasikitishwa, walimu wanasikitishwa, serikali inasikitishwa, Rais anasikitika, tunasikitika sote. Sasa atakayechukua hatua nani Mhe. Mwenyekiti.

Nilimsikia siku niliyemuuliza swali hapa sikupata nafasi lakini mwenyewe Mhe. Waziri alisema kwamba kunaandaliwa mkutano wa kitaifa ambao utakuja kutathmini suala hili. Nilikuwa naomba hili lifanyike kwa haraka Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tutafika tena kufanya mitihani tuje tupate matokeo mabaya zaidi kwa sababu matokeo ya mwaka huu ni mabaya zaidi kuliko ya mwaka jana, yale ya mwaka jana yalileta kasheshe sio ndogo katika nchi hii. Sasa ya mwaka huu yamekuwa ni mabaya zaidi kuliko yale.

Sasa nna wasi wasi na watakaofanya mwaka huu matokeo yake yatatoka mwakani yakawa ghasi zaidi, tuna tatizo gani Mhe. Mwenyekiti. Mimi naamini tunahitaji tuangalie mfumo mzima wa elimu. Nilikuwa nilete hoja binafsi kuhusiana na suala hili lakini niliposikia hii hoja ya mkutano, nikasema aah! Nitakuwa sitendi haki tutakuja kuzungumza hapa katika mkutano wa kitaifa,ambao nina hakika na sisi tutakuja kualikwa. Lakini tujitizame kuanzia mitaala, walimu wetu tunavyowapata, tunavyowasomesha, maslahi yao, majengo yetu, huduma, *sysllabus* zetu, vitabu vyetu vya kusomeshea. Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, ndani ya nchi moja kila skuli ina kitabu chake cha kusomeshea somo moja. Humu mfumo wa mchafu koge hauwezi kuleta tija katika elimu hata siku moja. Kila siku tutapata matokeo mabaya katika nchi yetu.

Kwa hivyo mimi nasema tujitazame sana kwa sababu mwaka jana, leo bahati mbaya muda sina nataka nizungumze kwa ufupi tu. Mwaka jana kuna wanafunzi ambao walifelishwa, mimi nasema wale walifelishwa sisemi kama wamefeli katika mitihani ya *NECTA*, lakini hawa hawa wanasomeshwa katika skuli hizi hizi wakenda kujisajili kufanya mitihani ya *Cambridge* katika kwenye skuli binafsi hapa Zanzibar, wengine wamefanya mitihani Arusha ya *Cambridge* wanafunzi wale wale wamepasi vizuri sana.

Sasa najiuliza mimi hivyo leo mitihani yetu sisi na mitihani ya *Cambridge* ipi iliyokuwa na viwango ukilinganisha na viwango vya elimu katika nchi husika. Na huku tulikotoka Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar tulikuwa tukifanya mitihani ya *Cambridge* kama nchi nyengine za Jumuiya ya Madola. Kwa hivyo nasema tunahitaji kuangalia masuala haya lakini pia na ufanyaji wa mitihani kama tunahisi *NECT* ni mzigo kwetu tuutuwe na serikali itazame kwa ujumla wake.

Na tunasema kama walivyosema kuwa wanataka kufanya mkutano nina hakika tutaalikwa tutakwenda kuyazungumza kwa urefu haya tupate ufumbuzi wa haya, lakini suala la mitihani tunawaonea na kuwatesa watoto wetu. Watoto wanahenyeka mwaka mzima sikatai yapo

mengine vishawishi mbali katika jamii kuna matatizo yake na yote hayo tutahitaji kuyatathmini hayo, lakini kwa yote hayo wapo watoto wanahangaika mwaka mzima kukabiliana na mtihani, yakitokea matokeo ya mtihani yanapotoka anamwagika hata ukimwambia kafanye mtihani anasema mimi sifanyi mtihani kwa hali hii.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa ninasema naomba maelezo katika maeneo hayo ili tuweze kuipokea ripoti hii. Nashukuru kwa kuchukua muda wako nakushukuru sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya mahiri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze waziri kwa ripoti yake nzuri na yenye ufanisi mkubwa. Kama tunavyojua katika sekta hii ya afya ni muhimu sana katika jamii yetu hasa kwa hapa Zanzibar, kwa sababu sekta ya afya ni tatizo kubwa sana linalokabili wananchi wetu na tatizo sugu.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Wizara ya Afya kwa juhudi yao kubwa waliyochukua kwa Ofisi ya Mkemia Mkuu jengo walililolifanyia ukarabati na kampuni ya Millenium ambayo ilishinda zabuni hiyo.

La pili Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha kabisa na kushangaza jengo hilo jipya hatimaye mpaka leo halina umeme wala fanicha. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa suala hili kweli tutakwenda wapi na tutafika wapi, jengo kama hili ambalo limetumia fedha nyingi ya serikali na hatimaye kwisha lakini mpaka leo halijafanikiwa ufumbuzi wa kulifungua na wananchi wetu kulitumia kwa ufanisi mzuri.

Tukitazama Mhe. Mwenyekiti, suala la Hospitali yetu ya pale Mwanyanya huu mwaka wa tatu au nne unaingia sasa haijafikia hatua yoyote ya kumalizwa hospitali ile. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii, kamati imeeleza ukweli kabisa na uwazi na kwa umahiri wao mzuri kabisa, naipongeza sana kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, wilaya zetu za Unguja na Pemba tatizo kubwa la hospitali linalokabili sasa hivi ni tatizo kubwa sana la tatizo la afya hasa suala la maji safi na salama, baadhi ya dawa muhimu na tatizo hilo limekuwa sugu katika hospitali zetu za hapa Unguja na Pemba. Mimi napenda kumshauri Mhe. Waziri kama tunavyojua serikali yetu kidogo fedha zake zipo chini lakini tusikae kimya tutafute wafadhili ambao wanaoweza kutusaidia haya madawa muhimu sana kwa sababu haya madawa ni maisha ya binadamu sote na bila ya dawa hizi nafikiri tutaishia pabaya kwa sababu wananchi wetu wanaumia sana na upungufu huu.

Tukitazama suala la upungufu wa madaktari, kwa kweli madaktari tunao kidogo sana na utakuta hata motisha zao au posho zao na maslahi yao ni madogo sana wanayopata. Unakuta madaktari wengine wanaondoka hapa wanakwenda kufanya kazi pengine. Mimi nitoe mfano mmoja tu mdogo.

Siku moja nilikwenda Tanzania Bara pale Hospitali ya Aga Khan nitamkuta Dr. Idrissa, ni *doctor* mzuri na ni *doctor* wa watoto lakini akaniambia kwamba maslahi yetu ya Zanzibar yapo

chini kwa nchi yetu, ndio hatimaye utakuta madaktari wale wanakimbilia Tanzania Bara. Sasa utakuta sisi wenyewe wananchi wa Zanzibar tunaumia kwa tatizo hilo kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, ukenda kwenye Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, kwa kweli wagonjwa hawa wanapata taabu sana, wanafika pale hospitali kwao hawapati huduma yoyote mpaka watoe shilingi elfu kumi ndio wapate tiba au wapate sindano. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa na tatizo gumu sana na kama tunavyojua wananchi wetu wa Zanzibar hali zao ni duni, wapo shida sana ya kuzipata hizi dawa na dawa hizi ni muhimu sana na ni dawa za utaalamu mkubwa sana.

Mhe. Spika, ripoti yetu imechambua mambo mengi sana. Ukitazama sekta ya afya. Kwa kweli ukitizama vituo vyetu vya afya hasa kule Pemba utakuta vyengine hata uwezo wa kulipia umeme wa elfu thamanini kwa mwezi kwa kweli wanashindwa. Utakuta hatimaye vituo vyengine vya Pemba havina hata umeme. Lakini ukitazama bajeti ya wizara ni elfu ishirini kwa mwezi, kwa kweli hii pesa kidogo sana kwa zahanati zetu kulipa na hatimaye ile hospitali inashindwa kulipia gharama za umeme.

Mimi niwapongeze sana ndugu zetu wa KMKM pale kituo chao cha afya kipo Kibweni pale, kwa sababu huduma zao unaridhika kabisa na ukitazama kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na wote pamoja na kikosi cha KMKM hata jenereta pale kama umeme unapozimika basi wanakuwa nao umeme wa kutosha kabisa ili wananchi wapate matibabu ya uhakika na salama kabisa.]
Kwa hivyo napongeza sana ndugu zetu wa KMKM kwa juhudi zao kubwa wanazochukua kwa wananchi wetu kufika pale kituoni kupata huduma nzuri kabisa.

Lakini pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kuliona hili kwa akinamama waja wazito. Mhe. Rais alitoa tamko hawa akinamama waja wazito washughulikiwe bila ya malipo, lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa mjamzito akenda hospitali anatakiwa awe na shilingi elfu thalathini mkononi. Kitu ambacho ambacho kinarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. Kwa sababu bajeti yao wanayopangiwa sijui kama inakuwa ni ndogo au inakuwa inatosha lakini kwa kuzingatia zaidi tungeomba bajeti hii iwe nzuri na ya uhakika. Kwa sababu hii inagharimu maisha ya watu na wananchi wetu. Kwa hivyo wanapofika pale waja wazito wanakuwa wengine hata ile pesa ya kulipia hawana. Lakini Rais wetu ninampongeza sana ka kutoa tamko hilo kwamba waja wazito watibiwe bila ya malipo.

Mhe. Mwenyekiti, hili Mhe. Waziri naomba anipe ufafanuzi mzuri kabisa wa uhakika ili kujua hawa wajawazito wanakwenda pale na malipo au waende bila ya malipo, kwa sababu wananchi wetu ni maskini kwa hali zao ni duni, wanakwenda pale wanadhalilika vibaya wanakuwa sasa wanamtafuta mwakilishi au mbunge yupo wapi, wakati ule hali ni ngumu na hali zao sio nzuri. Kwa kweli inasikitisha sana. Hivyo naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi mzuri kuhusu hili kuhusu hasa wajawazito.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama katika nchi yetu hivi sasa tatizo kubwa la waja wazito kupoteza maisha yao, asilimia karibu 49 hawa wanajifungua hospitali lakini asilimia 51 wanajifungulia wapi hawa. Hilo pia tuliangalie vizuri Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wanajifungua majumbani kabisa kwa sababu hali zao ni duni kabisa, unakuta hata uwezo wa kwenda hospitali

hawana. Ndio ripoti ya kamati tukaona hapa kuna asilimia 49 tu wanaojifungulia hospitali kwa sababu hawana uwezo, hawa asilimia 51 wanajifungulia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mmoja mzuri ambao nimeuona wiki moja iliyopita nyuma kutoka jimboni kwangu, mzazi kakaa nyumbani kwa sababu muda wote hana fedha ya kulipia hospitali ya Mnazi Mmoja, hatimaye inakwenda gari ya ambulance anajifungulia kwenye gari. Ukimuuliza kwa nini hujatoa taarifa, anasema mimi sina uwezo wa kulipa kule. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hili suala ni zito. Hivyo Mhe. Waziri anipe ufafanuzi mzuri kabisa wa kuridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi ni jengo la chanjo Machomanne lina idadi kubwa ya wafanyakazi lakini jengo hili linavuja na hali yake ni mbaya sana. Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, pia anipe ufafanuzi kuhusu jengo hili la Machomanne.

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja kama tunavyojua ni hospitali kubwa sana na inachukua wananchi wote kutoka Pemba na Unguja. Lakini cha kusikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hata ile mashine ya kuchomea zile taka basi hamna, zile taka zitiwa bahari kule kunasababisha uchafu mkubwa kwa ajili ya afya ya wananchi wetu na mazingira kwa ujumla.

Sasa na hili nalo Mhe. Mwenyekiti, ni suala muhimu sana kwa Wizara ya Afya ilichukulie kipa umbele kabisa kwa ajili ya mashine hii ya kuchomea taka kwa ajili ya hospitali yetu kubwa ya rufaa.

Mhe. Mwenyekiti, hii ripoti yetu kwa kweli tuwape pongezi hii kamati yetu ya Ustawi wa Jamii. Ukitazama jambo jengine la wazi kabisa kwenye Hospitali ya Wete na Mkoani Pemba, hivi sasa hata gari za kubebea wagonjwa hamna. Tangu gari walizokuwa nazo za mwaka 1990, kweli Mhe. Mwenyekiti, ni miaka 20 zaidi gari hiyo itakuwa inakwenda kweli. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwa Mhe. Waziri kwa haya magari ya wagonjwa wetu ambao yanawasaidia wananchi wetu wa Pemba kule.

Tukichukulia mfano mdogo tu kama Jimbo letu la Bububu kuwa hivi sasa tuna gari ya wagonjwa ya *ambulance* na pia Jimbo jengine la Tumbatu lina gari. Hivyo mimi naomba majimbo yote yaige mfano kama huu wawe na gari zao za ambulance kwa ajili ya wananchi wao ingekuwa ni jambo zuri sana.
Mhe. Mwenyekiti, kidogo naomba nijikite kwenye ustawi wa jamii wanawake na watoto. Hizi kwa kweli kesi za ubakaji hazipatiwa ufumbuzi mpaka leo. Kesi zimekuwa nyingi, watoto wadogo kudhalilishwa wakiwemo wanawake na wadogo kupitia chini ya umri wao kimaumbile. Mpaka leo hatujasikia ufumbuzi wao wa tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, hawa wenye matatizo haya hawajapewa bado adhabu ya kutosha. Kama wangepea adhabu ya kutosha hawa hili tatizo lingeondoka kabisa. Mtu akikamatwa na kesi hii ya ubakaji basi angefungwa hata miaka kumi, saba na kwenda mbele, nafikiri tatizo hili lingeondoka kabisa. Hizi kesi hivi sasa ni nyingi sana na kila siku tunapata kesi zilizokuwa za maajabu ajabu.

Hili tatizo la ajira kwa watoto Mhe. Mwenyekiti, ni hali ngumu ya maisha. Watoto wanaacha kwenda skuli kusoma kwa ajili hawana uwezo, hawana ada ya skuli, hawana nauli ya kwenda skuli. Kwa hivyo wanajikita kwenye suala la ajira. Hivyo ningeomba wizara hii iwape elimu hawa watoto ya kutosha kabisa kuwa elimu ni muhimu sana kwa maisha ya kesho.Kwa hivyo ningeomba Mhe. Mwenyekiti, na hili pia wizara ilichukulie kwa makini kabisa kwa ajili ya watoto hawa wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii pia naishauri sana iwe na Mwanasheria maalum wa kesi za ubakaji. Pia wizara hii haina Mwanasheria au Msimamizi Mkuu hasa wa kitengo hiki kikawa hakina ubabaishaji wowote, kikawa ni mahiri kabisa. Tatizo linapotokezea inakuwa Mwanasheria wake awepo ili kufanya kesi hiyo kuwa rahisi kabisa na kwisha bila ya tatizo na kupata adhabu ili asirudirue tena huyo mtu.

Mhe. Mwenyekiti, nijikite kidogo kwenye suala la elimu hapa. Hii Skuli yetu ya Sekondari hivi cha kusikitisha zaidi kuna eneo la wazi ambalo kwa sasa Mhe. Mwenyekiti, linatumika kama jaa. Eneo hilo hilo upande mwengine linatumika kama ni gereji ya kutengenezea magari.

Kwa hivyo hili naliomba Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wetu wanapata taabu kwa maeneo kama haya, hivyo yanashughulikiwa mambo ya maajabu ajabu na yasiyokuwa mazuri kwa skuli yetu hii ya sekondari.

Pia niseme Mhe. Mwenyekiti, katika Skuli ya Jang'ombe halikadhalika. Nilitembelea pale nikaja nikaona Manispaa imeanzisha jaa pale. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho cha kusikitisha sana. Hapa ni pahala pa wanafunzi wetu kusoma, mazingira mazuri ya afya lakini leo unakuta taka zinatupa bila ya mpangilio wowote.

Pili maegesho ya magari. Eneo la skuli limekuwa sasa linaegeshwa magari, sasa sijui walinzi wanachukua pesa kwa kulinda magari yale. Kwa hivyo na hili ninataka Mhe. Waziri pia aliangalie kwa makini kabisa suala la skuli zetu hizi.

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti, la kumalizia, naomba kwa unyenyekevu mkubwa hawa walimu wetu wanaosomesha watoto wetu maskulini mafao yao madogo. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba pia wapewe posho hawa walimu kwa sababu hali zao ni duni, kwa hivyo inakuwa kwa kweli inawapa shida sana kukidhi mahitaji yao ya kimaisha ya kila siku. Hawa ni walimu ambao wanafunza watoto wetu kwa leo na kesho kuwaweka watoto wetu wawe wazuri zaidi. Kwa hivyo naomba lifikiriwe sana.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*).

(Saa 1.40 Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 16/04/2013 saa 3.00 asubuhi)